ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Tisa - Tarehe 15 Juni, 2016

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi Maji, Nishati na Mazingira kwa mwaka 2016/2017, naomba kuwasilisha.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi: Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima naomba kuweka mezani, Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 121

Vikao vya Baraza kutofanyika Pemba

Mhe. Mussa Foum Mussa – Aliuliza:

Kwa muda mrefu sasa vikao vya Baraza la Wawakilishi havijafanyika huko Pemba kwenye ukumbi wake ulioko Wete.

(a) Je, suala hili ni kweli.

(b) Kama ni kweli ni sababu zipi zinazopelekea vikao vya Baraza kutofanyika Pemba.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo ya Pili wa Rais - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mussa Foum Mussa Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Kiwani swali lake Nam. 121 lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwa muda mrefu vikao vya Baraza la Wawakilishi havijafanyika Pemba kwa sababu ya upungufu wa vifaa na uchakavu wa jengo lenyewe. Kutokana na hali hiyo haikuruhusu kufanyika mikutano ya Baraza katika jengo hilo.

Mhe. Spika, jengo la Baraza la Wawakilishi Pemba, lilisita kutumika kwa Mikutano ya Baraza la Wawakilishi tangu mwaka 2006, ili liweze kutumika tena linahitaji gharama kubwa ya kulifanyia mabadiliko makubwa ili liendane na mifumo ya kisasa ya uendeshaji wa shughuli za Baraza Pemba.

Mhe. Spika, hata hivyo naomba kutanabahisha kuwa utaratibu nchi nyingi Duniani hasa za *Commonwealth*, Mabunge hufanya mikutano yake katika eneo moja la nchi. Hivyo kwa upande wetu Zanzibar, tukizingatia uwezo wetu wa kiuchumi, kwa sasa ni vyema tukaendelea kuimarisha jengo letu la Chukwani ili liweze kukidhi vigezo na kutoa huduma bora. Aidha, umuhimu wa kulikarabati jengo la Pemba utaendelezwa mara pale hali ya kifedha itakaporuhusu.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa amekiri kwamba jengo la Pemba kwa muda mrefu sana vikao havijafanyika na kwa kuwa amesema inahitajika ipatikane gharama kubwa sana. Je, anatueleza kwamba hivyo vikao vitachukua muda mrefu sana havitofanyika kwa sababu ya gharama za kutengenezea ukumbi huo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo ya Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwa hali yetu ya kifedha hususan kwa mwaka huu na kwa sababu hatukuweka fedha hizo za matengenezo kwenye bajeti ya mwaka huu na kwa kuwa kwa paa peke yake zinahitajika 396,000,000 licha ya matengenezo mengine. Wakati huo huo Mhe. Naibu Spika, wewe ni shahidi na mimi ni shahidi kwamba Baraza letu hili humu tulimo ndani yamo matengenezo muhimu yanahitajika ikiwemo *echo* na mengine. Kwa hivyo kama nilivyosema kwa sasa ni vizuri tukamalizia kuliimarisha hili ambalo tunalitumia kwa sasa na pale hali itakapokuwa nzuri kifedha tukaweza kushughulikia na ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Pemba. Hata hivyo, tumeanza matengenezo madogo

madogo kule Pemba kutokana na hali ya uwezo wetu. Kwa hivyo tabaan itachukua muda ili tuweze kukamilisha utengenezaji huo.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi naungana na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kutuamsha salama, ninamshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Kutokana na maelekezo mbali mbali yanayotolewa juu ya ukumbi na gharama kubwa ambayo ipo, je Waziri ameangalia vipimo ikiwa gharama zitakuwa kubwa je, si bora ukatengenezwa ukumbi wa kisasa ambao unaendana na wakati kuliko kutoa gharama kwa ukumbi ambao labda umeshapitwa na wakati na mchakavu kwa gharama kubwa zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo ya Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Suleiman Sarahangi Mwakilishi wa Chake Chake ambae hapendi kuitwa jembe lakini kwa upande mwengine ni jembe swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kujenga ukumbi wa kisasa gharama zake ni kubwa zaidi kuliko matengnezo ya ujenzi wa ukumbi wa Mtemani. Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, ukipima hasa gharama za uendeshaji ni vizuri tukawa na kituo kimoja cha kuendeshea shughuli zetu za Baraza. Lakini kwa sababu ya utamaduni wetu tumezoea kufanya Baraza hapa Zanzibar na wakati mwengine kufanya Baraza Pemba. Kwa hivyo bado dhamira ya Serikali ni kulifanyia ukarabati mkubwa jengo la Pemba ili huko mbele liweze kutumika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri mtaalam, naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Kwa kuwa utaratibu wa kufanyika vikao Pemba na Unguja ulianzishwa na viongozi wetu waliotangulia na walikuwa na sababu zao, je tunawaenzi vipi viongozi wetu hao juu utaratibu waliouweka.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo ya Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, ni kweli utaratibu ulianzishwa na viongozi wetu waliotangulia na kama ninavyoeleza katika majibu yangu ya awali, kuwa bado dhamira ya serikali ni kuendeleza kulifanyia ukarabati jengo hilo la Pemba ili liweze kutoa huduma bora kwa wajumbe wetu. Na nimuhakikishie Mhe. Jaku kwamba bado tutaendelea kuenzi vitendo vyote vyema vilivyofanywa na viongozi wetu ili kupiga hatua katika shughuli zetu za maendeleo katika nchi yetu.

Nataka nimuhakikishie kwamba bado dhamira ya serikali ni kulitengeneza jengo lile pale hali ya kifedha itakapokuwa nzuri, kwa sasa sote tunaelewa hali yetu. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Nam. 109

Kupanda kwa Kodi ya Income Tax kwa wafanyakazi

Mhe. Hamza Hassan Juma : (Kny. Mhe. Yussuf Hassan Iddi) - Aliuliza:

Kwa kuwa wafanyakazi wa Serikali wanapaswa kulipa kodi kwa mujibu wa Sheria kupitia mishahara yao, kodi ya *(Income Tax)* hiyo imepanda sana ukilinganisha na kipindi ambacho mishahara inatengenezwa katika taasisi husika kabla ya kitengo cha mishahara (*Payroll*) cha Wizara ya Fedha kuanzishwa.

a) Je, ni kanuni *(formular)* gani wanayotumia kitengo cha *Payroll* kukata kodi ya *income tax* kwa wafanyakazi wa Serikali.
b) Je, ule utaratibu wakutumia jadueli *(schedule)* inayotoka Idara ya Kodi ya Mapato *(Income Tax Department)* haupo, na kama haupo ni sababu gani zilizopelekea utaratibu ule kusitishwa.
c) Tokea kitengo cha *Payroll* kuanzishwa kodi ya *income tax* kwa wafanyakazi imekuwa kubwa na kuwaumiza wafanyakazi, je Serikali inalijua hilo na hatua gani mmechukua kurekebisha hali hiyo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mhe. Yussuf Hassan Iddi Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni swali Nambari 109 lenye vipengele (a), (b) na (c) lakini kwanza naomba nitoe maelezo ya jumla.

Mhe. Naibu Spika, Kitengo cha Kusimamia Mishahara chini ya Wizara ya Fedha kimekuwepo kwa miaka mingi sana sasa, kikihusika na kusimamia malipo ya mishahara kwa Wafanyakazi wote wa Sekta ya Umma. Kazi hii inafanywa kwa kutumia Programu maalum ya TEHAMA yenye orodha ya Wafanyakazi wote, kiwango chao cha mshahara, mikopo na mikato mbalimbali pamoja na taarifa nyengine muhimu kwa kila mfanyakazi.

Mhe. Spika, kwa upande wa Kodi ya Mapato, ni vyema ieleweke kuwa tofauti na kodi za ununuzi wa bidhaa, kiwango cha kutozea Kodi hii huongezeka kulingana na kipato cha muhusika. Wakati watu wenye kipato kisichozidi

shilingi laki moja na hamsini elfu kwa mwezi kwa sasa wamesamehewa kodi hiyo, kiwango cha chini cha kodi kwa sasa ni asilimia 13 na kiwango cha juu ni asilimia 30. Huu ndio utaratibu wa kawaida kwa kodi ya mapato kuongezeka kwa kutegemea kipato (*progressive*). Mabadiliko ya kuongeza mishahara ya wafanyakazi hupelekea kubadilisha Jadueli ya kutozea kodi na hivyo kuwa na athari katika kiasi cha kodi ya mapato kinacholipwa na mfanyakazi. Katika hali ya kawaida, haitegemewi kuwepo na tofauti ya Kodi ya Mapato kwa wafanyakazi wanaolingana kipato.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya jumla naomba kujibu swali nambari 109 lenye kipengele (a, b, na c)kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, katika kukata kodi ya mapato inayotokana na ajira, Kitengo cha Mishahara *(payroll*) kilichopo Wizara ya Fedha na Mipango kinatumia Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004, kifungu 81(1) ambacho kimempa Waziri wa Fedha uwezo wa kutegeneza Jadueli (*Tax Schedule*), ambayo ndio inayotumika kutoza kodi hiyo.

(b) Mhe. Naibu Spika, bado utaratibu wa kulipisha kodi ya Mapato kwa kutumia Jadueli ya Kodi upo na ndio unaotumika hadi sasa.

(c) Mhe. Naibu Spika, kuwepo kwa Kitengo cha Kusimamia Mishahara hakuathiri kiwango cha Kodi ya Mapato na kama nilivyoeleza hapo awali, kiasi cha kodi kinaamuliwa kwa kuzingatia kipato cha mtu na kiwango kilichowekwa kwa maana ya *tax rate.*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, ninamshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa ufafanuzi na majawabu yake hayo aliyoyatoa. Pamoja na hayo nilikuwa nataka anisaidie tu katika swali hili la nyongeza kwamba kama alivyosema ili mkato wa kodi ya mfanyakazi au wa mtumishi wa umma inapotokezea marekebisho sheria au kanuni imempa mamlaka waziri kuweza kutoa jadueli ya mkato huo. Sasa swali langu liko hapa kwamba kwa kuwa Baraza la Wawakilishi linapopitisha bajeti linakuwa tayari limeshaidhinisha pamoja na yale makusanyo ya kodi yote kwa mwaka husika. Sasa swali langu je, mfano kama hawa wafanyakazi ambao serikali imetangaza kwamba wataongezewa mshahara kima cha chini na wakati huo utakuwa ni mwezi Aprili, sasa je, huu utaratibu hapa utakuwa vipi ili ile kodi ya Serikali ipatikane kutokana na lile ongezeko ambalo litaongezeka baada kuongezeka hicho kima cha mshahara.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, tunachotarajia katika kupunguza kiwango cha kodi kwa kima cha chini hakitaathiri mapato ya jumla na hii itatokana kwamba tumepunguza kima cha chini lakini wale wa vima vya juu mapato yataongezeka. Kwa hivyo yanapoongezeka na kupungua matarajio yetu yata-*equalize* kwa hivyo haitaathiri ile sheria ambayo tayari tumeipitisha ya kodi ya mapato.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Fedha kujibu swali la msingi. Serikali imekusanya kiasi gani kwa mwezi na kwa mwaka, wakati tukishuhudia *income tax* hiyo hivi sasa katika vituo vya hospitali, madawa hamna. Ngojea nirudie tena Mhe. Waziri naona kama hunipati vizuri, serikali imekusanya kiasi gani kwa mwezi na kwa mwaka kupitia *income tax*.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku kanuni zinakukataza kusoma, kama unauliza muulize moja kwa moja Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Haniskikii Mhe. Naibu Spika, ndio nikainamia hii spika mimi. Mhe. Waziri *income tax* imekusanya kiasi gani kwa mwezi na kwa mwaka na wananchi wanafaidika vipi na *income tax* hiyo wakati vituo vyote vya hospitali hivi sasa hakuna dawa? Ukizingatia kwa wananchi hawa ndio wanaolipa kodi.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na kima tunachokusanya kwa mwezi na mwaka naomba nimpatie kwa maandishi. Lakini wananchi wanafaidikaje na kodi inayokusanywa na serikali, kwa sababu kodi ya mapato kwa maana ya *personal income tax* ni sehemu ya mapato ya serikali. Kwa sababu ni sehemu ya mapato ya serikali kwa hivyo huduma zinazotolewa na serikali zinategemea mapato hayo ya serikali. Ikiwa huduma ya elimu, ya afya, maji safi na salama zote hizo zinategemea mapato ya serikali. Lakini pamoja na mishahara yetu ya wafanyakazi, Waheshimiwa Wawakilishi yote yanatokana na kodi hiyo.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Fedha na mimi nataka niulize kwamba kwa kuwa kwa mwaka huu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Magufuli alipunguza asilimia kwa kodi ya wafanyakazi. Kwa vile Zanzibar ninahisi mishahara yetu ni midogo kwa wafanyakazi wetu, je serikali haioni muhimu wa kuondoa kodi kwa wafanyakazi wake.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa rudia swali.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Kwa sababu mwaka huu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika sikukuu ya wafanyakazi alipunguza asilimia ya *income tax* kwa wafanyakazi na sisi kwa kuwa wafanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar mishahara yao ni midogo je, serikali haioni umuhimu wa kuondoa kodi moja kwa moja kwa wafanyakazi wake.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, kama ilivyofanyika kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupunguza kodi kwa wale wafanyakazi wa kima cha chini na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nayo imefanya hivyo hivyo, na sisi tumepunguza kwa kasi kubwa zaidi kutoka asilimia 12 hadi asilimia 9. Hii imefanywa makusudi kuwapunguzia wananchi hasa wale wa kipato cha chini makali ya maisha, lakini kodi ndio inayoendesha shguhuli za serikali. Kwa hiyo, kuiondoa kodi kabisa kabisa hakuna nchi yoyote inayofanya hivyo, kwa sababu kuondoa kodi za serikali ni kuinyima mapato serikali na kwa namna hiyo kuondoa uwezo wa serikali kutoa huduma kwa wananchi wake.

Nam. 106

Kupanda kwa Bei ya Vyakula

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) (Kny: Mhe. Yussuf Hassan Iddi) - Aliuliza:-

Kwa kuwa bei za bidhaa muhimu za chakula kama unga, sukari na mchele zipo juu licha ya msamaha wa kodi wanaopewa waingizaji wa bidhaa hizo.

a) Je, serikali imeliona hilo na hatua gani zimechukuliwa.

b) Tunaelekea kwenye mwezi mtukufu wa Ramadhani je, serikali imejipangaje kuona kwamba wafanyabiashara hawapandishi bei za vyakula.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 106 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, serikali imeliona suala hilo, na napenda kuwaeleza wananchi kuwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inafanya juhudi kubwa za kusimamia suala zima la bei hasa bidhaa muhimu

ikiwemo, mchele, unga wa ngano na sukari ili kuhakikisha hakutokei upandaji wa bei usio wa lazima.

Aidha, bei za chakula muhimu kama vile unga wa ngano, sukari na mchele zimepanda ingawa si kwa kiwango kikubwa, hali hii imetokana na kupanda mara kwa mara dola na kuongezeka kwa gharama nyengine za biashara zikiwemo kuongezeka kwa bei ya ununuzi wa bidhaa hiyo, bei ya upakizi, kuchelewa kwa ushushaji wa mizigo bandarini na gharama nyenginezo.

Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa na wizara ili kuondosha tatizo hili, ni kwamba wizara ilifanya mazungumzo na Shirika la Bandari pamoja na Jumuiya ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Wakulima (*Zanzibar Chamber of Commerce Industry and Agriculture)* ili kutafuta ufumbuzi wa suala hili.

(b) Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masomo inaendelea kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara juu ya uwepo wa bidhaa muhimu za chakula kwa ajili ya mwezi mtukufu wa Ramadhani zikiwemo unga wa ngano, tende, sukari na mchele na kuhakikisha kuwa vinaingizwa nchini kwa wakati na vinapatikana kwa bei nafuu ili kuhakikisha kuwa hakutakuwepo kwa upandaji wa bei kubwa ambao utaweza kuleta madhara kwa watumiaji.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Naibu Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Biasha, Viwanda na Masoko; kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, hivi sasa tumeshuhudia kwamba pamoja na upandaji wa bei wa bidhaa mbali mbali hususan mchele, sukari na unga wa ngano, lakini nasema kwamba serikali imejitahidi kudhibiti hilo. Lakini kwa kuwa bei ya mchele asilimia kubwa tunaagizia mchele kutoka Tanzania Bara na Tanzania Bara mchele umeshuka bei mpaka 1300 au 1500.

Je, wizara inachukua hatua gani za kuwaambia wenye maduka waachane na kuuza mchele 2300 au 2400 ili kuwapunguzia ukali wananchi wetu wakati mchele wao kutoka Bara wanapata rahisi hadi hapa.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, ni kweli wafanyabiashara wanachukua mchele kutoka Bara na bei za mchele kutoka Bara zimepungua kidogo, lakini tukumbuke kwamba mchele unapotoka Bara mpaka ukafika Unguja kunakuwa na gharama ya usafirishaji. Kwanza

usafrishaji kutoka Mikoani lakini pia usafirishaji wa kutoka Dar es Salaam bandarini mpaka kufika Unguja. Kwa hiyo, bado gharama zinakuwa vile vile kubwa kwa sababu ya usafirishaji, lakini pamoja na hayo tutazungumza na wafanyabiashara kuona kwa kiasi gani tunaweza kusaidiana ili kuzipunguza zile bei zilingane na hali halisi ya wananchi wetu.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Naibu Spika, suala langu ni kwamba uzoefu wa wafanyabiashara wa Zanzibar wanapandisha bei ikiwa kitu kimo ghalani tu baada ya kuadimika kwa muda mfupi. Je, serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha vile vilivyomo ghalani ambavyo vimenunuliwa kwa bei nafuu ili kuhakikisha wafanyabiashara wetu wadogo wadogo, kwa sababu biashara hizi zinatoka kwa tajiri huko alikokwenda kununua, zinakuja kwa mfanyabiashara mdogo. Lakini wafanyabiashara kawaida yao wakisikia kitu kimeadimika wao wanapandisha bei. Je, serikali ina mpango gani wa kuzuia utaratibu wa upandishaji bei kiholela.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, ni kweli wafanyabiashara wakati mwengine hutumia mbinu hizo pale wanapoona bidhaa imeadimika, lakini nichukue mfano wa kipindi hiki kabla ya mwezi wa Ramadhani tulitembelea maghala yote yanayowekwa vyakula vyote muhimu kwa ajili ya mwezi wa Ramadhani, na tulikuta kwamba maghala mengi yameshaagiza vyakula muda mrefu na vimo katika maghala. Jambo moja ambalo tumekubaliana kwamba vile vyote ambavyo vimeagiziwa kabla ya mwezi wa Ramadhani inakuwa utaratibu mzuri wa kodi waliyopewa hawana ruhusa ya kupandisha bei, kwa sababu hamna sababu ya kupandisha bei. Lakini kuna bidhaa ambazo zimekuja baada ya mwezi huu wa Juni hizo zitaweza kupandishwa bei.

Mhe. Naibu Spika, lakini la pili niseme kwamba tunafuatilia wafanyabiashara na tunakwenda nao sambamba kipindi hiki na ili kuimarisha zoezi zima la kuangalia bei wizarani kwetu itabidi tuagizie kifaa kimoja cha kitaalamu cha kutuwezesha kutwambia bei zinavyobadilika kwa kila siku. Hiyo itatuwezesha kujua bei za biashara hasa vyakula muhimu kama unga wa ngano, mchele na sukari zinakwendaje katika soko. Mara nyingi husema kwamba bei zimepanda nje lakini tutakuwa na uhakika sasa wa kujua bei zikoje ili kuweza kuweka bei elekezi kwa wananchi wetu ambao wanatumia bidhaa hizo.

Mhe. Viwe Khamis Abdallah: Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kwa kunipatia fursa hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza. Mhe. Waziri kuna baadhi ya wafanyabiashara Pemba huwaongezea wananchi hasa wana CCM bei za vyakula. Je, wizara yako wanalijua hilo, na kama wizara

yako wanalijua hilo ni hatua gani ambazo zimechukuliwa katika kulishughulikia tatizo hili.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, suala la Pemba ni suala tofauti na hapa Unguja, kwa sababu Pemba kuna mchafuko wa kisiasa, wanasiasa wanatumia nafasi hii ya mambo ya kisiasa kuwadhulumu wananchi wetu na hasa wanachama wa Chama cha Mapinduzi. Kwanza hiyo Mhe. Naibu Spika si tabia nzuri hata kidogo kwa sababu tusichanganyishe siasa na mambo mengine ya maendeleo yanayohusu wananchi.

Lakini pia wizara yangu imesikia habari hizi kama kuna wafanyabiashara kwanza wanawazuia hawawauzii bidhaa wanachama wa CCM, lakini pia wanapokuwa wanawauzia kule ambapo wanalazimishwa kuuza wanapandisha bei bila ya kufata bei elekezi ambayo tumewapa. Kwa hiyo, ningependa niwahakikishie tu kwamba taarifa hizi nimezipata na Wakuu wa Wilaya wanachukua hatua. Lakini pia niseme kama Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko tutafunga leseni za wafanyabiashara. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, safari hii tukifunga leseni hatuzifunguwi kwa mwaka mzima. Huko nyuma wanafungiwa na kufunguliwa lakini safari hii Mhe. Naibu Spika ili kuwapa adhabu na onyo kali tutazifunga kwa mwaka mzima, wasubiri mwaka unaokuja. Ahsante Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Nam. 25

Upatikanaji wa Dawa Vijijini

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kabla sijajibiwa swali langu ningemuomba Mhe. Naibu Waziri nikamkabidhi orodha kidogo niliyokuwa nayo ya dawa zinazohitajika ili akazifanyie kazi.

Hospitali zinazotoa huduma kwa wananchi vijijini upatikanaji wake wa dawa umekuwa siyo wa uhakika na kuleta usumbufu kwa wagonjwa.

a) Kwa nini wizara inashindwa kupeleka dawa kwa wakati na kuwaumiza wanyonge wa nchi hii.
b) Kwa kuwa dunia ya leo ni ya Sayansi na Teknolojia inakuwaje kituo cha afya kutumia dawa hadi zimalizike bila ya kupatiwa mgao mwengine wakati matibabu ndio uhai wa binaadamu.

c) Ni lini Serikali itahakikisha imepanga mipango yake kwa kufuata mipango ya matumizi na mahitaji ili wananchi wanufaike na mgao wa dawa badala ya kwenda hospitali bila ya kupatiwa dawa zenyewe.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Naibu Waziri uje ujibu swali tu basi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, sikuliondoa swali mimi nilisema tu nimpe orodha ya dawa zinazohitajika katika jimbo langu ili serikali itoe jawabu.

Mhe. Naibu Spika: Chengine wewe hapo unatakiwa uulize swali lako tu, hilo jengine litafanyiwa kazi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hewallah Mhe. Naibu Spika,

Mhe. Naibu Spika: Sawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 25 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Afya kupitia Bohari Kuu ya Dawa inao mfumo maalum wa usambazaji wa dawa ambapo kituo cha afya pamoja na hospitali zinaagiza na kupelekewa dawa kila baada ya kipindi cha miezi mitatu (yaani kila robo mwaka). Mahitaji ya dawa yanafanywa na wafanyakazi wa kituo husika kwa kuangalia idadi ya wagonjwa na maradhi yanayowasumbua zaidi wananchi katika eneo husika. Licha ya kuagiza kila robo mwaka, lakini idadi ya dawa wanazoomba na kupatiwa ni kwa ajili ya matumizi ya miezi 6. Yaani wakati wanapeleka maombi yao bado wana dawa za miezi 3 inayofuata inaitwa *buffer stock*. Hali hii inakifanya kituo kisikose kabisa dawa.

Mhe. Naibu Spika, tatizo kubwa linalojitokeza ni uchache na uhaba wa dawa katika Bohari Kuu ambayo inasababishwa na uhaba wa fedha zinazopatikana kwa ajili ya ununuzi wa dawa zinazohitajika kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na Serikali. Hali hii inawalazimu watendaji wa bohari kugawa baadhi ya dawa chini ya kiwango kilichoombwa na kupelekewa dawa hizo kuisha kabla ya mgao mwengine. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana pamoja Mhe. Naibu Waziri kutojibu swali la msingi naomba kuuliza swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Ni robo gani ya mwaka ukizingatia mnazotoa dawa wakati wananchi wa Jimbo la Paje tokea Oktoba kuanza uchaguzi mpaka muda huu hawajapata dawa, na ukizingatia kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ni haki yetu kupata matibabu na hivi sasa kupitia kwa mwakilishi wao na maduka ya madawa ndio wamepata dawa hizo tokea Oktoba mpaka muda huu hawajapata.

b) Je, ni lini wananchi watarajie kupata huduma hiyo katika vituo vya Paje, Jambiani, Bwejuu na Kitogani ili kuondokana na tatizo hilo ukizingatia afya ni haki ya Kikatiba na ya msingi kwa nchi hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Mwakilishi arudie swali lake kwa sababu mna *echo* kwa kweli sisikii. Naomba mheshimiwa rudia kwa taratibu ili niweze kulipata swali.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku atarudia wengine mnasimama wakati mheshimiwa hajajibu, mnasimama nini sasa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, swali langu ni kwamba je, ni robo gani ya mgao wa dawa ya mwaka unayoizungumza wakati wananchi wa Jimbo la Paje tangu Oktoba mwaka jana wanakabiliwa na tatizo hili na inabidi wajinunulie wenyewe kupitia kwa mwakilishi. Hilo la kwanza.

Je, ni lini wananchi watarajie kupokea dawa katika vituo vya afya kikiwemo Paje, Jambiani, Bwejuu na Kitogani. Tatizo hilo limekuwa ni la muda mrefu na ukizingatia ni haki yao kupata matibabu kutoka serikalini kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, la kwanza nimelisikia vizuri anahitaji takwimu lakini naomba nimjibu kwamba nitampatia kwa maandishi, kwa sababu takwimu sahihi sasa hivi hapa sina. Lakini swali la pili bado linanichanganya, sio kama silielewi isipokuwa simpati vizuri.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mahiri sana na pia nimpongeze Mhe. Mwakilishi kwa umahiri wake wa kuuliza maswali na kufatilia sana Wizara ya Afya mpaka chumba cha *generator* amefika ndani kabisa yeye mwenyewe. Na

la tatu Mhe. Naibu Spika, naomba niseme kwamba ni kweli sera ya Afro Shirazi Party ndio iliyotuagiza sisi sote kupitia kiongozi wa mwanzo Marehemu Mzee Abeid Amani Karume kuwa matibabu na elimu zitakuwa bila ya malipo Zanzibar. Kwa hiyo, ni haki ya msingi ya kila mwananchi.

Mhe. Naibu Spika, naomba niseme kwamba vituo hivi vya Paje, Jambiani, Bwejuu na Kitogani vinakuwa vinapata *essential drug list* kwa sababu hivi sasa fedha tunazozipata hazitoshi kwa dawa zote; ni dawa chache tu ndizo zinatolewa ambazo *essential drug list*. Lakini naomba nichukue fursa hii Mhe. Mwakilishi alikuwa anazunguka katika swali hili, nachukua fursa hii kumshukuru yeye Mhe. Mwakilishi kuwa anachangia moja kwa moja katika vituo hivi vya afya ndani ya jimbo lake kupitia hayo madawa. Pale panapokuwa na kasoro ya dawa naomba nimshukuru yeye anachangia, ilikuwa aseme tu moja kwa moja kwamba anatuchangia. Lakini amezunguka zunguka kidogo kumzungusha Mhe. Naibu Waziri lakini tunamshukuru anatuchangia sisi tunatoa *essential drug list.*

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha pesa zilizokuwa zinahitajika zote kwa dawa ni bilioni 7,000,000,000 lakini hadi sasa tumepata *allocation* ya bilioni 2.6 kutoka serikali kuu na bilioni 2,000,000,000 zinatolewa na wafadhili wa maendeleo (*Development Partners*). Kwa hiyo, bado tuna *deficit* pale kwenye dawa ya bilioni kama 2.2. Sasa hii ndio tukishajihishana sote kwa pamoja kama anavyofanya Mhe. Mwakilishi katika jimbo lake naamini na wawakilishi wote wengine watatusaidia pamoja na Mwakilishi wa Jimbo la Kiembesamaki ambae anaendelea kufanya hivyo katika jimbo lake. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Je, Mhe. Naibu Waziri serikali ina mpango gani wa kuweza kupata fedha zaidi ya kuongeza dawa na kuwaondoshea wananchi tatizo la kukosa dawa katika vituo vya afya.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, serikali kupitia Wizara ya Afya na kwa sababu ya kuliona tatizo hili la upungufu wa dawa na kwa kuwajali na kuwathamini wananchi wake imeamua kuunda kamati maalum kwa ajili ya kuzungumza na kupanga na washirika wa maendeleo ili kuona tatizo hili linaondoka. Kamati imeshaanza kukaa na kutafuta uwezekano na washirika hao na hivi karibuni inaendelea kukaa tena pamoja na washirika hao.

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): Mhe. Naibu Spika, pamoja na maelezo mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kumsaidia vizuri sana Mhe. Naibu Waziri majibu yake ni mazuri. Lakini moja katika maswali ambayo yalikuwa yakiulizwa wiki iliyopita Mhe. Waziri, alikiri kuwa kuna mfuko maalum wa mapesa ambao hutumika kununuwa dawa, lakini na Mhe. Waziri, amesema pesa kidogo, lipi hasa tamko la Serikali kuhusu migongano hiyo miwili ya Waziri na Naibu Waziri.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri, aliotoa, lilifuata sualila pili naomba nimshukuru Mhe. Dimwa, kuomba *clarification* ya hilo alilolitamka na ni vizuri hapa tukawa tunatoa *clarification* ndio sehemu ya Serikali ya kutoa *clarification* hapa na patakapokuwa na jambo linaleta *confusion* ama halijafahamika vizuri ni vyema kuuliza.

Mhe. Naibu Spika, naomba niseme hivi; mfuko uliokuwepo hivi sasa sio ule mfuko ulioanzishwa kisheria kama mfuko wa barabara au mifuko mengine, hakuna mfuko kama huo, mfuko uliokuwepo sasa hivi ni mfuko ambao ni baina ya Wizara ya Afya na Wahisani wetu wa maendeleo, kwa hiyo katika mfuko huo tunapokea mfano wanaochangia sana ni DANIDA, UNFPA, WHO, UNICEF na wengine tutawataja katika hotuba yetu tutakayosoma ya Wizara ya Afya, huo ndio mfuko uliokuwepo.

Mhe. Naibu Spika, Alichosema Mhe. Naibu Waziri katika wiki iliyopita ni kwamba tunatarajia kuanzisha mfuko wetu. Mhe. Hamza alizungumza hapa habari ya bima ya afya, tunatarajia kuanzisha mfuko wetu rasmi ambao utakuwa ni mfuko wa taifa sio wa Serikali wala sio wa Serikali wa Taifa, nikisema Taifa maana yake all *inclusive private sectors, government sectors,* pamoja na *individuals businesses* yaani informal *sectors* pia ataingia humo, ule mfuko ndio utakuwa bima ya afya pamoja na mambo mengine yote ambapo dawa pia itakuwa inachangiwa kupitia mfuko huo. Kwa hiyo huu mfuko uliokuwepo sasa hivi ni kama *joint accoun*t baina ya sisi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wale Wahisani wa Maendeleo. Kwa sababu wale Wahisani wa Maendeleo baadhi yao wana masharti yao wanasema sisi tutatoa asilimia thamanini lakini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iweke *down payment* ya asilimia ishirini kwanza ndio mfuko ule ufanye kazi. Nadhani hiyo ita-*clarify* suala alilouliza Mhe. Dimwa. Ahsante sana.

Nam. 127

Matatizo ya Uongozi ZFA

Mhe. Mussa Foum Mussa - Aliuliza:-

Katika kipindi cha mwaka 2015 Chama cha Soka Zanzibar Z.F.A. kimekuwa na matatizo ya viongozi wake wa Kitaifa kupelekana Mahakamani mpaka kufikia ligi ya Kitaifa kutochezeshwa na kupelekea vilabu vingi vya mpira wa miguu kupata hasara kubwa hasa kisiwani Pemba.

(a) Serikali inalifahamu tatizo hili.

(b) Ni sababu zipi zilizopelekea kutokea hali hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kabla ya kumjibu Mhe. Mussa Foum Mussa wa Jimbo la Kiwani, suala lake Na. 127 lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kuwa Serikali inafahamu matatizo ambayo yamejitokeza kwa viongozi wa Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFA), ambao ulichukua takriban kipindi cha miaka 2. Serikali kupitia WHUUM na Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar imechukua juhudi katika kutatua migogoro iliyokuwepo na suluhu imepatikana.

Mhe. Spika, ni matumaini yangu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwa migogoro hii haitojitokeza tena.

(b) Mhe. Spika, sababu zilizopelekea kusimama kwa ligi ni kutokana na baadhi ya viongozi wakuu wa ZFA kuyapeleka masuala ya michezo katika Mahakama za Kisheria jambo ambalo ni kinyume cha Katiba ya ZFA kwa mujibu wa Ibara ya 100 Ibara ndogo ya 1 na 2. Hii ilitokea baada ya aliyekuwa kiongozi mmoja ZFA Unguja kufungua kesi ya madai Nam. 62/2014 mnamo tarehe 12/12/2014. Shauri hilo baada ya kufunguliwa Mahakamani ilipelekea Mahakama kutoa agizo la kuundwa Kamati ya muda isimamie masuala yote ya Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar. Jambo hili lilipelekea baadhi ya vilabu kugoma kushiriki katika ligi ambayo inasimamiwa na Kamati

iliyoundwa na Mahakama vikidai kuwa masuala yote ya michezo yatatuliwe na vyombo vya michezo vya ndani, ahsante.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba nimuulize suala moja la nyongeza. Kwa kuwa amekiri kwa muda mrefu sana ligi ilisita kuendelea na kwa kuwa amekiri kwamba vilabu vitakuwa vimepata hasara kwa vile vilikusanya wachezaji wake kambini, je Mhe. Waziri ana mpango gani wa kufidia gharama za vilabu hivyo?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante sana Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu suala lake la nyongeza Mhe. Mussa Foum kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza nakubaliana na Mhe. Mussa Foum kwamba ni kweli kwamba migogoro ilikuwepo lakini na pia vyama vimeingia hasara kwa kutoshiriki katika michezo hiyo. Nimuahidi kwamba kupitia Serikali na kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa ufuatiliaji wake na usimamizi wake mzuri hili tumelifuatilia kama nilivyojibu katika suala mama kwamba migogoro na hasara hizi hazitotokea tena na tutaendelea na michezo yetu kama kawaida. (*Makofi*)

Mhe. Wanu hafidh Ameir: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii nimuulize Mhe. Naibu Waziri, suala moja la nyongeza. Kwa kuwa uongozi wa ZFA kwa mujibu wa Mhe. Naibu Waziri wakati anajibu swali imekiuka hata Katiba ambayo ninaamini, Katiba yao ninamaanisha ambayo ndio tunaamini ni muongozo mkuu wa kuiendesha hii association ya *football*. Je, Serikali haioni kwamba ipo haja sasa kwa sababu huu mgogoro umeshakuwa wa muda mrefu na hakuna lililotatuka, Serikali haioni kwamba ipo haja ya kuufuta uongozi mzima wa ZFA na kuitisha uchaguzi mwengine upya ambao utasimamisha uongozi mpya wa ZFA ili kuona kwamba *soccer* linaendelea. Kwa sababu Mhe.Naibu Spika, kulumbana kwao kunapelekea *soccer* kurudi nyuma na kuiacha Zanzibar kuachwa nyuma katika *field* hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba niendelee kumjibu Mhe. Wanu wa viti maalumu swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, nimwambie Muheshimiwa Muwakilishi kwamba hichi chombo cha ZFA kwa kuwa vyombo hivi ni vya kujitegemea na vinaongozwa na kanuni zake na havipaswi kuingiliwa, kwa hiyo hii nimwambie Mhe.

Mwakilishi kwamba tutaendelea kuvisimamia na sisi hatupaswi tuviwekee pingamizi au tuvipe amri mfanye hivi. (*Makofi*)

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona na kunipa nafasi niulize suala la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, suala langu liko hivi, je ni lini hatma ya timu ya Malindi ambayo ilikataa kucheza mashindano chini ya mwamvuli wa Kamati Tendaji ambapo ilikuwa si halali kuongoza mpira wa nchi hii, la kwanza, na je, Mhe. Naibu Waziri, anafahamu kwamba ZFA baada ya kumaliza uchaguzi bado kuna Kamati mbili Tendaji zinaongoza mpira wa nchi hii?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri aliyojibu Mhe. Naibu Waziri niendelee kumpongeza kwa majibu yake. Lakini pia nimjibu Mhe. Abdalla Diwani wa Jimbo la Jang'ombe kwamba Chama cha Mpira kinaongozwa kwa Katiba, Kanuni na Sheria zake. Kwa hivyo hatma ya vilabu vinavyogoma kikiwemo Malindi kinapaswa kabisa kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa Katiba ya ZFA na sheria ziliopo katika vyama vya mipira. Na endapo hatua hizo zitashindwa basi FIFA ipo kwa sababu sheria zinawataka migogoro yao inaposhindikana ndani basi FIFA inaweza ikaingilia kati na kuweka hizo *amicable understanding.*

Na suala lake la pili nilikuwa namuomba aniweke vizuri kabisa angelirudia, ili tumjibu katika ile hali halisia, kwa sababu suala lake lilikuwa kidogo linatoka kama ushauri halikutoka kama swali. Namuomba aliweke suala lake vizuri.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante, swali langu nilimuuliza ni kweli ZFA imemaliza kufanya uchaguzi wake na kuna uongozi halali walioupata, lakini bado ZFA ina kamati tendaji mbili zinazoongoza mpira wa Zanzibar, je Serikali inalitambuwa hilo?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba sana kumjibu Mhe. Abdalla Diwani wa Jimbo la Jang'ombe suala lake kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, kama alivyokiri kwamba ZFA imemaliza uchaguzi wake kwa amani na salama na sasa hivi tuna chombo kamili cha kuongozea mpira hapa Zanzibar. Na badala ya hapo ZFA inaendelea na hatua nyengine ambazo zinatakiwa kuzifanya ikiwemo kupata Katiba ya ZFA. Hivyo Serikali inatambuwa zile taratibu zilizopangiwa kwenye makubaliano waliyokubali ndani ya Mahakama, haitambui uongozi huo mwengine uliokuwepo na wala

haielewi kwamba kuna vyombo zaidi ya viwili au vitatu vinaongoza katika suala zima la mpira, ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Nam. 102

Kujengwa kwa Barabara ya FUONI – MWERA

Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Aliuliza:

Kwa kuwa barabara ya Fuoni melisaba (kwachimbeni) kupitia Fuoni Birikani hadi Mwera Polisi ilikuwa njia mbadala ya kuingilia mjini kipindi cha mafuriko ya mvua mwezi wa April mwaka huu.

(a) Je, Serikali haioni ipo haja ya barabara hiyo kuwa ya kiwango cha lami badala ya kifusi kama ilivyosasa.

(b) Je, barabara hiyo kuendelea kuwa ya kifusi, Serikali haioni itapoteza fedha nyingi ya kuikarabati mara kwa mara ikizingatiwa hivi sasa ina mashimo matupu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 102 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, barabara ya Fuoni – Meli saba (Kwa Chimbeni) kupitia Fuoni Birikani hadi Mwera Polisi ni barabara iliyojengwa kwa kiwango cha kifusi kupitia Mradi wa MIVARF uliokuwa chini ya Wizara ya Kilimo na Maliasili ambao ulilenga kuwarahisishia wakulima kusafirisha mazao yao kutoka shambani hadi kwenye soko. Kutokana na mvua nyingi za masika kunyesha kuna baadhi ya sehemu ya barabara hiyo zimeharibika na hata maji kukatisha barabara. Kutokana na umuhimu wa barabara hiyo pamoja na zile zilizojengwa kupitia mradi wa MIVARF, Wizara yangu imeshaanza kuainisha kasoro zilizojitokeza kwenye barabara hizo na baadae itaziwasilisha inapohusika.

(b) Ni kweli barabara hiyo ikiendelea kuwa na kifusi itahitajika kufanyiwa matengenezo ya mara kwa mara. Serikali itaendelea

kutafuta fedha kwa ajili ya kuziwekea lami kwa awamu barabara zote zilizojengwa na mradi wa MIVARF, Unguja na Pemba, ikiwemo barabara ya Fuoni Birikani - Mwera. Ahsante Naibu Spika.

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza masuala mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: Kwa kuwa barabra hii ina umuhimu mkubwa sana hasa pale katika kipindi cha mvua kubwa na gari nyingi kushindwa kupita maeneo ya Kwerekwe na watu kutumia njia hii kupita Fuoni kwa Chimbeni, Birikani, Misufini mpaka kutokeza Mwera. Naomba Mhe. Waziri, awaahidi wananchi wetu ni lini barabra hii itatengezwa kwa fedha mahsusi maana hata katika bajeti hii bado hakuna fungu lolote la kusaidia barabara hii.

(b) Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba barabara hii ilijengwa kwa mradi wa MIVARF lakini mpaka hivi sasa barabra hii ipo chini ya Wizara ya Kilimo na bado haijakabidhiwa katika Wizara ya Mawasiliano. Je, ni lini sasa makabidhiano hayo yatafanyika ili barabara hii ipate kufanyiwa uharaka katika kukamilishwa kwake.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji napenda kumjibu Mhe. Mihayo Juma N'hunga Muwakilishi wa wananchi Jimbo la Mwera masuala yake ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzo barabara hizi zilikuwa ziko chini ya Wizara ya Kilimo na sisi tulikuwa tunapeleka wataalamu wetu tu kuangalia na sasa kama nilivyosema barabara hii ina umuhimu na tunameuona umuhimu huu wakati wa mvua, wakati barabara hizi za kuja Welezo zimefungika. Kwa hiyo hili suala ni muhimu sana kwetu na sisi kama tulivyo Wizara tunaumwa na barabara zote nchini tuzione kwamba wakati wote zinapitika na ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi inahitaji kwamba barabara zetu ziwe katika kiwango kizuri na zinapitika wakati wowote. Tumelichukuwa suala lako na tutalifanyia kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo ili kuhakikisha ile barabara tunaifanyia marekebisho makubwa na inapowezekana fedha ikaruhusu kuijenga kwa lami.

Mhe. Naibu Spika, na kuhusu suala lake la pili lini tutakabidhiwa hilo ni taratibu za kiserikali na za kimiradi kwa hiyo tutafanya juhudi kuhakikisha kwamba tunazitekeleza kwa haraka ili tuendelee na matengenezo ya bara bara ile, ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi ningependa kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, swali langu dogo la nyongeza lenye mafungu (a) na (b).

> (a) Mhe. Naibu Waziri, pamoja na majibu mazuri uliyotoa, ni lini Serikali itakamilisha barabara ya Jumbi kwenda zake Koani, maana hivi sasa barabara imekuwa hali bin taaban na hatujui nini kinachoendelea na;
>
> (b) Kwa kuwa wananchi wa kisiwa cha Uzi miaka nenda miaka rudi wamekuwa wanapata tabu na imeshazungumzwa mara nyingi na ahadi ambazo zimetolewa. Je, Serikali haioni kwa huruma baada ya ahadi zote miaka yote na mwaka huu angalau kutoa kauli ambayo kuhakikisha kwamba barabara ya Uzi, Unguja Ukuu itakamilika ili wananchi waweze kuitumia kwa unafuu, ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji napenda kumjibu Mhe. Simai Muhammed Said Muwakilishi wa wananchi la Tunguu, masuala yake ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, barabara ya Koani - Jumbi ni barabara ambayo ni muhimu na tutahakikisha kwamba inatengenezwa katika kiwango cha lami, kwa sababu wale wakandarasi waliopita waliacha mpaka katika hatua ya kifusi, kwa hiyo kulikuwa na matatizo ya kimkataba na matatizo baada ya kutatuliwa tu barabara ile tutaitia lami na kwa hiyo tunamuomba avute subira kwa sababu hii kesi ilikuwa imepelekwa Mahakamani.

Swali lake la (b) la nyongeza na vile vile kwamba barabara ya Uzi - Unguja Ukuu ni barabara muhimu lakini barabara ile kuiweka lami ni gharama kubwa tutaendelea kuifanyia matengenezo au marekebisho mara kwa mara ili ipitike wakati wowote. Mhe. Naibu Spika, ahsante.

Mhe. Muhammed Said Muhammed (Dimwa): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukuwe nafasi hii kumpongeza sana kwa majibu yake mazuri anayotujibu. Pamoja na majibu mazuri naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri barabara zote ndogo ndogo chafu zinawakera sana na kwa sababu hiyo wanatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, na kutokana na viongozi wa jimbo la Mpendae hasa Mhe. Mbunge

kujenga barabara kutoka Soko la Mboga Mboga Migombani mpaka Skuli ya Jang'ombe ili kurahisisha upitaji na kupunguza *traffic jam.*

Je, ni lini barabara ile itamalizwa kwa kiwango cha lami.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, ni kweli tunathamini sana juhudi zinazochukuliwa na Wawakilishi wetu na Wabunge katika kuhakikisha kwamba wanazitatua kero za wananchi wao na sisi kama serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ tutaangalia namna gani ile barabara kuifanyia kazi ili kama itawezekana baadae tuitie lami kabisa. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 - Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa kabla ya kuendelea na majadiliano naomba niwatambulishe wageni wetu waliofika hapa leo ambao ni wageni wa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Wageni hao ni viongozi wa Shirikisho la Vyuo Vikuu Zanzibar (*ZAHILFE*) jumla yao ni watatu, wanaongozwa na Makamu Mwenyekiti wao Ndugu Abdul-latif Kadir Mussa, naomba wasimame, nimeambiwa watatu naona mmoja wengine wako wapi, naomba wote msimame msalimie. Ahsanteni na karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe jana tulimaliza na wachangiaji wote, lakini alikuwepo mchangiaji mmoja Mhe. Juma Ali Khatib Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum na aliniomba kuchangia lakini kwa bahati mbaya sana alikuwa hayupo alipatwa na dharura. Sasa basi nimuombe Mhe. Waziri na yeye aweze kuchangia kwa muda mdogo baadae moja kwa moja tutaanza na Mhe. Waziri wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Mheshimiwa karibu sana.

Mhe. Juma Ali Khatib - Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwanza napenda kumpongeza Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kumchagua waziri Maudeline Cyrus Castico, kwa kweli amechagua kiongozi mzuri na mahiri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ukizingatia wizara hii waziri ni mwanamke hodari, Katibu Mkuu Bi. Asha Bilali ni mwanamke mchapa kazi.

Mhe. Naibu Spika: Bi Fatma Bilali.

Mhe. Juma Ali Khatib - Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum: Bi Fatma Bilali, samahani nimekosea**.** Pia naibu wake Bi. Mauwa ni mchapa kazi hodari. Kwa hivyo, nataka kusema ule usemi unaosema kuwa wanawake wanaweza, kweli wanaweza. *(Makofi)*

Halafu nataka kukumbusha kwa wale ndugu zangu ambao wengine ni wadogo Mhe. Waziri wakati fulani tulikuwa na matatizo ya kisiasa katika nchi yetu alishiriki katika mazungumzo ya muwafaka wa CCM na *CUF* ule ulioamuliwa na *Chief* Emeka Anyaoku. Kwa hiyo, pale mimi ndio nilipata kumjua Mhe. Waziri kipaji chake na umahiri wake yeye akiwakilisha Chama cha Mapinduzi, alifanya kazi nzuri ya kuhakikisha nchi yetu inakuwa katika hali ya usalama na amani.

Mhe. Naibu Spika, sasa nikitoa mchango wangu nataka kuzungumzia lile suala la Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Chaani, Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf aliuliza hili suala la ubakaji litakwisha lini? Kwa hiyo, mimi nataka kumwambia kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa namna moja au nyengine inajitahidi kuondoa tatizo la ubakaji hapa Zanzibar, lakini tujue kwamba wale wabakaji ni sawa sawa na watu wenye maradhi kwa sababu wanakuwa kama wagonjwa.

Mhe. Naibu Spika, mvuta unga anafikia kuuza kitu hata cha mama yake, chake au cha mkewe ilimradi apate pesa ya kwenda kununua dawa za kulevya. Sasa na hawa wabakaji inafikia wakati hata mwanawe aliyemzaa anamtamani ndio maana nikasema hili ni gonjwa kubwa sana. Sasa nataka kumwambia Mhe. Nadir kwamba ni juu yetu sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Taasisi za Dini na viongozi wa sekta mbali mbali, sio suala la kwamba tuwaachie wizara hii tu kuwa wao ndio walisimamie. Serikali kwa namna moja au nyengine imetumia wataalamu wake mbali mbali kufanya semina, makongamano na kupitia vikundi mbali mbali na hata vyombo vya dola pia vile vile tumeona kutaka kukomesha jambo hili, lakini bado kuna watu watukutu, kuna watu kwa kweli unapopata hizo habari unasikitika mana haielekei wala haipendezi.

Kwa hivyo, sasa nataka kusema kwamba jambo hili tusiiachie wizara pekee. Jambo hili ni letu sote kama wazazi, wazee au viongozi. Kwa hivyo, Mhe.

Mwakilishi wa Jimbo la Chaani kwa pamoja tukishirikiana tunaweza kukomesha jambo hili la ubakaji katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, pia kuna suala alizungumzia Mhe. Mwakilishi Bahati Khamis Kombo, alitaka kujua juu ya usimamizi wa vikundi vya vyama vya ushirika, alikuwa na wasi wasi kidogo kuhusu vikundi hivi.

Kwanza mimi nataka kusema kwamba, katika jambo zuri serikali ililolifanya ni kuanzisha hii Idara ya Vyama vya Ushirika. Kwa sababu mimi mwenyewe niliwahi kuwa na kikundi cha chama cha ushirika katika miaka ya nyuma kabla ya kuwa mwanasiasa na kwa kweli kupitia Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar imenifanya mimi kunyanyuka kupitia kikundi hicho nikiwa Mwenyekiti wa Kikundi kinachoitwa *Universal Enterprise Cooperative Society;* kilikuweko pale Magomeni. Lakini kupitia idara hii kuna mkurugenzi Bwana Simba na Bwana Suleiman na wengine wengi walitupa elimu nzuri.

Kwa hiyo, ninachotaka kumwambia Mhe. Bahati Khamis kwanza ili kikundi kiendelee na kiimarike, tunahitaji kuwe na viongozi bora na wachapa kazi. Mwenyekiti, Muweka hazina na wale viongozi, uongozi ukiwa mzuri basi ndio mnaweza kuleta mafanikio. Sisi tuliweza kupata mafanikio na wakati ule kulikuwa na vikundi vingi vya vyama vya ushirika. Tulipata misaada ya boti, mashine za boti, nyavu na kadhalika kupitia Idara ya Uvuvi wakati ule alikuweko Ndugu Mussa Aboud Jumbe. Walitusaidia sana na tulinyanyuka na hao Bw. Simba na Bw. Suleiman walitutafutia misaada kutoka Ujerumani tukapata misaada ya vyombo vya kuchonga tukawa na kiwanda kikubwa sana, tukaongeza ajira, tukapata vijana wengi wakaajiriwa. Kwa hiyo, hii yote ni ushahidi kuonesha kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mipango na malengo mazuri kupitia wizara hii na kupitia kitengo hiki.

Mhe. Naibu Spika, namuomba sasa Mhe. Bahati basi ni vizuri yeye asaidie katika jimbo lake hivi vikundi kuhakikisha kwamba wanakuwa na uongozi mzuri na waadilifu. Vile vile wafanye kazi kwa bidii tusikae tu tukasubiri misaada au kusubiri serikali, lazima sisi wenyewe kwanza tuoneshe bidii yetu na tuoneshe kwamba tunazalisha mali na hata kwenye suala la muweka hazina basi pia kuwe na mtu muadilifu na aliyesomea.

Nataka kusema na kuwaomba Waheshimiwa Wawakilishi sote kwa pamoja tuipitishe bajeti hii ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto; sote kwa pamoja kwa sababu hawa viongozi niliowataja ni viongozi wachapa kazi. Yale yote mapungufu tulioyasema hapa, tulioyaonesha au zile changamoto mimi naamini tukiweza kupitisha bajeti hii wakapata pesa hizi basi

na hao viongozi niliowataja kazi itafanyika na itakuwa nzuri, hasa ukizingatia waziri ni mpya na hata Katibu Mkuu ni mpya. Sasa kutokana na imani yao na utendaji wao mzuri wa kazi tusiwe na kigugumizi, tushirikiane tupitishe vifungu hivi pesa ziende na tuone sasa mafanikio kwa wazee, kwa sababu tayari wizara hii imeweza kutuonesha jambo moja kubwa sana ambalo kwa duniani ni adimu.

Mhe. Naibu Spika, leo suala la wazee kupewa kiinua mgongo, kuna nchi nyingi sana ni matajiri lakini mpango huu hawana. Jambo hili alilizungumza Mhe. Rais wa Zanzibar na mimi nampongeza kwamba kalitekeleza. Kwa hiyo, wapo watu wanatubeza wale waliokuwa hawatutakii mema lakini nataka kuwaambia Serikali hii ya Mapinduzi imeweza.

Mhe. Naibu Spika, sasa wale wanaosema kwamba tunatoa kidogo bora kuanza kufanya kuliko kuwa huyo mwenye kingi hata hicho kidogo hatoi. Kwa hiyo, nina imani na wizara hii na nina imani na mpango huu wa serikali kwamba utafanikiwa.

Vile vile nataka watu wajue kwamba huu si mshahara; hii ni pencheni sio kiinua mgongo. Kiinua mgongo mbali hii ni pencheni na hili ni jambo la kuipongeza serikali kwa nguvu zote, itafikia wakati serikali itakapokuwa uchumi wake umekua itakuwa na mipango mizuri zaidi. Sasa hivi serikali hii ina mipango mizuri ya kuchimba mafuta na gesi; ni utajiri, itafikia wakati kwa serikali yetu na viongozi na Baraza la Mawaziri naamini watu wengi watanufaika hata wale wanawake wajane mipango itakuja mizuri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi tuipitishe hoja ya wizara hii ili wapewe mafungu haya wakafanye kazi kuleta maendeleo katika nchi yetu. Ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza kuendelea kuwatakia Waheshimiwa Wajumbe katika shughuli maalum wanayofanya ya maombi kwa ajili ya Mfungo wa Mwezi wa Ramadhani, najua katika dua zao wana mengi wanayoomba ni pamoja na amani ya nchi yetu pamoja na masuala yanayohusu wizara yangu.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaendelea ili nisisahau mambo yaliyojitokeza hivi juzi ya utekaji wa watoto wadogo. Imetolewa taarifa ya kwamba kuna mtoto mdogo si zaidi ya miaka mitatu alikuwa na wazazi wake, mzazi anasali

ameingia mtu na kisu mkononi akamchukua akatisha watoto waliokuwa pamoja huyo mtu akamteka mtoto yule na kuondoka naye. Ni baada ya siku nne mtoto bahati nzuri tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba kapatikana.

Ni masuala ambayo sijui yanatoka wapi na yanalenga nini. Ninatoa wito kuanzia sasa kwa wazazi wote wasiamini hata dakika moja kuacha watoto wacheze peke yao. Watoto wadogo pia wafundishwe elimu ya uaskari ya kusimamia na kutoa taarifa, akiona mwenzake mdogo anasogelewa na mtu asiyemjua atoe taarifa au apige kelele kupita kiasi. Walimu wa skuli nawaomba sana watoe elimu ya kuwaambia watoto waanze kujilinda na wasikubali kushikwa mkono na mtu yeyote ambaye hawamjui kupelekwa skuli wala kurudishwa nyumbani. Katika michezo ya aina yote wasishirikiane na watu wanaowazidi umri. Kwa hayo machache naomba Mwenyezi Mungu aendelee kutusaidia. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima naomba nichukue nafasi sasa kwa niaba yangu na kwa niaba ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Napenda kukushukuru wewe binafsi na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waliochangia hotuba ya bajeti ya wizara yangu moja kwa moja na kwa maandishi. Jumla ya Wajumbe 19 walichangia moja kwa moja na wajumbe 12 walichangia kwa maandishi.

Pia napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati kwa ushauri na maelekezo yake waliyotupa, Mhe. Ali Suleiman Ali maarufu kwa jina la Shihata. Michango yao itaimarisha ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya wizara. Aidha, napenda kuwashukuru wale wote waliotupa ushauri wa maelekezo katika kutekeleza majukumu ya wizara yangu, ushauri wao tunaupokea na tutaufanyia kazi.

Wajumbe waliochangia hotuba ya bajeti ya wizara yangu moja kwa moja ni kama wafuatao:-

1. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata).
2. Mhe. Nadir Abdul-larif Yussuf Al-Wardy.
3. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa.
4. Mhe. Suleiman Sarahan Said.
5. Mhe. Ali Khamis Bakar.
6. Mhe. Bahati Khamis Kombo.
7. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi.
8. Mhe. Hamza Hassan Juma.
9. Mhe Tatu Mohamed Ussi.

10. Mhe. Mihayo Juma N'hunga.
11. Mhe. Masoud Abrahman Masoud.
12. Mhe. Hidaya Ali Makame.
12. Mhe. Khadija Omar Kibano.
13. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis.
14. Mhe. Rashid Makame Shamsi.
15. Mhe. Wanu Hafidh Ameir.
16. Mhe. Zaina Abdalla Salum.
17. Mhe. Hamad Abdalla Rashid.
18. Mhe. Suleiman Makame Ali na
19. Mhe. Juma Ali Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum).

Waliochangia kwa maandishi ni kama wafuatao:

1. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa
2. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)
3. Mhe. Shamata Shaame Khamis
4. Mhe. Suleiman Sarahan Said
5. Mhe. Yussuf Hassan Idd
6. Mhe. Miraji Khamis Mussa
7. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha
8. Mhe. Simai Mohamed Said
9. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira
10. Mhe. Mgeni Hassan Juma
11. Mhe. Jaku Hashim Ayoub na;
12. Mhe. Panya Ali Abdalla.

Jengine zaidi ni pamoja na kwamba Mhe. Jaku Hashim Ayoub hivi punde tu ameniletea *page* zaidi ya tatu ambazo itabidi nimjibu kwa muda utakaofaa kwa sasa hivi haitakuwa rahisi. Naamini ni mchangiaji sawa na wajumbe wengine wanaochangia kwa nia nzuri ya uwakilishi wa majimbo yao, Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Mhe. Naibu Spika, napenda kujibu hoja mbali mbali za Waheshimiwa Wajumbe kama ifuatavyo:-

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) alichangia kuhusiana na suala Kamati ya Mifugo, Utalii Uwezeshaji na Habari, ukosefu wa Ofisi Pemba. Ni kweli wizara haina jengo la ofisi kwa Pemba. Katika kukabiliana na hali hiyo, Wizara

ya Fedha kwa mwaka huu imeahidi kuanza ujenzi wa ofisi hiyo eneo la Gombani Chake Chake. Ujenzi wa Limbani anasema ukamilishwe.

Napenda kusema ujenzi wa nyumba ya wazee Limbani uko katika hatua ya mwisho. Kuwaandaa vijana ili kuweza kujiajiri na kupatiwa vifaa vya kazi kuwasaidia kujiendeleza kwenye ajira. Wizara imeandaa programu mbali mbali za kuwasaidia vijana kujiajiri, programu hizo ni:

1. Kuanzisha kituo cha kulea na kukuza wajasiriamali; kilichopo Mbweni;
2. Programu ya Kilimo cha mboga mboga na matunda;
3. Mpango wa Ajira kwa Vijana;
4. Kutoa mafunzo kwa vijana 264 ya kuweza kujiajiri kwa kushirikiana na *VSO* na *ILO*;

Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambao umetoa ajira kwa vijana, (angalia uk 67) katika taarifa yangu.

Kuhusu usala la kulipa tozo na ada mbali mbali kupitia benki. Ushauri huu ni mzuri hata hivyo kwa utaratibu wa sasa, ada zote zinalipwa katika idara husika na zinatolewa risiti rasmi za serikali na kupelekwa benki kwa mujibu wa sheria inayohusiana na mambo ya fedha zinavyoelekeza.

Wizara ihakikishe kuwa hakuna mtu anayestahiki kupata penchini anaachwa kupokea pencheni hiyo. Ushauri umepokelewa na wizara mtu anayestahiki kupata pensheni hatoachwa kupokea pensheni hiyo.

Wizara ihakikishe kuwa kila miezi sita inafanya uhakiki kuwatoa wazee waliofariki. Uhakiki wa wazee unafanywa kila miezi mitatu. Wizara iongeze vituo vya malipo ili kuwapunguzia wazee masafa ya kuzifuata fedha vituoni. Wizara imeanza kuviongeza vituo vya malipo kwa kuvisogeza karibu na maeneo yaliyokuwa mbali Mfano, kituo cha Mwembe Makumbi kimesogezwa katika skuli ya Maandalizi Kwamtipura. Wizara inaendelee kutoa elimu kwa jamii kuhusu programu hii, wizara inaendelea na zoezi hilo na nyinyi kama washiriki naomba mtusaidie katika kutoa taarifa.

Mhe. Sada Ramadhan Mwenda, Mwakilishi wa kuteuliwa anauliza wanawake wa Mkoa wa Mjini Magharibi wameshajiishwa kwenda kuchukuwa mikopo na lini watapatiwa mikopo hiyo. Naomba nikwambie kwamba Mheshimiwa wanawake wote ambao wamekamilisha taratibu wamepatiwa mikopo kati ya shilingi milioni mia tano zilitolewa na shilingi mia moja na thamanini na moja

zilitolewa kwa mikopo ya Mjini Magharibi na zaidi ya shilingi milioni mia moja ziliwafikia wanawake. Natoa ushauri kwamba wale ambao hawajapatiwa mikopo wakamilishe taatibu ili nao wapatiwe mikopo hiyo.

Mhe. Ali Khamis Bakari amesema kuna ongezeko la vijana lakini hakuna ajira wala mikopo. Napenda kumjibu kwamba kuna mfuko maalum wa vijana ambao hutoa mikopo kwa vijana, nawashauri vijana watumie fursa hiyo na kama hawajui utaratibu wafike katika ofisi yetu wapate maelekezo.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud, ameonesha wasi wasi kwamba mikopo haipewi watu wenye kipato kidogo baada yake hupewa wenye kipato kikubwa na anataka kujua wakulima gani wamesaidiwa na mfuko.

Mifuko na mfuko wetu ni kwa ajili ya wajasiriamli wadogo wadogo, na kiwango cha mwanzo ni shilingi hamsini elfu na kiwango cha juu kabisa ni shilingi milioni tano. Wakulima waliofaidika na mikopo yetu ni wa Mwani. Hii ni jumuia ya wakulima wadoga wadoga na matunda wamepata milioni thamanini na mbili, kikundi cha ndimu Bwejuu wamepata milioni sitini na mbili, wakulima wa Chokochoko na Wambaa Pemba wamepatiwa *green house* na fedha za uendeshaji kila mmoja milioni kumi.

Mhe. Hidaya Ali Makame; Urasimu wa kuanzisha vikundi ili vipatiwe mikopo na kwamba gharama au riba za mikopo ni kubwa. Naomba kumjibu kwamba kwa sababu mikopo na mifuko ya uwezeshaji ni ya watu wa kipato cha chini na haina dhamana, vikundi ndio dhamana ya mikopo. Kuhusu riba kuwa ni mikopo ya mifuko ya uwezeshaji haina riba nawaomba wananchi wawe makini kuamua wapi wakachukuwe mikopo kwani taasisi za mikopo ziko nyingi.

Mhe. Mihayo Juma N'hunga, watu wenye ulemavu wamewezeshwaje. Naomba kumwambia wizara imeweka kipaumbele kuyawezesha makundi yote wakiwemo watu wenye ulemavu, elimu ya ujasiriamali hutolewa kwa wananchi wa makundi mbali mbali katika jamii yetu ikiwa ni pamoja na watu wenye ulemavu. Kwa mwaka 2015/16 vikundi vitatu viwili Unguja na kimoja Pemba vya watu wenye ulemavu vmepatiwa elimu ya ujasiriali pamoja na wajasiriamali wenye ulemavu watatu. Wananchi wengi wameomba mikopo na bado hawajawezeshwa.

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba mahitaji ya mikopo ni mengi kuliko uwezo. Utaratibu unaotumika ni kuwa wanaoomba mikopo mwanzo ndio wanahudumiwa mwanzo. Hivyo, namuomba Mhe. Mihayo Juma N'hunga

pamoja na wananchi kuwa awe na subira na wafuate maelezo wanayopatiwa na maasifa wa mikopo kuhusu hatua za maombi yao.

Mhe. Nadir Abdul- Latif Yussuf Al-Wardy, ni vigezo vipi vinavyotumika katika kuwawezesha wanawake na watoto wa kike katika kuwaozesha. Kwanza wanawake wanaruhusiwa kuolewa pale wanapofikia umri wa miaka 18 na kuendelea. Hata hivyo, wizara yangu sio muhusika wa moja kwa moja katika masuala ya ndoa bali inasimamia upatikanaji na uelewa wa haki za wanawake. Wizara inadhamiria kutoa elimu ya malezi katika Shehia na Baraza la Watoto ili kupunguza au kuondoa kabisa tatizo la ndoa za umri mdogo.

Mhe. Hamza Hassan Juma, ajira kwa watu wenye ulemavu. Kuhusiana na suala la ajira kwa watu wenye ulemavu wizara imefanya uajiri wa wataalamu wawili ambao ni watu wenye ulemavu. Hivyo, nalihakikishia Baraza lako kuwa tunatekeleza suala hilo kwa vitendo.

Kuanzishwa programu maalum ya vijana waliomaliza vyuo vikuu kupata ajira. Nalishukuwa suala lake kama ni ushauri muhimu sana katika kukuza ajira. Lakini naslichukuwa suala lake hili...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa Waziri samahani kidogo, Waheshimiwa naomba sana utulivu wenu minong'ono imezidi na wengine hawasikii vizuri. Kwa hiyo, naomba sana utulivu wenu kama mtu anajisikia kuzungumza bora atoke nje ili awapishe wengine wasikilize, sawa. Tuendelee Waziri. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante Mheshimiwa naomba kuendelea.

Napenda kumuhakikishia Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba nalichukuwa suala lake kama ni ushauri muhimu sana katika kukuza ajira. Lakini napenda kumjulisha Mheshimiwa suala lake hili tumelifanyika kazi, hivi karibuni vijana 500 walifanyiwa tamasha kwa kushirikiana na *VSO* lengo na kuwaunganisha na makampuni na tumefanya hivyo, wengi wa vijana hao ni waliomaliza Vyuo Vikuu na vyuo mbali mbali.

Wafanyakazi kutolipwa malipo ya zaida *over time*. Wizara yangu inatimiza wajibu wake kwa kuwalipa stahiki zao za *over time* wafanyakazi wote wanaostahiki. Wahusika ni walinzi na madereva wa vituo vya kulelea wazee. Tutaendelea kulipa mafao hayo kadiri hali ya upatikanaji wa fedha utakavyoruhusu.

Natoa wito kwa wizara zote ambazo zitakuwa hazijafanya hivyo basi tushirikiane katika kuwapa haki kwa sababu hawa wanaofanya kazi hii wanafanya kazi na wanatoa michango pasipo wao hatutaweza kufanikisha malengo yetu.

Kukatishwa mikataba na kupunguzwa kazini na kutokuwa na uhakika wa kurejea kazini msimu mwengine. Sheria ya ajira namba 11 ya mwaka 2005 inatambua aina nne za mikataba ya kazi ambazo muajiri na muajiriwa wanaweza kukubaliana mkataba wa kudumu, mkataba wa muda mfupi; kati ya miezi sita hadi miaka mitatu.

Mkataba wa muda maalum na mkataba wa kutwa unaishia miezi 6. Hata hivyo, wengi wanaingia katika mikataba ya muda mfupi kutokana na kuwa na kazi za utalii na ni za msimu tu na msimu huu baada ya kutembea nimekuta kwamba nchi nyengine hazifanyi kwa msimu, kwa sababu wanajenga mazingira ya kuendelea na kazi zinakuwa mahotelini na wanaendelea kufanya mambo mengi ambayo yanavuta watalii. Kwa hiyo, ningependa kuwa tufanye suala hili lisiwe la msimu, liendelee.

Suala la wafanyakazi kufanyiwa kazi kwa masaa 12 alitaka kujua mikataba ya kimataifa ya kazi inasemaje. Kwa mujibu wa mikataba ya kimataifa muda wa kazi hautozidi masaa kumi kwa siku. Sheria ya ajira namba 11 ya 2015 imeweka utaratibu wa saa za kazi kwamba ni masaa manane kwa siku au masaa 45 kwa wiki. Ingawa kwa kazi za *shift* masaa ya kazi yanaweza kuwa ni 10 na hayatazidi 48 kwa wiki na kwamba masaa yanayozidi 8 ni lazima yalipwe ziada *over time*.

Kufuatilia nafasi elfu tano za ajira Tanzania kutoka Qatar kati ya hizo elfu mbili ni za Zanzibar. Nimewafiki na kukubaliana na Mhe. Hamza Hassan Juma na kwa taarifa tu ya zaida ni kwamba hivi karibuni tulipokuwa tumesafiri mtendaji wangu Kamishna alikuwa apate safari ya kwenda Qatar kwenda kuthibitisha watu wanafanyakazi maeneo yepi na waonane na ubalozi ulioko kule na waajiri walioko kule. Lakini bahati nzuri imekuwa ni kipindi cha mwezi wa Ramadhani na wale watu hawawezi kufanya kazi katika kipindi hicho kwa hiyo tumempa muda atakwenda baadae.

Alitaka wizara kuandaa programu kwa vijana wanaomaliza Vyuo Vikuu ili waweze kujiajiri. Wizara yangu tayari imeanzisha programu kama hiyo na taaluma mbali mbali zinatolewa ambazo zina uwezeshaji vijana wanaomaliza Vyuo Vikuu kujiajiri na kuajiri wenzao na kuendesha biashara zao kwa faida.

Prgramu hii inaendeshwa na kituo chetu cha kukuzia na kulelea wajasiriamali kilichopo Mbweni.

Mhe. Salama Ramadhani Mwenda, kwa mara nyengine udhibiti wa ajira za watoto. Ajira za watoto ni jambo ambalo linapigwa vita sana duniani kote. Mikataba kadhaa ya kimataifa inakomesha tatizo hili, wizara yangu inalifanyia kazi sana tatizo hili kwamba kuzingatia miongozo ya sheria yetu ya ajira ya namba tano ya mwaka 2005 sambamba na mpango wa kupambana na ajira za watoto. Tumewatoa watoto elfu tano na saba waliotoroka skuli na familia zao kuwapatia vifaa vya skuli watoto husika na kurejea skuli.

Pia familia elfu moja sitini na tano zimepatiwa vifaa vya kuanzia miradi ya kilimo, mafriji na mifugo.

Mhe. Tatu Mohamed Ussi, wajasiriamali wanaopewa mikopo wapatiwe elimu ya ujasiriamali ili wafanye vizuri zaidi katika biashara zao na waweze kurejesha mikopo. Ushauri umepokelewa na mfuko utazidi kutoa mafunzo ya ujasiriamali katika wigo mkubwa zaidi hususan katika masuala ya masoko ili kuinua ubora.

Mhe. Ali Khamis Bakari na Mhe. Bahati Khamis Kombo wamesema wazee wapewe taalamu ya malezi ya watoto. Wizara kwa kushikiriana na *Save the Children*, imeandaa muongozo wa kusaidia wazazi katika makuzi na malezi bora ya watoto.

Mhe. Bahati Khamis Kombo, Jimbo la Chambani Kuwaelimisha kinamama kuhusu ubaya wa ajira za watoto. Nimewafiki nakubaliana na Mhe. Bahati tutalifanyia kazi suala hili.

Mhe. Masoud Abdulrahman Masoud Jimbo la Bububu namna gani Wizara itasaidia vikoba na vyama vya ushirika wizara haina mamlaka ya kusimamia vikoba na serikali inaandaa sera ya Kusimamia taasisi za fedha ambayo itasimamia masuala ya vikoba. Ushauri wa kuviimarisha *SACCOS* na vyama vya ushirika kwa mafunzo na misaada umepokelewa. Vijana wanaoajiriwa nje ya nchi wanafanyishwa kazi kubwa kuliko kazi walizoahidiwa kwenda kuzifanya.

Napenda Kuwajibu Waheshimiwa wote waliouliza suala hili kwamba, ajira za nje ya nchi zinaratibiwa kwa umakini na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambapo zimeweka taratibu za kuwalinda vijana wetu wanaopata fursa za ajira nje ya nchi. Taratibu hizo ni.

i. Wakala wa Ajira waliosajiliwa tu ndio waliopewa fursa ya kuwapeleka vijana kwenda kufanya kazi nje ya nchi na;
ii. Kabla ya ridhaa au ruhusa kutolewa mhusika awe amepata mkataba unaotoka ubalozini Ubalozi wa Tanzania nchi husika.

Kijana yeyote ni lazima awe anatambulika na Sheha wake aweke taarifa za wadhamini wake na aweke taarifa zake sahihi.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy wa Chaani kuhusu Idadi ya vyama vya Ushirika katika Jimbo lako la Chaani Idadi ya vyama vya ushirika vilivyosajiliwa kwa jimbo lako la Chaani ni 43, vyama vingine inawezekana kuwa vimesajiliwa na taasisi nyingine, kama vile Ofisi Mrajis Mkuu na kama unahisi kwamba viko kwetu lakini hatuna taarifa tafadhali fika ofisini na tuweze kushauriana vizuri.

Alitaka kujua kuhusu Ajira 9,542 zilizooneshwa katika kitabu cha Bajeti. Wangapi wazanzibari, watanzania na wa nje ya Tanzania.

(i) Wanafanyakazi kwenye Taasisi zipi na kazi gani?

Wizara ilifanya ukaguzi kujua idadi ya wazalengo Watanzania waliopo kazini katika taasisi zetu. Idadi hiyo ni kubwa kwa Tanzania tu Zanzibar na Tanzania Bara, haikujumuisha wafanyakazi wa kigeni. Taasisi zilizokaguliwa za mahoteli za ulinzi na skuli za binafsi.

Idadi ya watoto walioripotiwa kufanyiwa udhalilishaji tafadhani naomba uangalie katika ukurasa wa 41 ay 106.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy, je, ni watu wangapi wamekamatwa kwa ubakaji wangapi wametiwa hatiani. Takwim halisi za kesi zinaweza kupatikana Mahakamani yaliyiripotiwa ni matukio tu sio kesi angalia ukurasa wa 36 aya 90 na wangapi wameachiwa huru utapata hapo. Hatua gani zimechukuliwa kuhusu udhalilishaji wa wanawake na watoto na wazee, wangapi wanaomaliza mashauri wametiwa hatiani.

Hatua zimezochukuliwa ni pamoja na kuandaa mpango kazi wa miaka mitano kufanya kampeni ya miaka miwili na kushirikiana na vyombo vya habari kuelimisha jamii. Sababu zipi zilizopelekea wazee katika mwezi wa April wa Mei wasilipwe pesa zao za Pencheni.

Sababu zilizopelekea wazee wasilipwe pesa zao ni kufariki na wengine kutokuja kwenye vituo vya malipo.

Suala la ubakaji litamalizika lini? Kwa heshima kabisa naamini kabisa kwamba Mhe. Juma Ali Khatib amekujibu ipasavyo na mimi hapa labda ningeweza kueleza kwamba hili suala liko ndani ya nafsi ya mtu, pale tu watu watakapoamua na kuwa na ghofu ya Mwenyezi Mungu na watakaposikia mawaidha ya viongozi katika nyumba za dini ndio watakapoweza kubadilika. Kwa sababu hakuna hata mmoja anaeonesha dhahiri kwamba atafanya kitendo hicho.

Mhe. Suleiman Sarahan Said, suala la wazee waliopewa umri sio sahihi na hivyo wanakadiria kuwa ni wadogo na hali ya kuwa wameshatimiwa umri wa kupewa pencheni. Waziri alichukulieje suala hili.

Wizara inatumia nyaraka na vigezo mbali mbali kuthibitisha umri wa mzee hata hivyo kwa wazee wasiokuwa na nyaraka hizo au waliopewa umri mdogo katika nyaraka zao wanatakiwa kuwasilisha hati za kiapo kutoka Mahakamani au barua kutoka afisi za wilaya inayothibitisha kuwa mzee amefanyiwa tathmini ya umri ipasavyo. Kwa masuali ya zaida anaulizwa matukio mbali mbali yaliyotokea wakati akiwa mdogo au kipindi hicho alichokuwa amezaliwa, vita vikuu, alianzishwa lini, alizaliwa lini na mambo mengi.

Mhe. Bahati Khamis Kombo Jimbo la Chambani kasema kuwa pencheni izingatie wazee wanawake ambao hawajatimiza umri, lakini na wenye ulemavu je, wanafikiriwa vipi.

Mhe. Naibu Spika, ninataka kusema hivi programu hii ni kwa ajili ya wazee tu waliotimiza miaka sabini na kuendelea na watu wenye ulemavu wana mfuko watapaswa wautumie. Asilimia 43 ya wazee waliosajiliwa wana ulemavu. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis pia alikuwa na suala kama hili. Mhe. Ali Khamis Bakar wa Jimbo la Tumbe. Wizara iwatengee muda wazee wa Makaoni kuwatoa na kuwapeleka safari za mapumziko. Wizara ilianza kuufanyia ushauri huu katika mwezi wa Septemba kuwapeleka *day out* katika Kijiji cha Pongwe Wilaya ya Kati Unguja.

Aidha, wizara itaendelea kuufanyia kazi ushauri huo. Ninadhani munakumbuka hata ile siku ambayo niliwaleta humu ndani ni kwa ajili ya kutaka kuwaona na kuwapa *exposure* wazee wale waliotoka Sebleni. Wizara ilianza kufanya ushauri huu katika mwezi wa Septemba kwa kupeleka *day out* na sehemu chengine ambazo wanazishauri wao, wanakumbuka mambo mengi.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud wa Jimbo la Bububu. Jee, wanaolipwa elfu tano wanalipwa na shilingi elfu ishirini. Wanaostahiki Pencheni jamii elfu ishirini wanaondolewa kwenye elfu tano. Kwa maana wanalipwa ishirini na tano zinapunguzwa na wanakuwa wamepata faida ya elfu kumi na tano. Je, wanaolipwa ishirini na tano, wanalipwa elfu ishirini. Wanastahiki Pencheni ya jamii elfu ishirini ni kama nilivyojibu kwamba wanapewa hizo wanazozipata sasa.

Mhe. Hidaya Ali Makame nafasi ya wanawake. Wazee wengi hawajasajiliwa katika mpango wa pencheni kwa sababu watoto wao wana uwezo. Hii si dhana sahihi. Pencheni jamii ni haki ya kila mtu aliyefikia miaka sabini. Hata mimi nikiondoka nikifika kwenye miaka sabini ni mdau.

Mhe. Wanu Hafidh Amei nafasi ya wanawake. Kwa nini Mahakama ya Watoto haisikilizi kesi za kubakwa. Kwa mujibu wa kifungu na kwa msaada wa Mwanasheria Mkuu anaweza taarifa hiyo baadae akatusaidia. Kwa mujibu wa Kifungu Nam. 18; Kifungu 1(a), (b) Mahakama ya Watoto imepewa mamlaka ya kusikiliza kesi za watoto zinazohusiana na matunzo, ulezi, uzazi, ukaazi na kuwaona watoto. Pia Mahakama hii ina mamlaka ya kusikiliza makosa ya jinai wanayofanya watoto.

Makosa haya hayajumuishi makosa ya kuuwa, kuuwa bila ya kukusudia, uhaini na kubaka. Mahakama hii kushindwa kusikiliza kesi ya kubaka ni moja ya mapungufu ambayo wizara imeanza kuyafanyia kazi.

Pia ifahamike kuwa Mhe. Naibu Spika, Mahakama hii ni kwa ajili ya watoto tu. Mtu mzima anayemtendea kosa mtoto hatapelekwa katika Mahakama hii. Mahakama yenye mamlaka ya kusikiliza kesi ya kubaka ni Mahakama ya Mkoa ambazo zipo katika Mkoa.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rashid Makame Shamsi wa Jimbo la Magomeni. Mikopo ya watu binafsi ni mingi kuliko ya vikundi. Wana vikundi wanayo haki ya kuchagua kuchukua mikopo ya vikundi au mikopo binafsi. Wakala wa ajira wanapewa lenseni kiholela.

Mhe. Naibu Spika, utoaji wa lenseni umewekewa utaratibu wa kisheria na Kanuni. Katika kudhibiti tatizo hili tayari wakala wawili wamefutiwa lenseni zao na makampuni sita zimeshindwa kutokana na kutotimiza masharti.

Mhe. Naibu Spika, ninaamini kabisa inawezekana kuna wengine wameniletea masuala labda sijayajibu au sijayajibu wanavyotegemea, ninawakaribisha na mlango wangu upo wazi kuendelea kuuliza maswali. Kwa sababu mukipata uelewa wa kutosha mutasaidia na kutoa michango yenu ipasavyo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ninapenda kwa mara nyengine tena kukushukuru wewe na Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa michango na pongezi mulizotupa katika utekelezaji wa kazi zetu. Ninapenda kuahidi kuwa maoni na ushauri wenu tutaufanyia kazi ili kuongeza ufanisi wa majukumu yetu ya kila siku kwa manufaa na maendeleo ya wanawake, vijana, wazee, watoto na jamii kwa ujumla. (*Makofi*)

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kutoa hoja. Naomba kuwasilisha na ahsanteni sana. (*Makofi*)

Amani ya Bwana iwe nanyi.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri ametoa hoja, sasa niwaulize wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa. Wanaokubali wameshinda. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara ya Maalum SMZ: Mhe. naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwa mara nyengine kuwa Baraza limejadili na kuikubali Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Vijana, Wanawake naWatoto, sasa naomba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

Naomba kuwasilisha.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU Q 01 WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI, WAZEE, VIJANA, WANAWAKE NA WATOTO

Kifungu Q 0106 Idara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Shs.11,975,000/-
Kifungu Q 0107 Idara ya Maendeleo ya Ushirika

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ninampongeza sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na niliuliza suala langu katika kuchangia hoja kwamba kikundi hivi vikundi vya ushirika kwa ujumla katika kitabu chake upande wa Kaskazini, Kaskazini "A" niliona kwamba kuna vikundi vitatu ambavyo anavitambua vya Mcheza Mshauri na sehemu nyenginezo kwenye Jimbo langu la Chaani.

Suala langu lilikuwa kwenye Jimbo langu la Chaani nimeona vikundi vitatu vya ushirika lakini hapa Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri kanieleza vipo vikundi arobaini na tatu. Ningeomba tu anieleze hivi vikundi arobaini na tatu vipo katika ukurasa gani ili nipate kuangalie uzuri.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, vikundi vimewekwa katika sehemu mbali mbali. Inawezekana vimemezwa kati kati ya vikundi vyengine. Lakini ninataka kumthibitishia kwamba vipo na vitazingatiwa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, labda angenieleza vimefichwa wapi. Maana yake kama Kaskazini "A" vipo vitatu, hivyo vyengine vimepachika kwenye Kaskazini ipi au labda sehemu gani.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwa upendo kabisa Mhe. Nadir naomba unisaidie kwa kuangalia kwenye majadweli ambayo vikundi arobaini na tatu vipo katika daftari la usajili la serikali.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nitaangalia naomba tuendelee.

Kifungu Q 0107 Idara ya Maendeleo ya Ushirika

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, jana nilipokuwa nikichangia kupitia hapa kwenye masuala ya ushirika nilisema kwamba tunaipongeza sana

serikali yetu katika kuwasaidia wananchi wetu mbali mbali, kuwapatia fursa mbali mbali za mikopo. Na miongoni mwa hao ambao wamepata hizo fursa ni wananchi ambao waliotumia zile fedha kwa ajili ya kununua ng'ombe na kuwafuga. Na tuliomba kauli ya serikali.

Katika kadhia hii ambayo Waheshimiwa wengi waliizungumza kwenye *tension* kubwa sana, lakini bahati mbaya ile kauli ya serikali hatujaisikia mpaka sasa hivi. Na hoja yetu zaidi ilikuwa mazingira ya mjini hatuna tatizo nalo katika suala zima la ufugaji wa ng'ombe. Lakini katika ukanda wa Wilaya ya Magharibi, yaani Mkoa wa Mjini/Magharibi, kwa Wilaya ya Mjini hatuna tatizo lakini kwa Wilaya ya Magharibi hili suala limekuwa tatizo kubwa kutokana na mazingira ya Wilaya ya Magharibi yanaruhusu ufugaji wa ng'ombe.

Sasa tulikuwa tunataka maelezo ya serikali ili na wananchi sasa wajiridhishe kwamba serikali katika kulitatua tatizo hili, kuna utaratibu gani ambao unafanywa. Kwa hivyo nilikuwa naomba tu maelezo Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, ninataka nimshukuru sana Mhe. Hamza. Ni kweli alivyochangia jana alikuwa amezungumzia suala la vikundi vya ushirika na suala zima la operesheni kuondosha wanyama ndani ya Manispaa tatu.

Kwanza ninataka niliarifu rasmi Baraza lako Tukufu kwamba *qualification* ya Manispaa, eneo la Manispaa ni eneo lote la Wilaya kwa mujibu wa sheria. Na operesheni hii ya ondosha wanyama inayosimamiwa chini ya Mkoa wa Mjini/Magharibi imeendeshwa na mamlaka tatu. Mamlaka ya Baraza la Manispaa la Mjini, Baraza la Manispaa la Magharibi "A" na Magharibi "B".

Ni kweli wachangiaji watano wamelizungumzia suala hili kwenye bajeti ya Mhe. Waziri.

Kwanza alikuwa ni Mwenyekiti wa Kamati, wa pili alikuwa ni Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy, wa tatu alikuwa ni Mhe. Masoud Abrahman Masound, wa nne alikuwa ni Mhe. Mihayo Juma N'hunga na wa tano alikuwa ni Mhe. Hamza Hassan Juma. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, tulitakiwa tutoe kauli na nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ilipokuja hoja iliyoanzishwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub, alisema kwamba jambo hili

tumelisikia na serikali inao utaratibu wa kuleta Kauli za Serikali ndani ya Baraza hili. Kilichofuatia mimi Waziri mwenye dhamana ya suala hili, nimeshamuona Mhe. Spika kwa ajili ya kuomba muda, ili serikali ilete Kauli ya Serikali juu ya jambo hili. (*Makofi*)

Sasa Mhe. Hamza ameleta hoja ya kwamba ni vizuri nikalieleza. Ukiniruhusu Mhe. Mwenyekiti, tuache utaratibu ule wa Kauli ya Serikali, nilieleze hapa basi nitalisema hapa. Lakini serikali ina utaratibu wa kutoa kauli.

Sasa kwa sababu nilishaomba miadi na niliahidiwa kwamba nitapewa nafasi, nilikuwa naomba Waheshimiwa Wajumbe waliachie fungu la Mhe. Waziri, serikali italeta Kauli Rasmi ya Serikali kuhusu jambo hili. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza pamoja na wale wote ambao wamelizungumzia suala hili. Ningeomba basi ridhaa yenu tuendelee ili kwa sababu Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ tayari ameshatoa hatua na amesema kwamba atalitolea taarifa, na Mhe. Spika ametoa agizo hilo. (*Makofi*)

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru na ninashukuru sana Kauli ya Serikali, na kwa sababu hapa tunaendesha taratibu zetu kwa mujibu wa Kanuni na Sheria. Kwa hivyo, sisi hatuna tatizo na hilo na ninaamini wananchi wetu kuanzia leo watakuwa watulivu ili kuisubiri Kauli ya Serikali.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba sana serikali. Serikali inakuja na kauli na utaratibu wa kauli kuna taratibu zake hapa Barazani. Ili tusije tukasokotana hapa Barazani, tuna taratibu zetu, tuna *caucus* na mambo mengine. Kabla ya kuja Kauli ya Serikali ni vizuri tuka-*compromise* tukakaa tukajadili ili inapokuja ile Kauli ya Serikali, isije ikaleta tatizo hapa katika Baraza letu. (*Makofi*)

Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku kaa kwanza nimsikilize Mhe. Waziri halafu nitakuja kwako.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninataka nimpongeze Mhe. Hamza mwanafunzi

wangu wa hapa Barazani. Kwa kuelewa kwamba tunakwenda kwa mujibu wa taratibu, sheria na kanuni. Na niliposema ni vizuri nije na kauli kwa sababu hizo *process* au taratibu ambazo amezisema ndiyo ninazotaka tuzifuate. (*Makofi*)

Pengine ningetoa taarifa hapa kama ilivyotakiwa nisingepata muda na wao pengine wasingenielewa vyema. Kwa hivyo, hizo taratibu alizozielekeza ninadhani ndiyo msingi wa serikali kufuata taratibu na sheria na kanuni zake. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri, sasa Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri lakini kwa faida ya wananchi na uwepo wetu hapa, tupo kwa niaba ya wananchi na hichi kisingekuwepo bila ya kuwepo na wananchi. Na serikali hii isingekuwa madarakani bila ya kuwepo wananchi.

Ningemuomba tu kwa unyenyekevu na huu ni mwezi Mtukufu wa Ramadhani tumo kumaliza kumi la mwanzo. Kuna fununu tarehe kumi na saba ndiyo mwisho na leo ni tarehe kumi na tano. Nimezungumza jana mimi kwa spika lazima nikiri. Nilikuwa na hoja ya dharura mimi kuileta hapa ambayo niliiandaa. Lakini tukafika pahala tukaelewana na Mhe. Haji Omar Kheir. Sasa awafahamishe wananchi angalau badala ya kuhangaikia chejio wakapata kupumua, wale wale ng'ombe waliokamatwa ambao wengine wamekamatwa kwa maonevu makubwa wakiwa majanini wakila majani, wengine wakiwa ndani ya mabanda.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, kwani tangu hapo tulipokuwa tunazungumza hujafahamu?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nimefahamu, lakini kuna kauli ya tarehe 17 ndio mwisho.

Mhe. Mwenyekiti: Tumekubaliana kwamba, serikali itatoa taarifa na kwa mujibu wa kanuni ndivyo inavyotakiwa kuwa, serikali ije hapa, wewe umepeleka maombi kwa Mhe. Spika, na Mhe. Spika, ame-*consider* maombi ya watu wengine vile vile, hapa serikali itatoa taarifa. Hakuna la ziada zaidi ya hilo Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nimekuelewa sana tena sana kabisa. Nilichokiomba mimi kwa unyenyekevu kabisa na kwa lugha nyepesi na laini

ili kuwatoa wasi wasi wananchi Mhe. Mwenyekiti. Kuwa wale ng'ombe waliokamatwa hawatopigwa mnada, wa mwaka 2013 ndio watauzwa. Ni kauli hiyo tu ili wananchi wapate kusikia, hayo mazungumzo tunayajua mimi na yeye ni jambo dogo tu, na ni Kiswahili kifupi tu. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Jaku Hashim Ayoub, atakubaliana na mimi, hata hilo analolitaka nilishamwambia. Lakini kuna ng'ombe waliokamatwa mwaka 2013, ni miaka mingapi tokea muda huo wote. Wako ng'ombe 14 waliokamatwa muda huo basi serikali itawapiga mnada.

Lakini wale ng'ombe waliokamatwa katika kipindi hiki hatuwezi kuwapiga mnada, kwa sababu kuna taratibu na vigezo vifikiwe. Kwanza serikali hii haimuonei mtu nataka aelewe sana Mhe. Jaku Hashim, serikali hii inawapenda sana wananchi wake wote. Kwa hivyo, ng'ombe ambao Baraza la Manispaa na mabaraza mengine wamesema watawapiga mnada ni ng'ombe ambao wamekamatwa toka mwaka 2013 na serikali inawapa huduma zote kwa gharama zake, kwa sababu ya kukaa muda mrefu hawa ng'ombe 14, basi tarehe 17 itawapiga mnada, lakini hawa wengine kuna muda wa miezi mitatu, miezi sita, na hiyo itatokana baada ya kufanya hayo ambayo Waheshimiwa Wajumbe, wanayataka kuchunguza hayo manung'uniko. Kama kuna mtu ameonewa ina maana hataingia kwenye kundi hilo, lakini kwa hawa waliosemwa watapigwa mnada tarehe 17 hatuna *compromise*, kwa sababu ni mwaka wa tatu na utaratibu ni miezi mitatu hawa tutawapiga mnada. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kidogo tu. Mimi nimshukuru Mhe. Waziri, sana kwa kuweka wazi. Lakini je, hao ng'ombe waliokaa muda huo, mpaka waliozaa nao watapigwa mnada vile vile wa miaka mitatu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, hoja hii tayari imeshaulizwa kwa maswali matatu. Sasa tunaendelea.

Kifungu Q0107	Idara ya Maendeleo ya Ushirika	32,333,000
Kifungu Q0108	Idara ya Wazee na Ustawi wa Jamii	9,580,000
Kifungu Q0110	Idara ya Ajira	41,913,000
Kifungu Q0111	Kamisheni ya Kazi	343,698,000
Kifungu Q0112	Idara ya Usalama na Afya Kazini	47,901,000
Jumla Kuu		**487,400,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU Q01 WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI, WAZEE, VIJANA, WANAWAKE NA WATOTO

Kifungu PQ0101 Programu Kuu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, jana Mhe. Waziri katika maelezo yake alieleza katika kifungu hiki kuwa kuna mikopo hii ya kujitegemea, ambayo anatoa kwa wafanyabiashara wakubwa, wadogo na wa kati. Sasa niliomba anijulishe ni wafanyabiashara gani wanaopata mikopo kama hii.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, maelezo nitayatoa kwa maandishi zaidi.

Mhe. Masoud Abrahaman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, jana nilisema ikiwa kuna wafanyabiashara wakubwa ambao wanapewa fedha hizi za serikali wanakwenda kuagizia biashara adimu kule; kama mchele, sukari na unga na wanatupandishia bei. Je, serikali haioni kama inapata hasara.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nataka kumuambia kwamba, akiangalia kwenye taarifa tuliyotoa, tulisema mikopo tunayoitoa ya mwanzo ni shilingi milioni 50,000,000, na ya juu kabisa ni shilingi milioni 5,000,000. Kwa maana hakuna mtu yeyote mkubwa kiasi hicho anayepewa, na kwa kuwa imekusudiwa kwa ajili ya watu wasio na uwezo, wanaopewa ni wale wasiokuwa na uwezo tu, ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Masoud Abrahman, umeridhika.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ndio. Tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Haya. Mhe. Yussuf Hassan.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi wakati natoa mchango wangu nilimuuliza Mhe. Waziri, lakini naona sikupata majibu. Kuna huu mfuko wa uwezeshaji, lakini kabla mfuko huu kuja wa uwezeshaji, kulikuwa kuna mfuko wa JK na AK. Sasa nilitaka kujua huu mfuko wa uwezeshaji umeridhi deni la kiasi gani kutoka mfuko wa JK na AK, na hatua gani wizara imechukua ili wale wanaodaiwa katika mfuko ule wa nyuma waweze kulipa madeni hayo. Naomba majibu.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba ule mfuko wa JK na AK ulitolewa na kikajitokeza kitu ambacho nimejifunza mara tu nilipoingia kwenye wizara, kwamba wengi waliochukua mifuko ya nyuma walidhani kama wamepewa zawadi, hawakufikiria wala kurudisha. Lakini nikahakikisha kwamba tunaipitia yote. Kama mnafuatilia vizuri, nimesimamisha utoaji wa mikopo kwa muda wa wiki tatu. Hivi sasa nikirudi ofisini niliwapa kazi maalum vijana wangu, ya kwenda kuhakikisha wanafuatilia mikopo na bahati nzuri wamefanyakazi nzuri sana.

Kwanza walikuwa hawana usafiri wa kutosha, namna ya kufuatilia ilikuwa ni ngumu. Lakini kwa zoezi hili wameweza kuongeza zaidi ya milioni 40 za kukusanya. Kwa hivyo, suala hili litakwenda kufuatiliwa na wizara yangu inataka kuahidi kwamba haitatoa mikopo ambayo itapotelea mikononi kwa watu, tutaifuatilia ili wengine wapate kukopa. *(Makofi)*

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante, pamoja na majibu mazuri, nilitaka nimuulize swali jengine dogo tu. Kwa kuwa amesema kwamba mikopo iliyotolewa wakopeshwaji walichukulia kama ni sadaka tu waliopewa. Je, kabla ya kupewa mikopo hawakuelimishwa hawa wakopaji kwamba huu ni mkopo na wanatakiwa warejeshe, wizara haikuchukua juhudi hiyo ya kutoa elimu. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, elimu inatolewa usiku na mchana, na hata pale wanapokuja wanakuja wakiwa wanyonge sana na wanapoomba mikopo utawahurumia na wanaahidi kabisa kwamba watafanya. Lakini ni ubinadamu, mtu anapopata wengine wanakwenda kufanya shughuli nyengine.Tunaendelea kuwaelimisha na tutaendelea kuwafuatilia. *(Makofi)*

Mikopo iliyoridhiwa kutoka kwa JK ni milioni 500, tutaendelea kufuatilia na kuhakikisha kwamba tunaipata.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri. Naam, Mhe. Yussuf Hassan, swali la mwisho hilo.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Kwa vile Mhe. Waziri, ameahidi katika Baraza hili kwamba atahakikisha kwa wale ambao hawakulipa watalipa basi tuendelee. Lakini nitakwenda naye sambamba katika bajeti inayokuja ya mwaka 2017/2018. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Sawa, tuendelee.

Kifungu PQ0101 Programu Kuu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi
Kifungu SQ010101 Programu Ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa Mikopo ya Uwezeshaji 41,230,000
Kifungu SQ010102 Programu Ndogo

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, naomba niwape ruhusa watendaji wa Mhe. Waziri, washuke chini kwa ajili ya ku...

Mhe. Mjumbe Fulani: Wapo chini.

Mhe. Mwenyekiti: Wapo chini hapa, aaah! Naona siwaoni. Mhe. Waziri, wapo chini watendaji wako. Naam, Mhe. Wanu Hafidh Ameir.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia mchango wangu, nilizungumzia kuhusu masuala ya usawa wa kijinsia, sambamba na udhalilishaji ambapo katika fungu hili mimi *concern* yangu itakuwa katika hii programu ndogo ya mapambano dhidi ya udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Mhe. Mwenyekiti, nilimsikiliza vizuri sana Mhe. Waziri wakati anajibu na kwa asilimia kubwa sana nakubaliana na yeye kwamba kifungu cha *18 subsection 1(b)* cha Sheria ya Mtoto kina mapungufu. Nakubaliana naye kwa sababu hakuna ambaye ni mkamilifu na hata hao wanaotunga sheria nao pia ni wanaadamu, wanazoziandika ambazo na sisi huja hapa tukazijadili na kuzipitisha.

Mhe. Mwenyekiti, wakati waziri ananijibu alisema kwamba, mtu mzima anayefanya kosa juu ya mtoto haruhusiwi kusikilizwa katika Mahakama hii ya watoto, kwa maana ya kwamba zile *rape cases*. Lakini Mhe. Mwenyekiti, naomba niibiruwe sentensi ya Mhe. Waziri, nimwambie kwamba, pia kuna watoto ambao wanabaka watoto wenzao kwa kosa la kubaka, ambapo hii kubaka na kulawiti zote ni *sexual offences*, lakini kulawiti inaruhusiwa kusikilizwa katika Mahakama ya mtoto, kubaka hairuhusiwi kusikilizwa katika Mahakama ya mtoto. Sasa kuna watoto ambao wanabaka watoto wenzao na wao hawajafikia miaka 18, lakini bado kesi zao zinasikilizwa katika Mahakama za mikoa, na ambapo ndipo hoja yangu ilipo. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hoja ya Mhe. Waziri, ambayo...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Wanu Hafidh, tupo kwenye usimamizi wa uimarishaji wa vyama vya ushirika, bado hatujafika. Hujamaliza kuuliza swali lako, kwa hivyo, tunaendelea baadae ukifika *part* ya maneno yako tayari Mhe. Waziri, keshayasikia. Kwa hivyo, tunaomba moja kwa moja uende kwenye swali. Mhe. Mjumbe, itakuja. Iko programu ndogo ambayo inazungumzia mapambano dhidi ya udhalilishaji wa wanawake na watoto. Sawa?

UTARATIBU

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Mhe. Mwenyekiti, wakati unaruhusu wajumbe kuzuwia kifungu kikubwa na unatoa nafasi kwa kawaida tatu, sasa ukiruhusu kifungu kikubwa pale mtu anapokitaja halafu tukaondoka, basi vifungu vidogo vidogo tutashindwa kuvizuwia pale. Kwa hivyo, naomba kisome kifungu kikubwa, halafu uruhusu watu kuzuia kwenye vifungu vidogo.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa. Tuendelee.

Kifungu SQ010102 Programu Ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa vyama vya Ushirika

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukuwe fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri, kwa umakini wake na anapoku anajibu hoja kwa ufasaha.Vile vile, nimpongeze Mkurugenzi Khamis Daud Simba Mkuu wa Idara ya Vyama vya Ushirika. Hawa watu katika idara hii huwa wanafanyakazi Jumamosi na Jumapili, hakuna malipo ya *overtime*, sijui Mhe. Waziri, anawaambia nini na ukizingatia ni haki yao ya msingi.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna upendeleo kati ya Mkurugenzi na Watendaji Wakuu, wanalipwa kwa sababu ya shughuli wanazofanya za ziada. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri Mhe. Waziri, hajanifahamu. Kuna watendaji siku za Jumamosi na Jumapili, sio Mkurugenzi tu na watendaji wake, ndio nikasema ni stahiki zao kwa mujibu wa katiba na sheria za kazi, hawa hawapati *overtime* yao. Kama halijui nimwachie muda ili atuletee jawabu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, suala la *overtime* kwa vyovyote kwa mfanyakazi yeyote ambaye anafanyakazi kwa *level* fulani, lakini kwa Wakurugenzi na kuendelea hakuna masuala kama hayo, lakini kwa

wafanyakazi wa chini kwa mujibu wa sheria zinafuatwa na wanawajibu wa kulipwa.

Kwa hivyo, kama wapo ambao wanadai hii *overtime*, wamefanyakazi zaidi ya saa zile za kazi, basi kuna utaratibu wa kisheria wa kulipa suala hilo. Kwa hivyo, hakuna matatizo walete tu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri. Je, niwalete lini leo, kesho au keshokutwa.

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee. Tunaendelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, au tunaendelea.

Mhe. Mwenyekiti: Eee! Tunaendelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hawa ni wafanyakazi wana haki zao, tusije tukapiga mipira, hii ni bajeti. Mwenyekiti, hii ni bajeti tunaijadili ya wananchi, isiwe tunaendesha tu. Nauliza tu niwalete leo, kesho au keshokutwa. Haya ndio majibu ya serikali Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim, nisikilize, usiseme wewe tu na wewe uweze kuwasikiliza watu. Tunaendelea kwa sababu hayo mtazungumza wewe na Mhe. Waziri, uwalete lini, ndio maana yake. *(Makofi)*

Kifungu SQ010102	Programu Ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa vyama vya Ushirika	25,400,000
Kifungu SQ010103	Programu Ndogo ya Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi	460,910,000
Jumla Kuu		**527,540,000**

Kifungu PQ0102	Programu Kuu ya Kukuza Usawa wa Kijinsia na Uendelezaji wa Wanawake

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, twende kwenye vifungu vidogo tumesema. Hapa limetoka wazo la vifungu vidogo ndio tuvipigie buti. Sawa?

Waheshimiwa Wajumbe: Sawa!

Mhe. Mwenyekiti: Haya. Tuendelee.

Kifungu SQ010201

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipochangia hoja hii nilimuambia Mhe. Waziri kwamba, labda tu niseme anielezee kwa maelezo mafupi kwamba suala la wanawake katika kuachana na mume pamoja na watoto wao, ambapo watoto wale wanakuwa mzigo kwa serikali na kupoteza maisha yao kwamba, hawatakuwa na elimu na kila kitu. Nilimuambia Mhe. Waziri, suala hili ataliangaliaje ili mama yule apate haki yake ambayo amesumbuka kwa muda mrefu na baba yule na watoto wale kwa muda wa mwaka mmoja mpaka miaka 18 kuwa watapata haki yao kutoka kwa baba. Kwa hivyo, nilitaka suala hili Mhe. Waziri anieleze, japo alisema kwamba mambo haya yapo kidini. Atayafuatiliaje, anieleze tu ili tuweze kujua ni hatua gani hiyo.

Lakini suala la pili, nilimuelezea kwa maandishi habari ya Magereza, ingawa lilijibika kwamba suala la Magereza watu wanapewa nafasi. Mhe. Mwenyekiti, nililokusudia kwenye suala la Magereza ni kupewa nafasi baba na mama faragha kwa siku nzima, ili kuondosha matatizo. Anieleze suala hili litakwendaje.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru, nadhani Mhe. Sarahani, anakumbuka kama hoja hii pia aliiuliza pia wakati tukichangia na tukipitisha bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na yeye nikamwambia kuna Sheria Nam.4 ya mwaka 1985 ndio inayolinda wajane, wari wote hao wametajwa kwenye sheria ile na kuna utaratibu mzuri wa kupata matunzo kwa wale ambao wamefanya hivyo vitendo, sasa ningemuomba airudie ile sheria aisome kwanza atizame kama kuna hayo ambayo anayauliza hayakuwemo aje sasa atueleze ni maeneo gani ambayo sasa itabidi tu-*improve*, lakini utaratibu wa kisheria umewekwa kwenye sheria hii na hata ukisoma Sheria ya Mtoto upo pia utaratibu. Sasa kama kuna la ziada zaidi ya hili la kisheria basi angetwambia ili tukaelezana nae vizuri. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Suleiman, majibu umeyasikia?

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mheshimiwa, nakubaliana nae nitalifuatilia hilo suala, lakini suala la magereza naona hakunipa vizuri au inakuwaje? Nasema nitaifuatilia ingawa katika mazoe sijawahi kusikia kwa Zanzibar kwamba, kuna mtu ameachwa na watoto pakafanywa mitaala ya malipano,

lakini nitaifuatilia sheria kama Mwanasheria Mkuu alivyoniambia isiwe tatizo hilo naliachia.

Lakini niliuliza kuhusu suala la pili kuhusu suala la magereza kwamba, nilijibiwa na Mhe. Waziri kwamba, wanaachiwa kwenda kuangalia jamaa zao, lakini nilichokusudia wapewe faragha wazee kama ni baba au mama angalau siku moja waweze kuweka mambo sawa ili kupunguza mambo.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kwanza kwa majibu yake ya awali aliyoyatoa kuhusu suala lile la mwanzo la kuwahudumia wajane na watoto pale ndoa zinapokuwa zimetengana, lakini hili suala pia aliliuliza Mhe. Suleiman Sarahan, siku ile ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum na nikamwambia kwamba, utaratibu uliopo sasa hivi ni familia kwenda kuwaangalia wanafunzi wakiwa vyuoni, awe mwanamke au awe mwanamme na wanapewa muda wa kuzungumza.

Lakini lile suala ambalo amelitaja, nilisema kwa sasa hivi kwa mujibu wa sheria halipo lakini tutajifunza kutokana na sheria za nchi nyengine kama itakuwepo nchi ambayo inaruhusu utaratibu huo hatuoni na sisi tusifanye utaratibu huo, kwa hivyo, atupe muda tujifunze na tu-*study* kama kuna haja ya kuweza kuwepo hilo jambo litakuwepo kwa mujibu wa sheria, lakini kwa sasa kwa mujibu wa sheria ziliopo hilo halipo. Nilimjibu siku ile na nilidhani kwamba aliridhika, nadhani Mheshimiwa, airuhusu Serikali ilifanyie kazi hili jambo kama kuna uwezekano tutarekebisha sheria, hakuna uwezekano kwa sababu ya uzoefu wa nchi nyengine halitakuwepo. Lakini kama upo uwezekano basi tutarekebisha sheria, ahsante sana.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Tuendelee Mheshimiwa.

Kifungu FQ 010201 Program ndogo ya uratibu wa masuala ya kijinsia na uendelezaji wa wanawake 178,990,000

Kifungu FQ 01

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa uliniambia kuwa Mhe. Waziri, ameshapata maelezo sina haja ya kurudia ili tu-*save* muda, naomba niende moja kwa moja kwenye hoja yangu, kwamba Waziri yeye atafanya rejea kwenye Sentensi yake na mimi naomba nifanye rejea kwenye Sentensi yangu kwamba, kuna watoto ambao wanaobaka watoto wenziwao, na wao hawajafikia miaka kumi na nane, lakini bado kesi zao zinasikilizwa katika

Mahakama za Mikoa na sio Mahakama za watoto. Sasa utaona hapo mkanganyiko wa sentensi mbili baina ya Waziri na hii ambayo nasema mimi unapotokea, kwa hivyo, naomba ufafanuzi zaidi juu ya hili.

Lakini pia nataka kujua kwamba kuna *cases* ambazo zinatokea wakati yule mfanyaji bado anakuwa mtoto kwa mujibu wa sheria, lakini kesi huenda mpaka yule mtoto akafikia ule umri wa kuwa mtu mzima au akapitiza kuwa ule umri wa mtu mzima. Nilikuwa nataka kujua kwa faida yetu pia kwa faida ya wananchi ambayo haya mashaka ndio yanawakuta hizi kesi zikitokea hivi zinakuwa zinasikilizwaje, zinasikilizwa ki-*juvenile* ama zinasiklizwa kama kesi za kawaida.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Wanu, kwanza nafurahishwa sana kuona kwamba unachangia suala hili na kama ni mama ambaye utakuwa na nafasi kubwa ya kuweza kutetea watoto, ni jambo ambalo linagusa na linaumiza kila mtu, kwa sasa hivi haya ni mapugufu ambayo tumeyaona na tumeanza kuyafanyia kazi kama ni Wizara, kutokana na wakati tuliandaa Sheria ya Watoto ya mwaka 2011, kwa sasa tunafanyia kazi watoto wanaowalawiti na wanaowabaka wasikilizwe katika Mahakama hii, na atahukumiwa kwa umri ambao aliofanya kosa.

Mhe. Wanu, naamini kabisa ukipata muda wa ziada tukakaa pamoja tutafanya mambo mazuri zaidi ili tuweze kutoa mchango unaostahili na nimeona kabisa wewe ni mtu ambaye nitakutumia katika maeneo mengi hata kwenye semina ya Wizara yangu, kwa sababu nataka watu wanaoguswa, mtu asiyeguswa ukimpeleka pahali hafanyi kazi inayostahili, lakini madam unaguswa kiasi hicho naamini kabisa utakuwa na faida kubwa sana kwa Wizara yangu, ahsante sana.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Waziri, kwa majibu yake mazuri, lakini pia nimshukuru Mhe. Wanu, kwa hoja ambayo ameielezea nafasi ya kifungu cha 18 cha Sheria ya Mtoto, sina hakika kama Mhe. Wanu, amesoma pia Jaduweli la pili la sheria ile ile ya mtoto, kama angesoma jaduweli la pili Sheria ya Mtoto angeona pia kuna kesi ambazo zimeorodheshwa zikiwemo hizo ambazo Mhe. Wanu amezitaja ambazo Mahakama ya mtoto pia imepewa uwezo wa kusikiliza. Tatizo lililokuwepo ni kwamba kesi hizi zinakwenda na adhabu kubwa, adhabu ya kesi za kubakwa kifungo chake cha juu ni maisha na kifungo chake cha chini ni miaka 30, sasa Mahakama ya Mkoa uwezo ambao umepewa kusikiliza kesi kifungu chake kisizidi miaka 7.

Sasa ni kweli alichosema Mhe. Wanu, pamoja na haya yote na Mahakama ya Watoto pia imepewa uwezo wa kusikiliza kesi hizo, lakini kwa sababu ya sheria ya mwendo wa jinai kama angeisoma Mhe. Wanu, angeona kwamba Mahakama za Mkoa zimepewa uwezo wa kusikiliza hizi kesi na uwezo wao wa kutoa kifungo ni miaka saba kuja chini, hawana uwezo wa kutoa miaka saba kwenda juu. Sasa kesi za aina hii kifungo chake cha chini kabisa ni miaka 30, ndio maana zinasikilizwa *High Court*, kama zinataka zisikilizwe Mahakama hizi za Mkoa Jaji Mkuu inabidi sasa *extend Jurisdiction* kwa Mahakama ya Mkoa ili iweze kusikiliza kesi hizo. Lakini kwa sasa utaratibu uliokuwepo ni huo na kwa sababu tu ya sheria hizi zilivyo. Nakushukuru Mheshimiwa.(*Makofi*)

Mhe. Wanu Hafidh Amer: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe.Waziri, kwa majibu yake mazuri, lakini pamoja na hayo naomba nimwambie Waziri kwamba, tunapopitisha bajeti tunakuwa tunapitisha pesa za wananchi ambazo tunatoa ridhaa Serikali wakazitumie, kwa hivyo, wanavyosema kwamba tutakaa na tutajibu kwa makaratasi, sisi inakuwa baadae tukishakukaa wakatuletea na hayo makaratasi watakayotujibia, inakuwa tulate kwa sababu pesa tayari tumeshazipitisha.

Lakini nakubaliana na majibu ya Waziri na sina la kuongeza juu ya Waziri, lakini nakuja kwa Mwanasheria Mkuu. Mhe. Mwenyekiti, hakuna Mwanasheria juu ya Mwanasheria Mkuu, kwa hivyo, nakubaliana nae na majibu yake lakini nilikuwa nataka kukiri kwamba *within* majibu yake alikuwa anasema kwamba, kuna sheria ambazo zina matatizo na kwa vyovyote vile itabidi ziletwe hapa tuzifanyie marekebisho, ama watafanya *process*, lakini ninachoomba ni kwamba, Serikali ilete zile sheria hapa haraka iwezekanavyo ili tufanye marekebisho ili kuona kwamba haki za watoto zinapatikana. Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba tuendelee.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba nilitaka kuelewa katika ule udhalilishwaji ambao kuna ndugu zetu tunapeleka nchi za nje, kuna ndugu zetu tayari wamedhalilishwa na tayari tunao, nilitaka kujua hatua gani zinachukuliwa kwa ndugu zetu wale.

Lakini la pili nilitaka kujua mmejipanga vipi katika muendelezo mzima wa hizi kesi za jinai za huu udhalilishaji, kwa sababu inaonekana hakuna *proper person at proper place*, yaani askari anayesimamia kesi haelewi ule utaratibu na zile *terminologies* za kidaktari, nilitoa mfano kwamba daktari anaandika kitu *ruptured* askari haelewi '*ruptured'* maana yake nini, kwa maana ile inaleta chini ile nguvu ya ile kesi. Daktari kaandika '*Traumatic injury'* kaandika pengine

'*inflammation'* yule polisi haelewi na wale kinamama nao *laymen* hawaelewi vile vile, zile kesi haziendi vizuri, matokeo yake ndio tunaona kesi nyingi haziendi kwa mpango unaotakiwa lakini ushahidi upo, inakuwa kitu rahisi hata daktari kuweza kudanganya pale kwa sababu daktari nae akipata chochote anaweza kuandika kitu baada ya mgonjwa kupata *rupture*, daktari akaandika ni *bruises*, lakini polisi nae haelewi mambo hayo yote.

Tumejipanga vipi katika utaratibu huu wa kusimamia kesi hizi ili tupate tupate *proper person at proper place* ili udhalilishaji huu uweze kupungua naomba majibu Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba nimshukuru sana Mhe. Hamad Abdalla Rashid, kwa kutoa taaluma yake za kutumia *Norman cloture* za *Medical terms* na ni kweli naomba nikiri kwamba hivi sasa tumeanzisha *programme* maalum ambayo inaitwa 'huduma ya mkono kwa mkono', huduma ya mkono kwa mkono ipo ukurasa wa 41 wa kitabu cha hotuba ya Mhe. Waziri, ukurasa wa 41 *page* 106, hizi huduma za mkono kwa mkono zinajumuisha wabiya au *partners* wafuatao.Ipo Wizara ya Afya, wapo wale wanaoandika *PF3 Form* ambao ni polisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kipo kitengo cha Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake, na Watoto, na pia kuna mtu mmoja ambae anakuwa *signed* kwenye jamii kufuatilia masuala hayo.

Ni kweli kabisa anachosema Mhe. Mhe. Hamad Abdalla Rashid, tuna *programme* maalum ambayo sasa hivi tunatoa mafunzo tukishirikiana na wenzetu wa *Save The Chilren* ambao wana mpango maalum wa kuelimisha wanaita *'Enforcement Agencies'*, yaani wale askari wa utekelezaji, na ni kweli sio kila mtu anaweza akaelewa *terminologies* za masuala ya afya, si rahisi, lakini wao wanaelimishwa kwa upande wa sheria kidogo na wa *medical terms*, nakadhalika.

Naomba, hii ni *process* ambayo inaendelea ya kutoa mafunzo, naomba atuvumilie tunaendeka *process* hii na baada muda watakuwepo askari maluum ambao pia katika *programme* hiyo *Save The Children* wanapelekwa *University* sasa hivi kusomeshwa, *University* ilokuwepo Tunguu, kusomeshwa *programme* hii tu *'Child Protection and with Enforcement Agency'*, hii *programme* ilioanzishwa pale, baada muda kama miezi sita au miezi nane tutakuwa na askari wazuri sana ambao wana tafsiri nzuri ya sheria na wakati huo huo wanatafsiri ya *medical terms* yakuweza kuwafuatilia ile *PF3 Form* mpaka ifike mwisho wake. Kwa sababu sisi lengo letu lifikie mwisho wa ile *PF3*

kwamba isijazwe tu, ifikie mwisho kabisa kutolewa mpaka hukumu mahakamani ndio lengo letu.Ahsante Mheshimiwa.

Mhe Hamad Abdallah Rashid: Nashukuru Mheshimiwa, kwa majibu mazuri ya Mhe Waziri wa Afya. Kwanza nimpongeze hayo ndio tunayoyataka ili kesi zetu ziende vizuri, lakini naomba nimulize Mhe Waziri wa Afya kupitia Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Je, baada mafunzo haya haitakuwepo ile shughuli ambayo Jamhuri baada ya kumshitaki mshitakiwa kwa kesi maalum anatokea mzazi anasema aachiliwe?

Mhe Naibu Spika: Mheshimiwa, kiutaratibu huwezi kuuliza swali jengine, kwa sababu umeshauliza na umeshajibiwa maswali yako, unawanyima sasa wenzako nafasi, nao waweze kuleta hoja zao, nafikiri unauliza swala jengine jipya la pili. Mheshimiwa, mimi nilitegemea kwamba, sasa utasema basi tuendele na tumekubaliana na Mheshimiwa.

Mhe Hamad Abdallah Rashid: Tusiendele Mhe Naibu Spika, bado moja, moja amelifafanuwa Mhe Naibu Waziri, kama nilivyompongeza, hili la wale wenzetu walopata madhara au udhalishaji nchi za nje.

Mhe. Mwenyekiti: Hilo sawa hujajibiwa, lakini pia kwa *future* ilikuwa katika kifungu hichi unauliza suala hili moja, huwezi kuuliza masuala mawili, hatukukwambia tu, lakini hilo nitakuombea kwa Mhe. Waziri akujibu.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kabisa unasema kuna *echo* kubwa inayotokea humu ndani, mtu akisema kwa haraka haraka humpati na akikaa pembeni kidogo ya *mic* tunakuwa hatupati, unaweza kunisaidia kurudia tena.

Mhe Hamad Abdallah Rashid: Ahsante Mhe. Waziri, narudia kidogo kidogo.Katika hichi kipengele cha udhalilishaji wanawake, pengine hata na wanaume, kuna ndugu zetu ambao Wizara yako ina mikataba na watu hawa binafsi wanasafirisha wananchi nchi za nje kufanya kazi, tunasema kwamba wanadhalilishwa kule nchi za nje. Hivi ni hatua gani au kesi ngapi umezipata katika Wizara yako na hatua gani mmechukua katika kuhakikisha udhalilishaji huu nchi za nje unaondoka kwa ndugu wa Zanzibari wanaokwenda huko.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kabisa kama utakumbuka nilipokuwa najibu suala na kusema jinsi gani utaratibu umewekwa makusudi wa kuanzisha kamishina inayowasiliana na ubalozi nchi za nje, na kuhakikisha kwamba wale

watu wanaotaka ajira kutoka kwetu wanakuwa na mikataba ambayo inabidi iandikwe kabla ya ndugu zetu na watoto wetu hawajatoka mahali hapo na ufuatiliaji umekuwepo.

Inawezekana kuna matukio yanayojitokeza kwamba kule wanadhalilishwa, ndio maana kuwaambia kwa pamoja kabisa kama utakumbuka nimesema kwa muda mchache kwamba kuna makusudi ya kutaka kufuatilia, na Kamisheni wangu alikuwa tayari kutaka kufuatilia masuala haya akajionee mwenyewe na kufuatilia viongozi wanaohusika kule ambao ni mabalozi na hao waajiri na nimekuwa nikipata mawazo haya ndani mwenu humu humu wengine wameandika kwa maandishi kwa jinsi gani tufanye utaratibu ndugu zetu wasipate kudhalilishwa.

Tunaomba kabisa nyinyi kama ni wazazi muwashauri wengine wanakwenda siku mbili wanarudi, wanaema tulitaka kwenda kuangalia nje tu na sisi tuseme kwamba tumetoka na wakija huku wanakuja na hadithi nyingi baada ya kuona kwamba wanakaa hawana kazi, kwa hivyo, hayo ni masuala ambayo tunayafuatilia na tunataka kuhakikisha kwamba haya yote yanayozungumzwa tuthibitishe, hatutaki kuwafanya ndugu zetu wakanyanyaswa na wakadhalilishwe eti kwa kuwa hakuna kazi, kazi zinaendelea kufanywa na Wizara na maandalizi mazuri kwa ajili ya nchi yetu, sijui kama imetosha kukujibu.

Mhe hamad Abdallah Rashid: Imetosha Mheshimiwa, tuendelee.

Mhe. Naibu Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe, tumemaliza hoja tatu katika kifungu hichi tunaendelea.

Kifungu SQ 010202	Program ndogo ya mapambano dhidi ya usalilishaji wa wanawake na watoto	311,100,000
JUMLA		**490,090,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu PQ 0103 Program Kuu ya Kuimarisha Huduma za Ustawi

Kifungu kidogo SQ 010301

Mhe. Mwenyekiti: Sasa nyingi mmesimama kwa kufungu gani? Tumekubaliana mwanzo kwamba watu wanapiga buti vifungu vidogo, vidogo, lakini kabla ya kusomwa hivyo vifungu vidogo, nyinyi mmepiga buti.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilikuwa na moja wakati ninachangia kwa maandishi nilizungumzia suala la *Child Policy Protection*, nilikuwa ninamuuliza Mhe. Waziri, katika kujipanga kwa kushirikiana pamoja na Wizara ya Elimu, kwa sababu udhalilishaji hufanyika maeneo mengi.Wizara yake itajipangaje kwa kushirikiana pamoja na Wizara ya Elimu kuhakikisha kwamba hiyo *Child Policy Protection* sera ambazo tayari na sheria zipo zinakuwa *implemented* katika wizara yake pamoja kwa jumla ili kulinda haki za watoto na vijana wetu maskulini.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, utaona kabisa kabisa labda mimi naweza kuona kwamba jirani yangu hapa ni Waziri wa Elimu, kwa sababu mambo mengi yanayomgusa yeye ni ya kwangu hasa unaposema "watoto", mimi wananihusu watoto wote, kwa hiyo, kwa karibu kabisa yeye angalau watoto wake wanaanza darasa la saba na kuendelea. Mimi ni watoto wote pamoja na yule anayetarajiwa kuzaliwa mimi ninamhesabu ni mtoto katika wizara yangu. Kwa hivyo, kwa makusudi kabisa tumeshakutana mara ya kwanza na tutaendelea kukutana tena na tunaomba ushirikiano wenu.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, majibu aliyoyatoa Mhe. Waziri, ni mazuri, lakini bado sijaridhika nayo yaani kwamba nikafahamu. Ninachokiuliza labda kama nitafahamika zaidi, nataka kufahamu wizara yake japokuwa tayari limeshazungumzwa katika baadhi zilizopita kwamba tayari sheria zipo, lakini sasa hivi tunazungumza na serikali na wizara hii moja ni muhimu. Ni kwamba wizara yake inajipangaje kwa sababu yeye kama alivyosema kule analinda watoto wote kwa pamoja.

Lakini tuna tatizo hili la watoto ambao wanapokea ujauzito mashuleni. Yeye kama waziri husika katika kulinda maslahi na watoto wetu, vijana na wanawake wote kwa ujumla anajipangaje kuhakikisha kwamba hii sera ya *Child Policy Protection* inakuwa *implemented* pamoja katika hizo wizara, pamoja na elimu kuhakikisha kwamba hawa watoto wanalindwa? Kwa sababu sheria zipo nyingi, ni utaratibu wa kuzifuata na Mwanasheria Mkuu alizungumza katika bajeti ya Wizara ya Elimu kwamba, sheria zipo na sera zipo. Lakini sasa hii sera kuhakikisha kwamba inakuwa *implemented* katika Wizara ya Elimu ili kutokomeza hizi mimba za watoto ambao wanazipata ambao maisha yao mwisho ni kuharibikiwa.

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza sera hizi za *Child Policy Protection*, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imeanzisha kitengo kinaitwa "Elimu, Mjumuisho na *Study* za Maisha". Katika kitengo hiki kuna sehemu inayohusika na *guidance and counseling* ya watoto wa kike na tunafanya zaidi katika *prevension* zaidi kuwaeleza wataalam wetu wanawatembelea wanafunzi wa kike kuwaeleza namna ya kuweza kujikinga, namna ya kuweza kukwepa mitego na masuala kama hayo. Wale ambao watakuwa wameathirika pia tunatoa ushauri nasaha kupitia kitengo hicho. Kazi hii kama nilivyosema pamoja kwa ushirikiano na wizara inayohusika na wanawake na watoto.

Napenda hapa nimshukuru sana, sitaki nitaje lakini wizara hii wakati mwengine inatupatia taarifa za udhalilishaji za siri na sisi tunafuatilia na tumefanikiwa kuzuia baadhi ya matokeo katika skuli zetu. Ahsante sana.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru majibu mazuri aliyotoa Mhe. Naibu Waziri kwa niaba ya Waziri, basi ikiwa hiyo *policy* tayari ipo ya *prevention* ambayo wameanza nayo, basi na mimi nitaomba nipate kuiona, tuletewe pamoja na wajumbe wengine ili tuweze kujua siku za mbele, kwa sababu huko majimboni tayari hili jambo limekuwa ni janga, tuweze kujua. Naishauri wizara husika waanze kufanya kampeni za pamoja ili kwenye vyombo vya habari hizi taarifa zote zilizofika nchini, pia na walimu katika kulinda maslahi ya watoto.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, ushauri umetolewa.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana nimeupokea, ninakushukuru.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, na mimi katika kuchangia kwangu nilimuuliza waziri suala la malezi ya wazee, maana yake katika nyumba zetu utakuta mzee katupwa huko nyuma halafu hali ni mbaya, lakini kila mtu anayeuliza anaambiwa aa, ana watoto wake, huwezi kutia mdomo. Lakini mzee yule anadhalilika sana, maana mwananchi ndio mtu wa serikali, sasa kama wizara inalichukuliaje jambo hili kwamba, tunafuata watoto mpaka wamuue yule mzee au serikali ina mkondo wake.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwakilishi, nataka kukwambia kuwa pale kwenye nyumba za wazee kuna nyumba za kuweza kuweka wazee 144. Mpaka sasa hivi ni kama vyumba

38 ambavyo vina wazee vyumba vyote viko wazi. Tulipojaribu kufuatilia wengine ni kama hivyo ulivyosema kwamba, watoto hawataki kuwapeleka wazee wao, wanaona kama ni aibu. Lakini kwa taarifa yako uliyotupa tutafanya makusudi tuweze kufuatilia na kwa kutumia kama jinsi tunavyopata zaidi ya miaka 70, kwa mfumo huo huo tutafatilia kwa kutumia mashehia na *Local Government* zilizoko kuhakikisha kwamba tunawa-*identify* hawa wazee wa namna hiyo. Kwa sababu si haki mzazi kuwekwa akanyanyaswa, wakati kuna mahali ambapo anaweza kupewa akatunzwa na kwa gharama za serikali. Wewe kama Mwakilishi, ninakuomba sana kama wapo kwako tuambie tutawafuata ili waweze kuwekwa mahali panapostahiki.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nataka niunge mkono hoja zake, lakini Wawakilishi wenzangu hapa, mimi nataka niseme tu kuwa ninavyozungumza mimi ukenda jela kwa kusemea ile na mimi ninaweza nikatiwa jela, nikiwa mzee na mimi yanaweza yakanifika, mimi nikifika serikali ije inichukue isiwaachie watoto wakaniua.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi suala langu dogo sana wala sina nia ya kutaka kupiga buti, ninamuuliza Mhe. Waziri, ni lini alitembelea nyumba ya kulea watoto waliokuwa Mazizini, kama ameshafanya ziara au hajafanya ziara.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mheshimiwa, nataka kukwambia tu kwamba, ile ni njia yangu ya kwenda Ofisini. Nimeshatembelea pale zaidi ya mara 7. Mara ya kwanza, nilipoingia wizarani sikutaka kumwambia mtu kwamba ninakwenda kutembelea, nilikuwa ninatembelea kwa siri. Maeneo yangu yote ya kazi niliyokwenda sijatangaza popote ili nikute hali halisi, nikishajua hatimaye ndio nakwenda na viongozi na watendaji ili wanambie haya, kama wanadanganya ninawashushua pale pale.

Sasa niliwatembelea mara ya kwanza nilikuta ile nyumba inavuja nikatoa maagizo na ikafanyiwa marekebisho yaliyochukua zaidi ya shilingi milioni 3, kwa mara moja sasa hivi hapavuji, watoto wananifahamu sasa hivi, kwa sababu sasa hivi wanajua anayetembelea hapa ni Waziri. Na wewe kwa mfungo wa Ramadhani nadhani ni wakati mzuri wa kutoa sadaka kwa watoto.*(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nimshukuru sana Mhe. Waziri, maana yake nilimpa mtego kidogo na akaupangua. Tuendelee.

Kifungu kidogo SQ 010301	Program ndogo ya Uratibu au huduma za uhifadhi wa jamii	5,072,960,000

Kifungu kidogo SQ 010302 Program ndogo ya Maendeleo ya Vijana 337,480,000

Jumla ya Program Kuu **5,410,440,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu PQ 0104 Program Kuu ya Uongozi na Mipango ya Kazi Uwezeshaji Wazee Vijana Wanawake na Watoto

Kifungu Kidogo Q 010401 Program ndogo

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, niendelee kushukuru kwanza na nikushukuru katika kipindi kile ulikuja na hoja binafsi humu ndani ya Baraza kwa umakini wako Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa dhati kabisa na nikupongeze kwa jinsi unavyoumwa na watoto, ni Mwakilishi pekee uliyekuja na hoja binafsi ya suala hili, ingawa wengine tuko nyuma kwenye sekta ya Wizara ya Afya. Serikali hapa kwa muda mrefu imetuahidi mashine ya *DNA*, leo nataka kuhoji na ninashukuru serikali nzima ipo, nikiangalia kwa haraka haraka wapo, hebu watwambie ile mashine ya *DNA* imefikia wapi, ipo au haipo ili wananchi wapate kujua.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kama ambavyo Mhe. Jaku, amesema, *of course*, suala hili tumekuwa tukilizungumza kwa muda mrefu. Kuna wale ambao walikuwa wakisema ikiletwa itasaidia na kuna wale ambao walikuwa wakisema ni rahisi kupeleka Dar-es-Salaam kuliko kuwekwa hapa kwa hali ilivyo. Lakini serikali ikatoa maamuzi kama kile chombo kinunuliwe, huo ndio uamuzi wa serikali. Kwa sababu kuna *program* ya *Legal Sector Reform* fedha zake zimetengwa kwenye ile *program* ya *Legal Sector Reform*, sasa zile zinakwenda kwa awamu, unamaliza *program* moja ndio inakuja *program* nyengine. Sasa kusema lini hilo siwezi nikamjibu kwa sababu zile zinakwenda na *program* ni *program* ya miaka 5, lakini tunamuahidi uamuzi wa serikali kwenye chombo hiki cha *DNA* kwa sababu kimekuwa cha muda mrefu uamuzi kinunuliwe.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwanasheria Mkuu, mimi ninamuheshimu sana, lakini kwa hili itabidi kidogo hata kama atasalisha mimi itabidi nisimfate kwa hili, hili suala Mhe. Mwenyekiti, uzuri wewe mwenyewe ulikuwa shahidi, serikali miak 4 na huu wa 5 kuingia wa 6 tupo hapa, waseme tu serikali limeshindikana hili suala ili wananchi wakapata kujua, haina haja kuzongana, huu mwezi mtukufu wa Ramadhani. Waseme serikali, serikali ipo

wameshindwa hili suala, si aibu kushindwa, vibaya kuiba, lakini kushindwa si kitu kidogo, Serikali iseme; "nimeshindwa bwana" kurejesha kauli sio tatizo, wananchi wapate kufahamu.

Narudia tena Mhe. Mwenyekiti, serikali hii isingekuwepo madarakani bila ya kuwepo wananchi, wananchi ndio walioweka serikali madarakani, kama kushindwa hakuna tatizo, tuliambiwa kifaa cha *DNA* kimo ndani ya meli, Juma Duni kakaa pale. Tuelezwe tu kama ile meli imeharibika au vipi ili tujuwe! Huu si ustaarabu kabisa.Wananchi wanatusikiliza na wana imani na Baraza hili, leo tunataka kujitia matope kwa suala hili, Serikali iseme tu wala si aibu kushindwa, lugha ndogo tu imeshindwa.

Mhe. Mwenyekiti: Umeeleweka Mheshimiwa, mwache Mwanasheria Mkuu akupe majibu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba Mhe. Jaku, afahamu kama yeye anavyoumwa na jambo hili na sisi sote linatuuma, kwa sababu na sisi pia ni wazazi, sisi pia tuna watoto, sisi pia tuna ndugu. Kwa hivyo, haya anayozungumza yeye asidhani yanamuumiza yeye peke yake na sisi sote, mimi ninakuhakikishia Mhe. Mwenyekiti, yanatuuma. Na wewe ndio uliokuwa kiongozi ulioleta hoja binafsi ya mambo haya. Tumezungumza kwa muda mrefu ofisini kwangu juu ya mambo haya. Ninavyosema mimi na ninavyolifahamu, kwamba ni kweli tatizo hili limezunguzwa kwa muda mrefu na maamuzi ya serikali ni kwamba kifaa hiki kinunuliwe.

Kununuliwa kwake kimetiwa kwenye *program* ya *Legal Sector Reform* na zile fedha zinatolewa kwa awamu.

Sasa itakapofika awamu ya kununuliwa kile kifaa kitanunuliwa, wala sio fedha nyingi za kusema Mhe. Jaku, serikali imeshindwa kununua kifaa cha *DNA*, wala si pesa nyingi. Lakini awe na subra na wala asijenge hoja ya kama wengine wote humu hawaumwi na jambo hili, anayeumwa ni yeye tu peke yake. Sote Mhe. Mwenyekiti, hili jambo linatuuma kama ambavyo linawauma Waheshimiwa Wajumbe wote humu. Lakini hiyo ndio ahadi ambayo imetolewa na Serikali na hivyo ndivyo ambavyo tutakavyolishughulikia. Ninakushukuru.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nilichozungumza mimi ni Kiswahili, tena labda nizungumze kwa lugha nyepesi kidogo apate kunisikia. Serikali iliahidi ndani ya chombo hiki, Mhe. Mwenyekiti, kama ulikuwa makini na ulifuatilia Serikali iliahidi kwamba; 'chombo kimo kwenye

meli, itafika muda mfupi', wajumbe waliopo waje wanisaidie ni kweli au uongo. Sasa waseme, tumefunga.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku, ninakuomba kwa hisani yako, nasemaje aliyeahidi hayupo japokuwa serikali ipo.Sasa sikiliza Mhe. Mwanasheria Mkuu, ameshatoa maelezo mazuri sana ya kuwa wewe uridhike kwamba, ni *process* kubwa, sio jambo la leo au kesho mashine ikapatikana, tusubiri mwaka ujao Mungu atakuweka uhai utakuja kuiuliza serikali. Lakini tusi-*prolong* maneno na nini haisaidii Mheshimiwa, umenifaham?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ngoja mimi nilichouliza ni Kiswahili kidogo tu, tumeahidiwa ndani ya chombo hiki tena kwa lugha ya Kiswahili mashine ya *DNA* imo kwenye meli muda mfupi itafika, sasa wajibu tu kuwa labda mfadhili hajapatikana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku, tuache tuendelee, tuache ninakuomba, majibu umeshapata.
Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Wananchi watatuhukumu huko, tuendelee.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaingia katika suala hili la *DNA*, mimi ningeomba kujua hii *DNA* ina-*cost* fedha kiasi gani na ina ukubwa gani na kwa nini mpaka leo haijafika. Naomba kujua hii *DNA* ina-*cost*...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir, hili lishajibiwa tena unauliza nini, hili tumemaliza. Kama huna jengine Mheshimiwa, basi.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, hajaahidi mtu iliahidi serikali, sasa kwa nini jambo kama hili tuliachiwa wakati ni muhimu, mimi nataka kujua fedha kiasi gani ya hiki kifaa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, tufate kanuni, hili limepita.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, jambo hili mnalipeleka mnavyotaka nyinyi, lakini hatulikubali Wawakilishi, kwa sababu tunadanganywa, kwa nini tusiambiwe?

Mhe. Mwenyekiti: Sasa Mheshimiwa, unaingilia kazi yangu sasa. Hili tumelimaliza, tumesema tumelimaliza, tuendelee na jengine.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kuniona na mimi wakati ninachangia kwa maandishi kwa vile sikupata nafasi ya kuchangia niliandika kwa maandishi kwamba, nilishauri katika nyumba ambazo za wazee kutokana na hii wizara ni kubwa na ina mambo mengi mazito na kwa kumsaidia Mhe. Waziri, nilitoa wazo kwamba, katika majengo ya Nyumba za Wazee Sebleni ili kuhakikisha kwamba zile nyumba zinakuwa zinapata matengenezo yake niliandika kwamba kuna utaratibu unatumika nchi za Ulaya na hata nchi za jirani unakuwa unatafuta familia au kampuni wanaweka kama kibao halafu unasema kwamba jengo hili linatengenezwa na kutiwa rangi kwa mwaka mzima na familia ya Mhe. Suleiman Sarahan, kwa pamoja.

Wao familia kila mwisho wa mwaka unapeleka *invoice* yako kama milioni mbili ile familia inalipa rangi, jengo linakuwa linashughulikiwa. Lakini katika mchango wako sikulisikia, sasa sijui kama ile karatasi ilifika. Lakini naomba ulichukuwe hili wazo na ulifanyie utafiti na nitakuwa niko tayari kukusaidia kwa siku za mbele.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mheshimiwa, naendelea sana kuheshimu michango yako kwa sababu una upeo mkubwa na pia, nalichukua. Ahsante sana.

Kifungu SQ010302 Maendeleo ya Vijana
Kifungu Kidogo HQ 01030201

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ninashukuru Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia nilimwambia Waziri kwamba, kwa hali inavyokwenda kwamba wanaume nao wanahitaji kupata Idara ya kusemea mambo yao kwa wale wanaoonewa. Mheshimiwa, hakulisemea hili. Ningeshauri aliseme kidogo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba mtakuwa mmechelewa wanaume wenyewe, kwa sababu katika maeneo mengi hata sisi katika masuala ya Wakristo mpaka wanaume wana *forum* ya wanaume wajadili, wapange na sio kupanga tu, waoneshe ubabe wao kwamba ni wanaume kwamba, wanaweza kufanya mambo mengi mazuri kwenye familia kama vichwa vya familia. Kwa hivyo, naomba kabisa kama una wazo zuri na maelezo unaweza kuyaleta basi karibuni muanzishe chama cha wanaume, nadhani mtaweza kutatua mambo mengi kwa urahisi zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa, kwa taarifa yenu ipo Jumuiya ya Akinababa ambao wanashirikiana sana na wizara hiyo. Kwa hivyo, Mhe. Suleiman, unaweza kwenda ukajiunga na wewe.

Kifungu SQ 010401	Programu Ndogo ya Kusimamia Mipango Sera na Tafiti za Wizara	75,000,000
Kifungu SQ 010402	Programu Ndogo ya Usimamizi wa Huduma za Utawala na Utumishi	2,149,300,000
Kifungu SQ 010403	Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba	

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyekiti wangu wa Kamati Mhe. Ali Suleiman (Shihata), kwa umakini wake kwenye kamati hii. Kwa muda mrefu kule kuna kiwanja na wizara inaendelea kukodi nyumba. Je, kuna mpango gani wa kujenga ofisi ile ikiwa kipindi hiki karibu miaka sita au saba wizara inakodi jengo na pesa nyingi zinapotea.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima nataka kusema tu nimemtambua kabisa kwamba Mhe. Jaku, kuwa yeye ni Mjumbe wa Kamati na yeye ndiye aliyetushauri mambo mengi katika haya. Sasa labda kuna mahali ameweza kuchangia vizuri, basi nataka kumuhakikishia kwamba, kuna maandalizi ya ujenzi yanaendelea na yanafanyiwa kazi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti, hili nimemuuliza kwa maslahi tu, tumeshalizungumza kwenye kamati, lakini wananchi wanataka kufahamu tu ukweli wenyewe, naomba tuendelee.

Kifungu SQ 010403	Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba	3,322,889,000
	Jumla Kuu	**5,547,189,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu PQ 0105 Programu Kuu ya Kuratibu Uzalishaji, Upatikanaji wa Ajira za Staha na Usimamizi wa Utekelezaji wa Sheria

Kifungu SQ 010501	Programu Ndogo ya Ukuzaji na Upatikanaji wa Ajira za Staha	29,512,000
Kifungu SQ 010502	Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini	37,339,000
Kifungu SQ 010503	Programu Ndogo ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kimataifa na Majadiliano ya pamoja Kazini	62,350,000
	Jumla	**29,201,000**
	Jumla Kuu	**12,104,460,000**

(Baraza linarudia)

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza iyakubali makadirio hayo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri, ameshatoa hoja, sasa niwaulize wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri, nikupongeze sana kwa kupitisha bajeti yako, wewe pamoja na watendaji wako wote, lakini basi nikutakie kheri na mafanikio katika utekelezaji wako na naomba sana ukumbuke kwamba kuna mwaka 2017/2018.

Kwa hiyo, nakuomba sana kwamba yale yote ambayo umeyaahidi kwamba utayatekeleza uwafanyie Waheshimiwa Wajumbe, ili waweze kupitisha kirahisi hotuba yako ukifika mwaka huo, na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atakupa wepesi.

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa
Mwaka wa Fedha 2016/2017 –
Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu sasa likae kama kamati ili liweze kupokea, kujadili na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, aidha, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uzima na afya njema na kwa kuniwezesha kwa niaba ya wafanyakazi wenzangu kuwasilisha mbele ya Baraza lako hotuba ya Wizara Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mhe. Naibu Spika, kwa furaha kubwa naomba nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuchaguliwa tena na wananchi kuendelea Kuiongoza Zanzibar kwa ushindi mkubwa katika uchaguzi wa marudio uliofanyika Machi 20, 2016.Kuchaguliwa kwake kumedhihirisha kukubalika kwake kwa wananchi kutokana na uongozi wake imara wenye busara na hekima nyingi katika kuwaletea maendeleo wananchi wa nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kuteuliwa tena kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Kuteuliwa kwake na Mhe. Rais wa Zanzibar ni ushahidi wa uwajibikaji katika kutekeleza majukumu ya serikali na kutoa mchango wako katika kuwaletea wananchi maendeleo katika shughuli zao za kila siku.

Mhe. Naibu Spika, kwa namna ya kipekee napenda kukupongeza kwa dhati wewe binafsi pamoja na Spika kwa kuchaguliwa kwenu kuwa Spika na Naibu Spika wa Baraza la Tisa la Wawakilishi, tunamuomba Mwenyezi Mungu akuzidishieni uwezo, hekima, busara na uadilifu katika kuliongoza vyema Baraza letu hili. Vile vile, naomba kuwapongeza Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waliochaguliwa na wananchi na walioteuliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar kupitia viti maalum ili kuweza kushirikiana na serikali katika kutatua changamoto zinazowakabili wananchi. Aidha, shukurani za pekee ziwaendee wanachama, watendaji na viongozi wa UWT na Chama cha Mapinduzi kwa kunipa nafasi ya pekee kuwawakilisha ndani ya Baraza hili.

Mhe. Naibu Spika, naomba pia niungane na wafanyakazi wenzangu kutoa mkono wa pole kwa wananchi wote walioathirika kutokana na maafa yaliotokana na mvua kubwa zilizonyesha katika visiwa vyetu. Sote tunaamini kwamba mvua ni neema, lakini haya yote yametokea kutokana na kudra ya Mwenyezi Mungu Muumba Mbingu na Ardhi. Hivyo, tunamuomba Mwenyezi Mungu awape subra wale wote ambao kwa namna moja au nyengine wamefikwa na maafa hayo.

Mhe. Naibu Spika, naomba uniruhusu kuelezea utekelezaji wa shughuli za wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na muelekeo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kama ifuatavyo:-

Mapato na Matumizi:

Mhe. Naibu Spika, suala la ukusanyaji wa mapato ni kiashiria muhimu sana katika kupima mafanikio ya utekelezaji. Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2015/2016 ilipangiwa kukusanya jumla ya Tsh 4,799,625,000/= kutokana na vyanzo mbali mbali vya taasisi zake. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016 jumla ya Tsh 3,596,948,678/= zimekusanywa. Kiwango hiki ni sawa na asilimia 75% ya makadirio. (Kwa ufafanuzi zaidi naomba angalia **kiambatanisho "A**").

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa matumizi ya mwaka wa fedha 2015/16, wizara yangu imepangiwa kutumia jumla ya Tsh 35,949,460,587 /=. Kati ya fedha hizo kazi za kawaida ni Tsh 7,198,900,000 /= na kazi za maendeleo ni Tsh 28,750,560,587 /=. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016 wizara yangu ilikwishapatiwa Tsh 3,838,441,267/= kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 13.4% na Tsh 5,319,579,160/= kwa kazi za kawaida, sawa na asilimia 74 %ya makadirio. Hivyo, kufanya jumla ya fedha zote zilizopatikana kuwa ni Tsh 9,152,556,878/= sawa na asilimia 25.5% ya makisio yote. (Kwa ufafanuzi zaidi angalia **kiambatanisho B1 na B2**).

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa utekelezaji wa shughuli za wizara, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, wizara yangu ilifanikiwa kutekeleza majukumu yake kupitia programu kuu tano zifuatazo:-

1. Programu ya Mipango, Sera na Utawala wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.
2. Programu ya Usimamizi na Upangaji wa Matumizi ya Ardhi.
3. Programu ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe, Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Ujenzi na Nyumba za Serikali.

4. Programu ya Usimamizi wa Huduma za Uzalishaji na Usambazaji wa Nishati na Maji na
5 Programu ya Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi.

PROGRAMU YA MIPANGO, SERA NA UTAWALA WA ARDHI, MAKAAZI, MAJI NA NISHATI

Mhe. Naibu Spika, programu hii ilikuwa na jukumu la uratibu katika utekelezaji wa kazi za wizara. Programu hii inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Utumishi na Uendeshaji, na Afisi Kuu Pemba kupitia programu ndogo tatu ambazo ni Mipango na Sera za Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, Utawala na Maendeleo ya Rasilimali watu pamoja na programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati Pemba.

PROGRAMU NDOGO YA MIPANGO NA SERA ZA ARDHI, MAKAAZI, MAJI NA NISHATI.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 utekelezaji wa programu hii ndogo ulilenga kutekeleza shughuli za Kuratibu/Kuandaa Mipango na Miongozo ya Kisera ya utekelezaji wa kazi za wizara, kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa programu na miradi na shughuli za wizara pamoja na kuendeleza tafiti kwa ajili ya kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma katika sekta za wizara.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia mwezi wa Machi, 2016, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imefanikiwa kutekeleza mambo yafuatayo kwenye programu hii ndogo.

Kuratibu shughuli zote za Wizara ikiwemo Programu na Miradi ya Maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa miradi ya maendeleo, idara imesimamia Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa kufanya kazi za uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji (*monitoring and evaluation*) kwa lengo la kuhakikisha kwamba miradi hiyo inatekelezwa kwa ufanisi kama ilivyopangwa. Miradi iliyosimamiwa na Idara hii ni hii ifuatayo:-

i. Usambazaji Umeme Vijijini;
ii. Uimarishaji wa Miundombinu ya Umeme na Kulijengea uwezo Shirika.
iii. Usambazaji Maji Vijijini;
iv. Uimarishaji wa Shughuli za Maji Mijini;

v. Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji Awamu ya Pili;
vi. Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira;
vii. Utekelezaji wa Sera ya Nishati;
viii. Utafiti wa Nishati Mbadala.

Kuandaa Miongozo ya Kisera na Kisheria

Mhe. Naibu Spika, katika uandaaji wa miongozo ya kisera na kisheria, wizara imekamilisha utayarishaji wa Rasimu ya Sera na Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia na hivi sasa ipo katika hatua za mwisho za ukamilishwaji wake. Hatua hii itaihakikishia Zanzibar kupata fursa ya uendelezaji wa shughuli za mafuta na gesi asilia.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, katika kutekeleza programu ndogo ya Mipango na Sera za Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, jumla ya Tsh 161,884,000/= ziliidhinishwa kutumika. Hadi kufikia Machi, 2016, fedha zilizoingizwa ni Tsh 101,654,949/= sawa na asilimia 63% ya Makadirio.

PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA NA MAENDELEO YA RASILIMALI WATU

Mhe. Naibu Spika, programu hii ndogo inatekelezwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji na inajukumu la usimamizi na utawala wa rasilimali za wizara ambapo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 iliweza kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuajiri wafanyakazi 12 katika fani mbali mbali ambazo zilihitajiwa kujazwa kwa sababu tofauti ili kuongeza ufanisi wa kazi kwa kutoa huduma zenye tija kwa wananchi;

ii. Jumla ya wafanyakazi 546 wamepatiwa fursa ya kushiriki mafunzo mafupi, wafanyakazi 162 wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu na jumla ya wafanyakazi 41 wamemaliza mafunzo ya muda mrefu;

iii. Iliratibu shughuli za kustaafisha wafanyakazi na kuwatayarishia mafao yao ambapo jumla ya wafanyakazi 45 walistaafu na kuratibiwa mafao yao. (Kwa ufafanuzi zaidi wa uendelezaji wa mafunzo **Viambatanisho C na D** vinahusika).

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, katika kutekeleza programu ndogo ya Utawala na Maendeleo ya Rasilimali watu, jumla ya Tsh

804,252,000/= ziliidhinishwa kutumika. Hadi kufikia Machi, 2016, fedha zilizoingizwa ni Tsh 570,016,314/= sawa na asilimia 71% ya makadirio.

PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA SHUGHULI ZA ARDHI, MAKAAZI, MAJI NA NISHATI PEMBA

Mhe. Naibu Spika, programu hii ndogo inatekelezwa na Ofisi Kuu Pemba na ina jukumu la uratibu na usimamizi thabiti wa kazi za wizara ikiwemo Programu na Miradi ya Maendeleo kwa Pemba ambapo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 iliweza kutekeleza yafuatayo:-

i. Kufanya utambuzi wa maeneo (*parcels*) 4,939 katika maeneo ya Kiungoni, Limbani, Selemu na Kipangani kwa Wilaya ya Wete. Wara, Msingini na Mkoroshoni kwa Wilaya ya Chake Chake. Chokocho, Uweleni na Ng'ombeni kwa Wilaya ya Mkoani pamoja na kusajili jumla ya maeneo (*parsels*) 544 yaliyofanyiwa utambuzi. Vile vile, taratibu za kuwapatia kadi za usajili wa ardhi wananchi 236 ambao wameomba kupatiwa kadi hizo tayari zimeanza;

ii. Jumla ya hatimiliki za matumizi ya ardhi 58 zimetayarishwa kati ya hizo hati za muda (*provisional*) ni 34 na hati za kudumu ni 24;

iii. Kukamilishwa kwa kazi ya uthamini wa nyumba zilizoathirika katika ujenzi wa barabara ya Ole/ Kengeja na uthamini wa mimea katika barabara ya Bahanasa /Mtambwe. Vile vile, kazi za uthamini wa maombi 138 ya uhaulishaji wa ardhi zimefanywa;

iv. Jumla ya viwanja 324 vimepimwa kwa ajili ya shughuli mbali mbali kama vile makaazi, biashara, taasisi, vitega uchumi mashamba na mengineo.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, katika kutekeleza programu ndogo ya uratibu wa shughuli za Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati Pemba, jumla ya Tsh 1,018,229,000/= ziliidhinishwa kutumika. Hadi kufikia Machi, 2016, fedha zilizoingizwa ni Tsh 624,347,150/= sawa na asilimia 61% ya makadirio.

PROGRAMU YA USIMAMIZI NA UPANGAJI WA MATUMIZI YA ARDHI

Mhe. Naibu Spika, kufuatia kuundwa kwa Kamisheni ya Ardhi mwaka 2015, jukumu la programu hii limeanza kutekelezwa kupitia chombo hiki kipya chini

ya usimamizi wa Katibu Mtendaji. Chombo hiki ndio chenye dhamana ya Utawala na Usimamizi wa Ardhi hapa nchini. Jukumu la programu hii ni kuhakikisha kunakuwepo na usalama wa matumizi ya ardhi kwa maendeleo ya nchi (*security of tenure*), pamoja na kujenga matarajio ya kuwa na matumizi ya ardhi yaliyo bora na yenye ufanisi. Jukumu hili lilipangiwa kutekelezwa na Idara ya Ardhi, Afisi ya Usajili wa Ardhi, Afisi ya Usajili wa Ardhi, Idara ya Upimaji na Ramani na Idara ya Mipango Miji na Vijiji, ambazo zote hizo zimo ndani ya Sheria ya Muundo wa Kamisheni.

Mbali na taasisi hizo Mahakama ya Ardhi nayo inahusika katika utekelezaji wa programu hii. Utekelezaji wa programu hii umegawanyika katika programu ndogo mbili ambazo ni Utawala wa Ardhi na Upangaji Miji na Matumizi ya Ardhi.

PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA WA ARDHI

Mhe. Spika, Programu hii ndogo inatekelezwa na Idara ya Ardhi na Usajili, Idara ya Upimaji na Ramani pamoja na Afisi ya Msajili wa Ardhi ambapo kwa mwaka wa Fedha 2015/2016 programu hii ndogo iliweza kutekeleza Huduma za Ugawaji na Usimamiaji wa Ardhi, Uthamini wa Ardhi, Usajili wa Ardhi pamoja na utatuzi wa migogoro ya Ardhi kwa kutekeleza shughuli za msingi zinazohusiana nazo.

IDARA YA ARDHI

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Ardhi kwa mwaka wa fedha 2015/16 katika kutekeleza programu ndogo ya Utawala wa Ardhi imetekeleza yafuatayo:

Mhe. Naibu Spika, Kuhusu utayarishaji wa Hati Miliki, jumla ya Hati 362 zilitayarishwa kati ya Hati 650 zilizolengwa kutayarishwa. Hii ni sawa na asilimia 55.69 ya lengo lilowekwa. Kati ya hizo Hati 131 ni za Muda na Hati 231 ni za kudumu. Kuhusu Utayarishaji wa Mikataba ya Ukodishaji Ardhi, jumla ya Mikataba 58 ya Ukodishwaji Ardhi ilitatayarishwa kati ya mikataba 60 iliyopangwa. Hii ni sawa na asilimia 96 ya lengo lilowekwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa shughuli za Uthamini wa Ardhi jumla ya kazi za utiaji thamani 200 kwa mali zisizohamishika zilipangwa kutekelezwa ambapo hadi kufikia Machi Mwaka 2016 kazi 121 zilitekelezwa ikiwa ni asilimia 60.5% ya lengo la mwaka. Kazi hizo ni pamoja na kazi 116 za uthamini kwa ajili ya mirathi, 1 kwa ajili ya uthamini wa fidia, na 4 kwa ajili ya uthamini wa kujua soko la sasa (yaani *market determination*).

Mhe. Naibu Spika, Shughuli ya Utambuzi wa Kumjua Mwenye Haki ya Matumizi Ardhi ni utangulizi wa zoezi la usajili wa ardhi na haikuainishwa katika malengo ya Wizara ya mwaka 2015/16, lakini ilitekelezwa kwa mashirikiano ya bajeti ya washirika wa maendeleo Finland chini ya mradi wa *SMOLE* na pia Mradi wa Urasimishaji Mali na Biashara (MKURABITA) unaotekelezwa kwa pamoja baina ya SMZ na SMT. Jumla ya maeneo 1,207 yalifanyiwa utambuzi kati ya hayo maeneo 300 ni katika Shehia ya Chwaka na maeneo 907 yalifanyiwa katika Shehia ya Jang'ombe.

IDARA YA UPIMAJI NA RAMANI

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Upimaji na Ramani kwa mwaka wa fedha 2015/2016 hadi Machi, 2016, katika kutekeleza programu ndogo ya Utawala wa Ardhi imetekeleza yafuatayo:

Usimamiaji wa Shughuli za Upimaji.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Upimaji na Ramani, Katika mwaka wa fedha 2015/16 imeweza kupima jumla ya viwanja 506, kwa matumizi mbalimbali, kama inavyoonekana katika jaduweli iliyopo chini.

Jaduweli Namba 1 : Maeneo Yaliyopimwa

Nam	Matumizi	Idadi ya Viwanja
1	Makaazi	202
2	Hudma mbalimbali	41
3	Vitega Uchumi	46
4	Taasisi	15
5	Mashamaba ya Kilimo (Watu binafsi)	202
JUMLA		506

Chanzo: Idara ya Upimaji na Ramani

Mhe. Naibu Spika, Idara pia imeweza kuweka Mipaka ya Wilaya ya Unguja na Pemba, kwa kusirikiana Uongozi wa Mikoa na Wilaya husika. Kazi iliyofanywa inakadiriwa kufikia Asilimia 32% ya mipaka yote.

Mhe. Naibu Spika, Aidha, Idara imeanza zoezi la kuzingiza kumbukumbu za Alama za Upimaji (*Control Points*) katika *database* maalumu ili ziweze kupatikana na kutumika kwa urahisi katika kazi mbalimbali za Upimaji na Ukushanyaji taarifa za Kijografia. Kazi hii nayo imeweza kufanikishwa kwa asilimia 20%.

Utayarishaji na utowaji wa Ramani Msingi.

Mhe. Naibu Spika, Idara Katika utayarishaji na utowaji wa Ramani Msingi. Idara imeweza kuchapisha ramani msingi (*Topographical Base Map*)100 za Zanzibar za kipimo cha (1:10,000) na ramani picha (*Othorphotographs*) 31. Aidha, katika kufuatilia taarifa za kupwa na kujaa kwa maji ya bahari, kutoka chombo kilichopo Malindi (*Tide Gaudge*) Idara imeweza kukushanya taarifa za utabiri wa mwaka mzima.

Ukushanyaji na uwekaji wa taarifa za Ardhi

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Upimaji na Ramani kwa kushirikiana na Idara za sekta ya Ardhi zilizopo, ambazo sasa ziko chini ya Kamisheni ya Ardhi, imeimarisha Mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za ardhi (*Zanzibar Land Information System* (*ZALIS*) kwa kiwango cha asilimia 25%. Kwa ushirikishaji wa wadau wengine. Aidha, jitihada za awali zimeanza kuchukuliwa kwa kuwaeleimsha wadau husika wa matumizi ya mfumo huo wa *ZALIS*.

AFISI YA MRAJIS WA ARDHI

Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Mrajis wa Ardhi ni Taasisi yenye jukumu la kusajili ardhi yote ya Zanzibar kwa kuweka taarifa za wamiliki wa haki ya matumizi ya ardhi. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Afisi ya Mrajis imeweza kutekeleza programu ndogo ya Utawala wa Ardhi kwa kutoa huduma ya kusajili ardhi na utowaji wa kadi za usajili, kama ifuatvyo:

Usajili wa Ardhi

Mhe. Naibu Spika, katika kazi za usajili jumla ya maeneo 300 yalisajiliwa kwa upande wa Unguja, baadhi ya Shehia za Wilaya za Mjini na Magharibi ndizo zilizokwisha sajiliwa, ambazo ni Malindi, Kiponda, Shangani, Mkunazini,

Kisiwandui, Kisimamajongoo, Kikwajuni Juu, Kikwajuni Bondeni, Miembeni, Mwembeshauri, Rahaleo, Gulioni, Mwembeladu, Kwahani, Kwaalinatu, Mchangani, Vikokotoni, Mwembetanga na Shehia ya Nungwi na jumla ya maeneo 109 yamesajiliwa kwa shehia ya Mkoroshoni na Limbani za huko Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa huduma ya Utolewaji wa kadi za usajili wa ardhi, hadi Machi Jumla ya Kadi za usajili wa ardhi 410 zimetolewa kwa wananchi ambao ardhi zao zimeshasajiliwa kwa Unguja. Kwa Pemba wananchi 236 wanategemewa kutengenezewa kadi zao kwa kipindi cha miezi mitatu ijayo.

Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Mrajisi katika kufanikisha huduma ya usajili pia imefanikiwa kuanzisha mfumo wa elektroniki katika usajili wa ardhi ambao utafanyakazi kwa karibu na sekta nzima ya Ardhi. Hatua za matayarisho ya kutumia mfumo wa elektroniki katika uhifadhi wa data za usajili wa ardhi zinaendelea. Hadi sasa viwanja 3000 taarifa zake tayari zimeshaingizwa katika mfumo wa elektroniki.

Mhe. Naibu Spika, Katika utowaji wa huduma ya Usajili wa Ardhi, Afisi ya Mrajisi inawajibu wa kufanyakazi kwa karibu na Afisi ya Usajili Wa Ardhi Za Mirathi. Katika mwaka 2015/16 hadi Machi, 2016, Jumla ya nyumba za mirathi 934 kati ya 1415 kwa baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Mjini na Magharibi yameshafunguliwa majalada, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, aidha na maeneo mengine ni Nungwi 266 na Chwaka 62.

Mhe. Naibu Spika, Katika kufanikisha suala zima la Usajili wa Ardhi, Afisi inafahamu umuhimu wa kutoa elimu kwa ngazi tofauti. Katika mwaka tunaomaliza Afisi iliweza kutoa elimu ya usajili kwa wananchi kwa kufanya mikutano mitatu (3) ya kuelimisha wananchi kuhusiana na usajili wa ardhi. Mikutano hiyo imefanyika katika Shehia ya Jang'ombe, Mji Mkongwe na Shehia ya Chwaka. Aidha, mikutano hiyo pia ilitumika kutoa elimu ya mirathi kwa wananchi kwa kushirikiana na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana.

MAHAKAMA YA ARDHI

Mhe. Naibu Spika, Mahakama ya Ardhi inaendelea na kazi zake za kupokea, kusikiliza na kuamua kesi za migogoro ya ardhi zinazowasilishwa na wananchi pamoja na taasisi mbali mbali. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Mahakama ya Ardhi imepokea kesi mpya 168 ambazo zimefunguliwa Unguja na Pemba

pamoja na kesi za awali. Mahakama imeendesha vikao 12,283 vya kusikiliza kesi ambapo kesi 138 zimetolewa hukumu kwa mchanganuo ufuatao:-

Unguja: Kesi mpya 118 zimepokelewa na kesi 96 zimetolewa maamuzi.

Pemba: Kesi mpya 50 zimepokelewa na kesi 40 zimetolewa maamuzi.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Katika kutekeleza programu ndogo ya Utawala wa Ardhi, jumla ya **Tsh 1,011,941,000**/= ziliidhinishwa kutumika. Hadi kufikia Machi, 2016, fedha zilizoingizwa ni **Tsh 728,607,314/=** sawa na asilimia 72% ya makadirio.

PROGRAMU NDOGO YA UPANGAJI WA MIJI NA MATUMIZI YA ARDHI

Mhe. Naibu Spika, Programu hii ndogo inatekelezwa na Idara ya Mipango Miji na Vijiji, ambapo katika kutekeleza programu hii ndogo kwa mwaka wa Fedha 2015/2016, Idara hii ililenga kutowa huduma zifuatazo:

i. Kupanga Matumizi bora ya ardhi kwa miji yote ya Zanzibar,
ii. Kusimamia maendeleo ya ardhi mijini, mikoani na maeneo ya fukwe, na
iii. Kuimarisha miji ili kukuza uchumi na kuleta maisha bora.

Mhe. Naibu Spika, Katika kipindi cha mwaka 2015/2016, Idara kupitia programu hii ndogo imeweza kutekeleza malengo yake kama ifuatavyo:

Kupanga matumizi bora ya Ardhi kwa Miji yote ya Zanzibar

Mhe. Naibu spika, Katika kutekelza lengo hili, Idara imeweza kutekeleza yafuatayo:

i. Kuelimisha jamii kuhusu malengo ya Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Ardhi Zanzibar **(***National Spatial Development Strategy - NSDS).* Jumla ya semina tatu (3), zilizowashirikisha wadau mbali mbali zilifanywa. Serikali ilipitisha rasmi Mkakati wa Maendeleo ya Ardhi Zanzibar (*NSDS*), mnamo tarehe 4 Machi 2015.

ii. Kupanga matumizi ya ardhi ya miji midogo miwili, mmoja Pemba na mmoja Unguja ili kuongeza huduma katika mikoa yote ya Zanzibar na kuhakikisha kuwa wananchi wote wa Zanzibar wanakuwa karibu na

miji midogo na wanapata huduma zao zote katika miji hiyo. Idara ya Mipango Miji na Vijiji tayari imeshapanga mipango midogo (*Local Area Plan)* ya miji mitatu hadi sasa. Miji hiyo ni Chwaka, Mkokotoni na Nungwi.

iii. Idara ya Mipango Miji na vijiji tayari imeshayapanga maeneo matatu ya wazi; Eneo la Kibanda Maiti, eneo la Daraja bovu na eneo la Kiembesamaki. Hivi sasa Idara inafanya jitihada kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Mji *(Urban Development Fund)* kuyajenga maeneo hayo. Lengo la Serikali ni kuhakiksha kuwa katika maeneo yote ya makaazi kuna maeneo ya wazi yenye hadhi kama ile ya bustani ya Forodhani.

Kusimamia Maendeleo ya Ardhi Mijini, Mikoani na maeneo ya Fukwe

Mhe. Naibu Spika, Katika kutekelza lengo hili Idara imeweza kutekeleza yafuatayo:

i. Sambamba na utayarishaji wa *Master Plan*, Idara ilitayarisha Rasimu ya Sheria Mpya ya Mipango Miji, (*Planning and Developement Act*), ili kuchukua nafasi ya sheria kongwe ya Mipango Miji na Vijiji (*Town and Country Act, Cap 85*) ya mwaka 1955.

ii. Kuelimisha jamii juu ya Sera, Sheria na Kanuni Mpya za Mipango Miji kwa kufanya mikutano mitatu juu ya Sera na kuweka kanuni mpya. Mnamo Agosti 2015, kanuni mpya ya usimamizi na udhibiti ujenzi Zanzibar ilipitishwa rasmi (GN 38, 2015). Kanuni hii imeweka mfumo mpya wa utoaji vibali ambao unasimamiwa na taasisi saba, ikiwemo Manispaa, Halmashauri, Wilaya ya Magharibi B, Mamalaka ya Mji Mkongwe, Bodi ya Usajili wa Wahandishi, Wasanifu na wakadiriaji majengo, Jumuiya ya Wafanyabiashara Zanzibar na Idara ya Mipango Miji na Vijiji.

Kuimarisha Miji ili kukuza uchumi na kuleta maisha bora

Mhe. Naibu Spika, Katika kutekelza lengo hili Idara imeweza kutekeleza yafuatayo:

i. Mnamo tarehe 4 Machi 2015, Serikali ilipitisha Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi ya Jiji la Zanzibar (*Zanzibar City Master Plan*). Kwa mujibu wa mpango huu, kitovu cha Mji wa Zanzibar kinahama

kutoka eneo la Mji Mkogwe na kuja eneo la Ng'ambo. Kwa maana nyengine maeneo mapya ya shughuli mbali mbali za kijamii, kibiashara na kiuchumia kama vile maofisi, maduka, sehemu za huduma na sehemu za mapumziko zitaongezwa na kuimarishwa katika eneo la Ng'ambo.

Idara kwa msaada wa Serikali ya Holand, kupitia Manispaa ya Mji wa Amsterdam, ilifanya mpango mdogo (*Local Area Plan*) wa eneo la Ngambo: "Ng'ambo Tuitakayo". Mpango huu umefanywa kwa mashirikiano na taasisi za Serikali, za kiraia na wananchi kwa ujuma. Aidha, idara imefanya mikutano na wakaazi na masheha wa Shehia zote 15 ambazo zimo katika eneo la kitovu cha mji.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Katika kutekeleza programu ndogo ya Upangaji wa Miji na Matumizi ya Ardhi jumla ya **Tsh 270,055,000**/= ziliidhinishwa kutumika. Hadi kufikia Machi, 2016, fedha zilizoingizwa ni **Tsh 226,514,649/=** sawa na asilimia 84 % ya makadirio.

PROGRAMU KUU: UHIFADHI WA MJI MKONGWE, URATIBU NA USIMAMIZI WA UJENZI NA NYUMBA ZA SERIKALI

Mhe. Naibu Spika, Programu hii ilikuwa na jukumu la kusimamia shughuli za ujenzi wa Nyumba na Uhifadhi wa Mji Mkongwe. Programu hii inatekelezwa na Idara ya Ujenzi, Shirika la Nyumba na Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe kupitia programu ndogo mbili, ambazo ni Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Ujenzi na Nyumba za Serikali na Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe.

PROGRAMU NDOGO YA URATIBU NA USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA UJENZI NA NYUMBA ZA SERIKALI.

Mhe. Naibu Spika, Programu hii ndogo inatekelezwa na Idara ya Ujenzi na Shirika la Nyumba, ambapo kiutekelezaji programu hii ndogo kwa mwaka wa Fedha 2015/2016 shughuli zifuatazo zimetekelezwa.

Kuzifanyia matengenezo nyumba za maendeleo Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, Shirika la Nyumba Zanzibar limeweza kusafisha mfumo wa maji machafu ikiwa ni pamoja na kujenga mashimo wa maji machafu Mombasa na kusafisha karo Michenzani na pia kubadilisha mabomba yaliyoharibika. Aidha, Shirika limefanikiwa kuondoa matope yaliokuwa

yakisababisha kujaa kwa makaro na kusambaa kwa maji machafu katika Nyumba za Mchina Mombasa na baadhi ya Nyumba za Michenzani.

Uimarishaji wa Mapato

Mhe. Naibu Spika, Shirika la Nyumba la Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ilipangiwa kukusanya jumla ya **Tsh. 624,000,000/=**. Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2016 Shirika limefanikiwa kukusanya jumla ya **Tsh. 471,650,550/=** sawa na asilimia 76% ya makadirio.

Mhe. Naibu Spika, Kwa upande wa Idara ya Ujenzi, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 imeweza kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuandaa michoro na makadirio ya ujenzi kwa jengo la ZRB Pemba pamoja na jengo la ZECO- Unguja

ii. Kuandaa michoro na kusimamia matengenezo ya jengo la Tume ya Sayansi liliopo Maruhubi.

iii. Kusajili wakandarasi 29 na kufikisha jumla ya 181.

iv. Kusajili miradi 97 ambao imesimamiwa na wataalamu waliosajiwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Katika kutekeleza programu ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Ujenzi na Nyumba za Serikali jumla ya Tsh 757,854,000/= ziliidhinishwa kutumika. Hadi kufikia Machi, 2016, fedha zilizoingizwa ni Tsh 564,614,059/= sawa na asilimia 75 % ya makadirio.

PROGRAMU NDOGO YA UHIFADHI NA UENDELEZAJI WA MJI MKONGWE

Mhe. Naibu Spika, Programu hii ndogo inatekelezwa na Mamlaka ya Uhifandhi na Uendelezaji Mji Mkongwe ambapo kiutekelezaji programu hii ndogo kwa mwaka wa Fedha 2015/2016 kupitia taasisi hii imeweza kutekeleza malengo yaliyokusudiwa kama ifuatavyo:

Utekelezaji wa mpango wa matumizi ya barabara

Mhe. Naibu Spika, Mamlaka imetayarisha na kuwasilisha Serikalini mpango wa matumizi ya barabara zilizomo katika eneo la Mji Mkongwe (eneo la Urithi

wa Kimataifa), kwa madhumuni ya kupunguza msongamano mkubwa ulioukabili mji huu unaoletea athari kubwa kwa majengo ya kihistoria pamoja na viliyomo, unaoushushia hadhi Mji huu kama ni Urithi wa Kimataifa.

Ujenzi wa Ukuta wa Ukingo wa Bahari ya Mizingani
Mhe.Naibu Spika, Kazi ya ujenzi wa ukuta mpya inaendelea vizuri, ambapo kutokea upande wa bustani ya Forodhani mita 30 za ujenzi wa ukuta umekamilika, na kwa kutokea upande wa mkahawa wa *Mercury* kazi ya ujenzi wa msingi (*foundation*) wa ukuta huo imekamilika. Kinachoendelea hivi sasa ni ujenzi wa ukuta ambapo wastani wa asilimia 22 ya kazi ya ujenzi wa ukuta mpya kwa pande zote imekamilika.

Ukarabati wa Jengo la *Chawl* liliopo Darajani

Mhe. Naibu Spika, Jengo la *Chawl* ni miongoni mwa majengo mashuhuri (*Monuments*) yenye daraja la kwanza ndani ya Mji Mkongwe. Mamlaka ilikamilisha utayarishaji wa ramani za awali (*Existing drawings*) na za mapendekezo *(Proposed drawings*) pamoja na makisio ya gharama kwa ajili ya ukarabati wa jengo hilo na baadae kuwasilishwa (*ZSSF*) ambao ndio waliokabidhiwa rasmi jengo hili na Serikali kwa ukarabati na kulirejesha tena kwenye matumizi ambayo yatakuwa na tija zaidi tofauti na hali ya sasa. *ZSSF* wameanza kuchukua hatua za awali kwa kuwatumia washauri elekezi ambao wanahitajika kufuata maelekezo ya kiutalaamu wa kiuhifadhi kutoka Mamlaka ya Mji Mkongwe.

Ukarabati wa Jengo la Beit-el-Ajaib

Mhe. Naibu Spika, Jengo la Beit-el-Ajab ni miongoni mwa majengo mashuhuri yanayotambulikana kimataifa na lenye daraja la kwanza kiuhifadhi. Mamlaka ya Mji Mkongwe imekamilisha utayarishaji wa ramani za awali (*existing drawings*) na za mapendekezo *(proposed drawings*), pamoja na makisio ya gharama kwa ukarabati na ujenzi mpya wa eneo lililoanguka wa jengo la Beit-el-Ajaib na kuwasilisha nchini Oman. Kilichofata ni kuletwa kwa mtaalamu kutoka Oman kwa ajili ya uhakiki wa makisio hayo, utayarishaji wa nyaraka nchini Oman na zabuni (*tender documents*). Kwa kushirikiana na wataalamu wa Mamlaka ya Mji Mkongwe kazi hiyo imemalizika na kuwasilishwa nchini Oman. Mamlaka tayari imepokea barua kutoka Wizara ya Urithi na Utamaduni ya Oman ambayo ndiyo iliyokuwa ikishughulikia suala hili tangu hapo awali na kwamba shughuli za ujenzi wa Beit-el-Ajab zinatarajiwa kuanza rasmi mapema mwezi wa Juni 2016.

Kuweka kumbukumbu za matumizi ya maeneo ya wazi.

Mhe. Naibu Spika, Mamlaka inaendelea na kazi ya kuhakiki na kuweka kumbukumbu za matumizi ya maeneo yote ya wazi yaliyomo ndani ya Mji Mkongwe ambayo baadhi yake hayakuwa na mpangilio mzuri wa matumizi ambayo yanatambulika na Mamlaka. Mamlaka imeandaa mpango wa matumizi ya maeneo hayo ambao unahusisha utoaji wa mikataba kwa watu binafsi kwa matumizi yao mbali mbali ya kijamiii na kibiashara, bila kuathiri uhifadhi na kwamba bado maeneo hayo yatakuwa milki ya Serikali. Jumla ya mikataba 10 imefungwa baina ya Mamlaka na watumiaji binafsi wa maeneo ya wazi kwa kuchangia mapato na uimirashaji wa uhifadhi ndani ya Mji Mkongwe.

Mpango wa Uwekaji wa Posta na Mabango ya Matangazo

Mhe. Naibu Spika, Mamlaka imetayarisha mpango wa uwekaji wa mabango ya matangazo na ubandikaji *"Advertisements and Publications"*(*postas*) kama inavyokubalika kwa miji yenye hadhi Ulimwenguni. Madhumuni ni kuondoa tatizo la kuzagaa kwa mabango ya matangazo ya aina mbali mbali katika kuta za majengo, miti na mapambo ya ndani ya Mji Mkongwe ili kusaidia kuuweka mji wetu katika hali ya usafi ambao hivi sasa kuta nyingi zimechafuliwa kwa ubandikaji ovyo wa mabango ya matangazo hayo.

Takwimu za Idadi ya Mahoteli na Maduka ya Vinyago

Mhe. Naibu Spika, ukaguzi uliofanywa na Mamlaka umegundua kuwepo kwa mahoteli 68 ndani ya Mji Mkongwe na maduka 94 ya biashara za vinyago hususan katika eneo la Shangani. Lengo la takwimu hizi ni kuweka mpango utakaosaidia Mamlaka kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, katika kutekeleza programu ndogo ya Uhifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe jumla ya Tsh 360,047,000/= ziliidhinishwa kutumika. Hadi kufikia Machi, 2016, fedha zilizoingizwa ni Tsh 306,343,500/= sawa na asilimia 85% ya makadirio.

PROGRAMU YA USIMAMIZI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI

Mhe. Naibu Spika, Programu hii inajumuisha Programu Ndogo moja tu ambayo ni Usimamizi, Uendelezaji na Usambazaji wa Huduma za Maji na Nishati na inatekelezwa na Taasisi nne ambazo ni Mamlaka ya Maji (*ZAWA*), Shirika la Umeme (*ZECO*), Mamlaka ya Kudhibiti na Kusimamia Ubora wa Viwango vya Huduma za Maji na Nishati Nchini (*ZURA*) na Idara ya Nishati

na Madini na ina jukumu la kusimamia Uzalishaji na Usambazaji Endelevu wa Huduma za Maji na Nishati.

MAMLAKA YA MAJI

Mhe. Naibu Spika, sekta ya maji inaendelea kutoa mchango mkubwa katika ustawi wa jamii zetu Mijini na Vijijini katika kuimarisha afya za wananchi kwa matumizi ya majumbani, maendeleo ya kiuchumi katika kuendeleza kilimo, utalii, biashara, na kubwa zaidi ni umuhimu wa maji katika utunzaji wa mazingira kwa ajili ya ustawi wa maendeleo ya taifa letu.

Ukusanyaji wa Mapato

Mhe. Naibu Spika, Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa bajeti ya mwaka a fedha 2015/2016 ilipangiwa kukusanya jumla ya TShs bilioni 5.1 kutokana na mauzo ya maji na shughuli nyenginezo. Hadi kufikia Machi 2016, jumla ya TShs bilioni 1.9 zimekusanywa sawa na asilimia 37.3% ya makadirio ya makusanyo yote.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Sekta ya Maji kupitia Mamlaka ya Maji ilifanikiwa kutekeleza Shughuli za Programu na Miradi ya Maji sita ambayo ni Programu ya Usambazaji wa Maji Vijijini, Programu ya Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini, Mradi wa Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji Awamu ya Pili (*JICA PHASE 2*), Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji na Kuijengea Uwezo Mamlaka kifedha (*ADF 12*), Mradi wa Uchimbaji Visima wa Ras al- khaimah pamoja na Kazi za Kawaida zikiwemo Kulinda na Kuhifadhi Vianzio vya Maji na Kufanyia Matengenezo Miundombinu ya Maji.

Mhe. Naibu Spika, kwa kipindi hichi cha mwaka wa fedha 2015/2016 wizara yangu iliendelea kuwapatia maji safi na salama wananchi waishio vijijini kupitia Programu ya Usambazaji Maji Vijijini kwa kujikita zaidi na ukarabati wa miundombinu ya maji kwa ulazaji wa mabomba, ujenzi wa vibanda vya kuendeshea mitambo, ununuzi na ufungaji mita za watumiaji maji, ujenzi wa vituo vya malipo ya maji na huduma kwa wateja pamoja na ujenzi wa matangi katika maeneo mbali mbali ya vijijini Unguja na Pemba kama inavyoonesha katika jadweli lifuatalo:

Jaduweli namba 2. **Utekelezaji wa Programu ya Usambazaji Maji Vijijini**

SN	KAZI ZILIZO TEKELEZWA	MAELEZO YA UTEKELEZAJI	MAENEO HUSIKA
1	Ulazaji wa mabomba	Jumla ya kilomita 17.634 zimefanyiwa kazi ambapo kilomita 10.134 kwa Unguja na 7.5 kwa Pemba kazi hii ni endelevu	Mwanguo, Mvuleni, Makunduchi, Tumbatu na Kinduni kwa Unguja. Kidundo, Mtambwe, Mtuhaliwa, Wambaa, Rui na kilindi kwa Pemba.
2	Uwekaji wa Pampu na Mota mpya	Maeneo husika yamefanyiwa kazi kutokana na na pampu na mota za awali kuungua au kuzidiwa na mahitaji ya watumiaji. Aidha kazi hii ni endelevu	Kizimkazi, Kitogani, Ukongoroni, Kisongoni, Matemwe, Jambiani Kivulini, Bwejuu na Kibele kwa Unguja. Na kwa Pemba ni Mgagadu, Mchanga Mdogo, Shengejuu Ng'ambwa, Konde ,Kironjo A, na Michenzani.
3	Ujenzi wa Vibanda vya kuendeshea pampu	Kazi hii inatarajiwa kuendelezwa katika mwaka wa fedha ujao.	Kinduni, Makunduchi Uwandani, Kibuteni kwa Unguja. Na kwa Pemba ni Shumbavyamboni na Mahuduthi.

4	Ujenzi wa matangi ya kuhifadhia Maji	Kazi imekamilika kiasi kwa hatua za awali kwa upande wa makunduchi na imekamilika kwa maeneo yaliyobakia.	Makunduchi, Mtende, Michamvi, Upenja na Tunguu Mjonga
5	Ujenzi wa ofisi ya afisa wa maji wilaya ya kusini na huduma kwa wateja	Kazi hii inaendelea na inatarajiwa kukamilishwa ndani ya mwaka wa fedha ujao ili kurahisisha upatikanaji wa Huduma kwa Wateja hususan huduma za malipo kwa wananchi wa ukanda wa Kusini ya Unguja	Paje.
6.	Ufungaji wa Mita za watumiaji maji.	jumla ya mita 48 zimefungwa kwa upande wa unguja na mita 118 zimefungwa kwa upande wa pemba kazi hii ni endelevu	Marumbi, Matemwe na Pwani Mchangani kwa Unguja. Mgagadu,Jadida, Kizimbani, Limbani, Kipangani na Kifumbikai kwa Pemba.

Chanzo: Mamlaka ya Maji, Zanzibar

Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji ilifanikisha kazi za Programu ya Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini kwa kuhusisha shughuli tofauti katika maeneo mbali mbali ya Mjini Unguja na Pemba kama inavyojionesha katika jaduweli ifuatayo:

Jaduweli nambari 3 : **Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini**

S/N	KAZI ZILIZOFANYIKA	UTEKELEZAJI HALISI	MAENEO HUSIKA
1.	Ufungaji wa Mita za watumiaji maji	jumla ya mita 211 zimefungwa kwa upande wa unguja na mita 477 zimefungwa kwa upande wa pemba Kazi ya ufungaji mita ni endelevu	Melinne kwa Unguja. Wawi, Tibirizi, Madungu, Uwanja wa Ndege, Limbani, Jadida, Bopwe, Uweleni, Mkoroshoni Bahanasa na kwa Pemba.
2.	Uwekaji wa Pampu na Mota Mpya	Maeneo husika yamefanyiwa kazi kutokana na na pampu na mota za awali kuungua au kuzidiwa na mahitaji ya watumiaji. Aidha kazi hii ni endelevu	Kaburi Kikombe, Kinumoshi N4, Mbweni matrekta, chumbuni,Selemu No 1, Mombosa kwa Mchina kongwe, Masumbani, Magogoni, Welezo, K/Kikombe, Mombasa afisini, na Kwa binti Amrani No 2 kwa Unguja. Na kwa Pemba ni kwa Sharif Ali namba-1,2 na 3, Darajani, Jondeni, Jamvini na Kwa Bi Mtumwa.
3.	Ulazaji wa Mabomba	Jumla ya kilomita 3.103 zimefanyiwa kazi Kazi hii ni Endelevu	Kwerekwe C, Welezo na Masingini kwa Unguja.
4.	Ununuzi wa vidhibiti umeme	Jumla ya vidhibiti umeme 15 vimenunuliwa	Chunga, M/Mchomeke,Kianga na Welezo kwa Unguja. Kwa Pemba ni kironjo Kijuki na Sizini, Mtambwe kaskazini, Kwa sharifuali na Darajani Mkoani.
5.	Upelekaji wa Umeme Vituoni	Kazi imekamilika	Kwerekwe C Unguja
6.	Ujenzi wa Matangi ya Kuhifadhia Maji	Kazi imekamilika	Chumbuni, Dole na Kianga

Chanzo: Mamlaka ya Maji, Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 mbali na shughuli za Programu,wizara yangu imefanikiwa kutekeleza Miradi ya Maji kama ifuatavyo:

Mradi wa Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji (Awamu ya Pili)

Mhe. Naibu Spika, mradi huu unaofadhiliwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la Maendeleo (*JICA*), umeendelea na kazi zinazohusu kuijengea uwezo Mamlaka ya Maji kwa kutekeleza shughuli za mradi huu kama inavyoonekana katika jaduweli ifuatayo:

Jaduweli nambari 4: Utekelezaji **wa Kazi za Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji (Awamu ya Pili)**

SN	Shughuli Mahsusi Zilizotekelezwa	Utekelezaji Halisi
1.	Ununuzi na Ufungaji wa mabomba na viungio vyake katika maeneo ya Gulion hadi Makadara	Jumla ya mabomba yenye ukubwa wa inchi 2½ hadi inchi 16 yamenunuliwa na tayari kilomita 2 zimeshalazwa.
2.	Ukusanyaji na Utunzaji wa taarifa za Mamlaka ya Maji.	Kukusanya taarifa zilizoweza kutambua mivujo ya maji kuanzia mwaka 2013-2015 kupitia (Survace leakage survey) ambapo jumla ya shehia 45 za Mjini na 23 za Magharibi zimeweza kuhifadhiwa katika mfumo wa GIS.
3.	Kupanga na Kutekeleza Shughuli za Kupunguza mivujo ya Maji	kukutana kwa wiki mara moja na kujadili jinsi ya kuandaa michoro (Technical Standards) juu ya uandaaji michoro, ulazaji na matengenezo ya mabomba, kuendelea na ulazaji wa mabomba katika eneo la Gulioni-Makadara na kuanzisha mfumo wa manifold kwa nyumba ishirini zilizofungwa mita ili ziatakazorahisisha ufungaji wa mita na matengenezo.
4.	Kuongeza viwango vya elimu na taaluma kwa wafanyakazi wa Mamlaka ambapo	Jumla ya wafanyakazi 4 wamepatiwa mafunzo nchini Japan
5.	Kuendesha Utafiti na Ukaguzi kwa Wateja kwa baadhi ya maeneo ya Mjini Magharibi ambapo	zoezi hili tayari limekamilika kwa zoni ya Saateni na lipo katika hatua za kumalizia katika zoni ya Mpendae

Chanzo: Mamlaka ya Maji, Zanzibar

Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji na Kuijengea Uwezo Mamlaka Kifedha (*ADF 12*)

Mhe. Naibu Spika, mradi huu umekamilisha kazi ya utiaji saini mikataba ya ujenzi wa mradi kwa wakandarasi kutoka Kampuni ya *NSPT* ya Tanzania kwa kazi ya Ujenzi wa vianzio vya maji na Kampuni ya *SPENCON* kwa kazi ya ujenzi wa miundombinu ya maji, ambapo tayari wakandarasi wote hao wawili wameshakabidhiwa maeneo ya mradi kwa ajili ya kuanza kazi. Kwa upande wa ujenzi wa vyoo maskulini na usafi wa mazingira ambayo ni sehemu mojawapo ya mradi huu, tayari Mshauri elekezi wa Kampuni ya *Howard Humphreys Tanzania Ltd*. ameshakamilisha Ripoti ya Usanifu wa Mradi na kuiwasilisha kwa hatua zinazofuata.

Aidha, kwa upande wa Kazi ya Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji, Mradi umeendesha warsha ya uchambuzi wa zabuni (*Tender Evaluation Workshop)* kwa lengo la kuijenga uwezo kamati ya uchambuzi wa zabuni na tayari taratibu za ununuzi wa mita 6,900 za watumiaji wa maji zinaendelea.

Mradi wa Uchimbaji Visima wa Ras al- Khaimah

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2016, jumla ya visima 136 vimechimbwa kati ya 150, sambamba na ujenzi wa matangi 6 ya kuhifadhia maji, ulazaji wa mabomba na ujenzi wa miundombinu mengine ya maji. Kazi inayoendelea kwa sasa ni ukamilishaji wa visima 14 vilivyobakia.

Mhe.Naibu Spika, kama zilivyo Mamlaka nyengine, Mamlaka ya Maji Zanzibar ina wajibu wa kutekeleza kazi zake za kawaida kupitia vyanzo vyake vya mapato ili kutimiza dhana ya kuwa taasisi inayojitejemea na kujiendesha kibiashara, kwa lengo la kuondokana na utegemezi wa rasilimali, hususan fedha kutoka Serikali Kuu.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Mamlaka imefanikiwa kutekeleza shughuli mbali mbali zinazohusiana na matengenezo ya miundombinu ya maji kama inavyoonekana katika jaduweli ifuatayo:

Jaduweli nambari 5: **Matengenezo ya Miundombinu ya Maji**

S/n	**Kazi zilizotekelezwa**	**Maeneo yaliyohusika**
1.	**Matengenezo ya mabomba**	Migombani, Kianga, Jang'ombe, Mchangani, Bambi, Kihinani, M/Makumbi, Kijangwani, M/Mchomeke, Shaurimoyo, Lumumba, Mpendae, Kijichi, M/Kwerekwe, Nungwi, Matemwe, Welezo, Kwamtipura, Magogoni, Chunga, Mbweni, Meya, Mikunguni, Sogea, Baraza la Wawakilishi, Kilimani, Michenzani, Kilimahewa, M/Ladu, Pangawe, Michungwa Miwili, Kinuni, Migombani Ikulu, Mwanyanya, Kibweni, Kwamchina, Kombawapya, na Daraja bovu, Matemwe, kilimani, Michenzani, Migombani, Meya, Welezo, Melitano, Mkunazini, Elimu Mbadala, Kwarara, Tunguu na Kianga kwa Unguja. Na kwa upande wa Pemba ni Jamvini, Mjini Chake, Mjini Mkoani, Mjini Wete, Kinyikani, Wesha,Vitongoji Kilindi,Kisiwapanza, Mtambile, Shumba Mjini Changaweni, Makangale, Konde, Makongwe, Gando, Junguni, Kojani, Pandani ,Ole.Wambaa na Ukunjwi.
3.	**Marekebisho ya Umeme**	Visima vya Kiashange, Kaburi Kikombe, Mwembe Mchomeke No 51,Kibuteni, Bumbwini, Kidanzini, Kiboje, Bweleo, Manzese, Mgambo, Muyuni, Chunga No 09, Chwaka, Chaani, Dunga S.S.Metha, Chumbuni,Kibele, Bweleo, Msikiti Mzuri No 10, Msikiti Mzuri 12, Kisongoni Nungwi Kae, Matrekta, Mfenesini, Kinumoshi No 3,4,5, Machui, Welezo No 2, Mombasa Ofisini, Umbuji, Kitogani, Kianga No 7 na Salem 1 kwa Unguja. Na Sizini,Kironjo,Kijichame,Makangale,Gawani,Bunguni, Kibomani, Penjewani,Ziwani,Ngambwa,Kwapweza, Kwa Sharifuali, Chanjaani, Changaweni, Mtambile, Ngombeni, Ngwachani, Mjimbini kwa upande wa Pemba.
4.	**Matengenezo ya pampu na mota zilizoungua**	Visima vya Bweleo, Machui, KaburiKikombe, Bumbwini Kidanzini, Mombasa Afisini, Kieshange No 4 Kitogani, Mwanyanya, Jendele, Maungani na usafishaji wa visima (Flushing) imefanyika katika maeneo ya MigombaniPangeni, K/Kikombe,Welezo na Saateni workshop kwa Unguja. Na Pemba ni Visima vya Mfikiwa, Ukutini, Makangale,Changaweni Chake Chake, Mjimbini, Sharifuali no-3 na Wingwi Mlindo. FlUshing Kwa Pemba imefanyika Visima vya Ng'ambwa, Mauleni, Ng'wachani, Bogoa, Kijichame,Mfikiwa, Ole skuli, Mazurui, Kwamkoba, na kinowe.

Chanzo: Mamlaka ya Maji, Zanzibar

IDARA YA NISHATI NA MADINI

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Nishati na Madini ni taasisi inayohusika na Usimamizi na Usambazaji wa Huduma ya Nishati hapa nchini kwa lengo la

Kuimarisha Upatikanaji na Usambazaji wa Nishati yenye ufanisi, kwa bei nafuu na inayozingatia uendelevu wa mazingira yaliyo salama na rafiki kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii, ambapo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 idara hii ilisimamia na kutekeleza mambo yafuatayo:-

Mradi wa Utekelezaji wa Sera ya Nishati

Mhe. Naibu Spika, mradi huu unatekelezwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Washirika wa Maendeleo na unahusika zaidi katika maeneo makubwa mawili, ambayo ni Kuijenga uwezo Sekta ya Nishati - Awamu ya Pili *(Zanzibar Energy Sector Support Consolidated Phase)* kwa mashirikiano na Shirika la Maendeleo la Sweden *(SIDA)* na eneo kuu la pili ni Kuimarisha Mazingira pamoja na Kupambana na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi, ambapo baada ya kukamilika kwa maeneo haya mawili, bila shaka Sekta ya Nishati kwa Zanzibar itakuwa imeimarika na kuongeza ufanisi kiutekelezaji ambayo ni hatua muhimu sana kwa mustakbali wa uchumi wetu na sekta zote kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, katika utekelezaji wa mradi wa Kuijenga uwezo Sekta ya Nishati - Awamu ya Pili, idara kwa kushirikiana na Ubalozi wa Sweeden tayazi imetiliana saini na Kampuni ya *Multy Consultant ASA* ya nchini Norway ambayo ilishinda zabuni ya ushauri elekezi kwa mradi huu unaotarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka huu wa fedha.
Aidha, idara kwa kushirikiana na iliyokuwa Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais chini ya mradi wa mabadiliko ya tabia nchi kwa ufadhili wa *UNDAP* imetekeleza yafuatayo:-

i. Jumla ya mifumo (38) ya umeme wa jua *(Solar Units)* imewekwa katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba;

ii. Ziara za ukaguzi katika maeneo yaliyofungwa mifumo hiyo kwa kutathmini ufanisi zimefanyika;

iii. Hati ya muongozo *(guidelines document)* imeandaliwa sambamba na kuendesha semina ya kushajihisha matumizi ya miongozo hiyo;

iv. Kuandaa Mpango Kazi wa utekelezaji wa Sera ya Nishati;

v. Kuandaa Kanuni za kupiga marufuku matumizi ya taa zenye kutumia umeme mwingi *(incandescent bulbs);* na

vi. Kufunga taa sanifu *(energy saving bulbs)* katika maeneo maalum ya majaribio *(pilot areas)* ambayo ni Fumba na Mwakaje.

Mradi wa Utafiti wa Nishati Mbadala

Mhe. Naibu Spika, serikali inaendelea na azma yake ya kukamilisha Mradi huu wa Nishati Mbadala unaofadhiliwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Jumuiya ya Nchi za Ulaya *(EU)* wenye lengo la kufanya utafiti ili kubaini uwezekano wa Zanzibar kupata umeme kwa njia mbadala.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/206, wizara imesimamia zoezi la usafishaji maeneo pamoja na ujenzi wa minara mitano yenye urefu wa mita sabiini na moja (71 m) pamoja na kufunga vifaa vya kurikodia (*sensors*) kwa lengo la kukusanya taarifa za mwenendo wa upepo na nguvu za jua. Ujenzi huo umetekelezwa chini ya Kampuni ya *AGMIN* kutoka Italy. Vile vile, wizara imekamilisha kupatikana kwa mkandarasi (Kampuni ya *MWH* ya Spain) ambae atashughulikia masuala ya kisheria pamoja na kuzijengea uwezo taasisi zinazoshughulikia miradi ya Nishati Mbadala. Aidha, Mshauri elekezi (Kampuni ya *Intec Gopa* ya Ujerumani) anaendelea na kazi na ukusanyaji wa tarifa hizo (*data collection*) na tayari ameshatoa ripoti yake awali ya miezi mitatu (Oktoba-Disemba, 2015) inayoonesha mwelekeo mzuri wa mwenendo wa upepo na upatikanaji wa nguvu za jua.

Mhe. Naibu Spika, mbali na shughuli za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Idara ya Nishati na Madini imefanikiwa kutekeleza Kazi za Kawaida kama ifuatavyo:-

Kushiriki katika Mikutano ya Masuala yanayohusu Nishati ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa pamoja na Kuendelea Kusimamia Upatikanaji wa Mafuta Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza hili, idara imefanikiwa kushiriki mikutano kadhaa iliyofanyika ndani na nje ya nchi ikiwemo vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki katika masuala ya nishati ya umeme (Dar-es-Salaam - Tanzania na Kigali - Rwanda). Ni dhahir kuwa fursa hii inaongeza uzoefu na utaalamu kwa wafanyakazi wa idara hii.

Aidha, katika kuhakikisha nishati ya mafuta inapatikana kwa uhakika, idara inaendelea kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Mani na Nishati (*ZURA*) ili kutambua mwenendo wa biashara ya mafuta pamoja na kuandaa utaratibu mzuri wa uagizishaji na uingizaji wa mafuta hapa nchini.

Kuendeleza Mashirikiano na Wadau wa Maendeleo katika Kuendesha Mafunzo yanayohusiana na Suala la Mafuta na Gesi Asilia pamoja na Kujenga Uelewa kwa Wananchi juu ya Masuala ya Nishati.

Mhe. Naibu Spika, katika jitihada za kuendeleza mashirikiano na wadau mbali mbali wa maendeleo wa ndani na nje, idara imefanikiwa kuendesha semina tatu zinazohusiana na masuala ya mafuta na gesi asilia ambazo zimewashirikisha wafanyakazi wa Idara ya Nishati na Madini ikiwa ni sehemu ya kuwajengea uwezo kitaaluma.

SHIRIKA LA UMEME

Mhe. Naibu Spika, Shirika la Umeme ni taasisi inayohusika na Usimamizi na Usambazaji wa Huduma ya Nishati ya Umeme hapa nchini kwa lengo la kuimarisha upatikanaji na usambazaji wa nishati hiyo kwa ufanisi, yenye uhakika na kwa bei nafuu kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa programu ya usimamizi wa huduma za maji na nishati. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, taasisi hii ilisimamia na kutekeleza kazi ya Usambazaji na Uimarishaji wa Miundo Mbinu ya Umeme Mjini na Vijijini.

Mapato na Matumizi

Mhe. Naibu Spika, kimsingi shirika hili kama ilivyo kwa mashirika mengine ya umma hapa nchini sio tu yana wajibu wa kuhakikisha upatikanaji wa huduma zenye ubora unaokubalika kitaifa na kimataifa na kwa gharama nafuu kwa lengo la kuimarisha ustawi wa jamii yetu kiuchumi, kijamii na kimazingira bali pia kuliwezesha shirika kujiendesha kibiashara na hatimaye kuweza kuchangia katika mfuko mkuu wa serikali.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, shirika lilikadiria kukusanya Tsh. 107,063,020,514/= kutokana na biashara ya kuuza umeme na huduma nyenginezo zinazotolewa kwa wananchi na wafanyabiashara, ikiwemo wawekezaji mbali mbali hapa nchini. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016 shirika limekusanya jumla ya Tsh. 63,277,985,396/= sawa na asilimia 59.1% ya makadirio.

Kwa upande wa matumizi, shirika lilikadiria kutumia jumla ya Tsh. 99,838,743,939/=. Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2016, shirika lilikwishatumia Tsh. 67,980,810,349/= sawa na asilimia 68.1% ya makadirio kama inavyoonekana katika jaduweli lifuatalo.

Jaduweli nambari 6: **Matumizi ya Shirika la Umeme kwa mwaka wa fedha 2015/2016**

MAELEZO	**MAKADIRIO YA MWAKA 2015-2016**	**MATUMIZI HALISI Julai,2015 hadi Machi, 2016.**
Ununuzi wa Umeme TANESCO	58,456,165,441.00	46,281,896,474.96
Kazi ya kawaida	26,378,880,650.00	11,699,728,964.07
Kazi ya maendeleo	15,003,697,848.00	9,999,184,910.39
Jumla	**99,838,743,939.00**	**67,980,810,349.42**

Chanzo: Shirika la Umeme, Zanzibar

Mhe. Naibu Spika, kwa kipindi hichi cha mwaka wa fedha 2015/2016, wizara yangu kupitia Shirika la Umeme iliendelea kuwapatia huduma za umeme wananchi waishio mijini na vijijini kupitia Programu na Miradi ya Umeme nchini kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na Washirika mbali mbali wa Maendeleo waliopo ndani na nje ya nchi kwa kujikita zaidi na ukarabati wa miundombinu ya umeme na usambazaji wa umeme Vijijini Unguja na Pemba.

Usambazaji wa Umeme Vijijini

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016, shirika limejenga kilomita 33.1 ya umeme mkubwa na kilomita 83.9 za laini ndogo ya umeme pamoja na uwekaji wa *Transfomers* 35 za kusambaza umeme katika vijiji 36 kwa Unguja na Pemba, kama inavyoonekana katika jaduweli ifuatayo:-

Jadueli nambari 7: **Vijiji Vilivyopatiwa Umeme**

UNGUJA	**PEMBA**
Binguni Mtakuja	Chupwe Micheweni
Bungi Usalama	Gongomawe
Cheju Kisomanga	Kisiwa cha Makoongwe
Donge Kiongwe Kidogo	Kisiwa cha Shamiani Muambe
Hanyegwa Mchana	Kisiwa Panza
Kandwi	Kiziwani Shungi
Kijini	Konde Mipurani
Matetema	Mazoweya Pujini
Maungani Kichakapunda	Mgeni nje Shumba vyamboni
Mbuyu Tende	Michungwani
Mgambo	Mitungujani
Ndijani Nyambiza	Mjananza Wingwi
Tunguu	Mjimbini Kangani
Ubago Wilayani.	Mtimbu Pujini
Upenja Kaskazini	Muambe kwasaanani
Uzi Pwani	Mwachawa
	Pujini Kibaridini
	Sebudawa Micheweni
	Shengejuu Mtambwe
	Wawi Magome

Chanzo: Shirika la Umeme, Zanzibar

Uimarishaji wa Miundombinu ya Umeme.

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha miezi 9, Shirika limebadilisha waya chakavu kilomita 37.9, nguzo mbovu 1,319 na kupima *transfomer* 576 kwenye maeneo ya Mijini na Vijijini pamoja na kuzifanyia marekebisho zile zilizokuwa na matatizo ili kuhakikisha kwamba hali ya upatikanaji wa huduma bora ya umeme inapatikana kwa uhakika na kwa wakati wote.

Ufungaji wa Mita za TUKUZA:

Mhe. Naibu Spika, lengo la mradi huu ni kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya shirika na kupunguza malimbikizo ya madeni. Hadi kufikia Machi, 2016, Shirika limenunua mita 13,000 za TUKUZA kwa gharama ya Tsh.1,423,500,000/=. Kati ya hizo, Mita 6,645 zimefungwa kwa wateja wapya na Mita 6,355 zimebadilishwa kwa wateja wa zamani wenye mita za kawaida na mbovu.

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI

Mhe. Naibu Spika, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati ni taasisi yenye jukumu la kusimamia huduma za maji na nishati nchini. Mamlaka inalenga kutekeleza lengo kuu la programu ya Usimamizi wa Huduma za Maji na Nishati ambalo ni kufikia Usimamizi Endelevu na Usambazaji Toshelezi wa Huduma za Maji na Nishati kwa jamii.

Mhe. Naibu Spika, kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016, Mamlaka ya Udhibiti ya Huduma za Maji na Nishati imefanikiwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

Kuandaa Kanuni za Usimamiaji wa Sekta ya Mafuta kuanzia Uagiziaji, Upakuaji, Uhifadhi, Usambazaji, Uuzaji na Ujenzi wa Vituo vya Mafuta

Mhe. Naibu Spika, mamlaka katika kujenga mazingira bora ya kusimamia biashara ya mafuta nchini, imeandaa Kanuni za Kusimamia Biashara ya Mafuta (*Petroleum Supply Regulations,2015*) na Kanuni za Kusimamia Ujenzi wa Vituo vya Mafuta ili kuweka mazingira ya vituo hivyo kuwa katika viwango vinavyokubalika.

Kuanza Shughuli za Utoaji wa Leseni

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza hili, Mamlaka imeanza kufanya ukaguzi wa vituo vyote vya mafuta kwa upande wa Unguja ili kujiridhisha juu ya

viwango na ubora wa vituo hivyo. Hadi Machi, 2016 Mamlaka imekagua vituo 30 kati ya vituo vyote 50 vilivyopo Zanzibar na kutoa maelekezo ya kufanya matengenezo na marekebisho kwa vituo ambavyo havikidhi viwango kabla ya kuwapa leseni.

Kuanza Kupanga Bei za Mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa

Mhe. Naibu Spika, Mamlaka ilikabidhiwa rasmi jukumu la kupanga bei elekezi na Bodi ya Mapato ya Zanzibar mapema mwezi Disemba, 2015. Kuanzia mwezi Februari, 2016 Mamlaka imeanza kazi ya kupanga na kutoa bei elekezi kwa bidhaa zote za mafuta hapa nchini ambapo zoezi hili linafanyika kila mwezi.

Kujenga Uelewa Juu ya Majukumu na Kazi za Mamlaka kwa Wadau na Jamii kwa Ujumla

Mhe. Naibu Spika, kwa vile mamlaka hii ni mpya, ni wazi kuwa wananchi wanahitaji kuijua na kuielewa vizuri, hivyo, mamlaka imekuwa ikifanya mikutano na makampuni yanayoleta mafuta Zanzibar (*Oil Marketing Companies*), wamiliki wa vituo vya mafuta na wataalamu kutoka katika taasisi mbali mbali za serikali na zisizo za serikali kwa lengo la kuwaelimisha kuhusu majukumu na kanuni zinazosimamiwa na *ZURA*. Jumla ya semina Tano (5) zimefanyika; Tatu (3) Unguja na Mbili (2) Pemba. Vile vile, Mamlaka imeanza kutoa vipindi vya kuelimisha jamii kwa njia ya televisheni na redio.

Ushirikiano na Taasisi za Kikanda Zinazohusiana na Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

Mhe. Naibu Spika, katika utekelezaji wa suala hili, mamlaka imekuwa ikishirikiana kwa karibu na Taasisi za Tanzania Bara kama vile Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (*EWURA*), Taasisi inayosimamia Uhifadhi wa Mafuta (*TIPER*), Wakala wa Uagizaji wa Mafuta ya jumla Tanzania (*PBPA*), Kampuni inayoweka alama katika mafuta (*GFI*). Vile vile Mamlaka imejenga uhusiano mzuri na Taasisi inayohifadhi mafuta ya Mombasa Kenya, *Kenya Pipe Line Company.*

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Katika kutekeleza program ya Usimamizi wa Huduma za Nishati na Maji jumla ya Tsh 31,565,198,587/= ziliidhinishwa kutumika. Hadi kufikia Machi, 2016, fedha zilizoingizwa ni Tsh 6,030,458,943 /= sawa na asilimia 19% ya makadirio**.**

PROGRAMU KUU: USIMAMIZI WA MAZINGIRA/MABADILIKO YA TABIA NCHI

Mhe. Naibu Spika, Itakumbukwa kwamba kufuatia uchaguzi mkuu uliofanyika tarehe 20 Machi, 2016 Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imefanya mabadiliko ya miundo ya Mawizara zake iliyopelekea kuundwa kwa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, hivyo programu hii ya usimamizi wa Mazingira na mabadiliko ya tabianchi hapo awali ilikua chini ya usimamizi wa Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais na hivi sasa inasimamiwa na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mhe. Naibu Spika, Kama tunavyofahamu kwamba suala la mazingira linachukua nafasi kubwa na ya pekee wakati wa kujadili suala la Mabadiliko ya Tabianchi. Kwa mantiki hiyo ni kweli kwamba suala la mazingira linapaswa kupewa kipaumbele wakati wa kujadili dhana nzima ya Mabadiliko ya Tabianchi huku tukilenga kuyafikia maendeleo endelevu ya kiuchumi, kiteknolojia na kijamii bila ya kuathiri mazingira yaliyotuzunguka katika maisha yetu ya kila siku.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Mazingira na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira (*ZEMA*) kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kupitia programu ndogo mbili ambazo ni Usimamizi wa Mazingira na Usimamizi wa Mabadiliko ya tabianchi kwa pamoja zilipanga na kutekeleza majukumu kama ifuatavyo:

Programu ndogo ya Usimamizi wa Mazingira
Mhe. Naibu Spika, Programu hii ndogo inatekelezwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira na Idara ya Mazingira ambapo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 imefanikiwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

Kutayarisha Kanuni za Usimamizi wa Mazingira.
Mhe. Naibu Spika, **r**asimu za awali za mapitio ya Kanuni ya Tathmini ya Athari za Kimazingira ya mwaka 2002 na Kanuni ya Marufuku ya Mifuko ya Plastiki ya mwaka 2011 zimetayarishwa kwa kuondosha mapungufu yaliyokuwepo na kuingiza hoja muhimu za wadau.

Kuendesha Operesheni 84 za mifuko ya plastiki na pia 84 kwa maliasili zisizorejesheka.
Mhe. Naibu Spika, jumla ya operesheni 16 za mifuko ya plastiki zimefanyika kwa Unguja na Pemba ambapo zaidi ya kesi 17 zimefikishwa mahakama husika na kutolewa hukumu.

Kufanya ufuatiliaji wa kimazingira kwenye maeneo 84 yaliyoharibiwa kimazingira.
Mhe. Naibu Spika, jumla ya maeneo 35 yenye uharibifu na uchafuzi wa mazingira yametembelewa na kutolewa muongozo wa kimazingira na kisheria. Kati ya maeneo hayo 23 yapo Unguja na 12 yapo Pemba. Kwa ufafanuzi zaidi angalia Kiambatanisho E ya taarifa hii**.**

Kufanya shughuli za Ufuatiliaji, Tathmini na Ukaguzi wa kimazingira kwa miradi ya Uwekezaji iliopo hapa nchini.
Mhe. Naibu Spika, jumla ya miradi 45 imefanyiwa ufuatiliaji na kutolewa muongozo wa kimazingira na kisheria. Kati ya miradi hiyo 30 Unguja na 15 Pemba. Miongozo hiyo ilikuwa inahusisha usimamizi wa taka na maji machafu hasa kutoka kwenye mabwawa ya kuogelea. Vilevile jumla ya miradi 25 imefanyiwa Tathmini za Kimazingira na kupewa vyeti vya kimazingira. Aidha jumla ya miradi 18 imefanyiwa ukaguzi wa kimazingira na kupewa vyeti vya ukaguzi huo. Kwa ufafanuzi zaidi angalia Viambatanisho F na G.

Kuelimisha jamii juu ya Sheria ya Mazingira kupitia vipindi vya Radio, TV na mikutano ya uhamasishaji.

Mhe. Naibu Spika, jumla ya vipindi 25 (18 Radio na 7 TV) vya kuelimisha jamii juu ya usimamizi wa mazingira vimetayarishwa na kurushwa kupitia *ZBC* Radio, *ZBC TV*, *Coconut*, *Hits FM Chuchu FM*. Aidha, *ZEMA* na Idara ya Mazingira zilitembelea wizara zote pamoja na Ofisi za Mikoa kuonana na watendaji wakuu wa taasisi hizo pamoja na taasisi zilizo chini ya Wizara hizo kwa lengo la kuelimisha wadau juu ya Sheria ya Mazingira ya mwaka 2015.

Mhe. Naibu Spika, , kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Katika kutekeleza programu zake, Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira na Idara ya Mazingira ziliidhinishiwa kutumia Tsh 255,000,000/=. Hadi kufikia Machi, 2016 taasisi hizi zilikwisha ingiziwa Tsh 38,375,000/= sawa na asilimia 15%.

Programu ndogo ya Mabadiliko ya Tabia nchi

Mhe. Naibu Spika, Programu hii ndogo inatekelezwa na Idara ya Mazingira, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kupitia Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka, Wizara Fedha na Mipango kupitia Idara ya Fedha za Nje, Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kupitia Idara ya Nishati na Madini na Jumuiya ya Maendeleo ya Jamii na Uhifadhi wa Mazingira Zanzibar *Community Development and Environmental Conservation in Zanzibar.*

Mhe. Naibu Spika, Mpango kazi wa utekelezaji wa Mkakati wa Mabadiliko ya Tabianchi umetayarishwa kutokana na vipaumbele vilivyoainishwa kwenye Mkakati wa Mabadiliko ya Tabianchi wa Zanzibar wa mwaka 2014. Mpango kazi huo unategemewa kuzinduliwa rasmi mwezi wa Juni, 2016 kwa ajili ya utekelezaji.

Mhe. Naibu Spika, Mpango wa Kijamii wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi *Local Adaptation Plan of Action - LAPA* kwa Wilaya 3 Micheweni, Kaskazini "A" na Kusini Unguja umetayarishwa. Mpango huu unakusudiwa kutumika katika kuhamasisha nyezo za utekelezaji za Mpango huo na hatimae kutayarisha mipango ya Wilaya nyengine zilizobakia hatua kwa hatua kutegemea na upatikaaji wa fedha. Aidha, katika suala la kuendelezwa baadhi ya maeneo yaliyoathiriwa na mabadiliko ya tabianchi, jumla ya hekta 100 za mikoko na mikandaa imepandwa kwenye maeneo 17 ya Unguja (10) na Pemba (7) kwa ajili ya kuendeleza maeneo yaliyoharibiwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Katika kutekeleza programu ndogo ya Mabadiliko ya Tabianchi, jumla ya Tsh 450,000,000/= ziliidhinishwa kutumika. Hadi kufikia Machi, 2016, fedha zilizoingizwa ni Tsh 459,345,000/= sawa na asilimia 100%.

MUELEKEO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima naomba kuwasilisha muelekeo wa Bajeti yenye kuzingatia programu ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ina jumla ya Programu Kuu nne ambazo ni;

a. Programu 1: Mipango, Sera na Utawala wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira;
b. Programu 2: Usimamizi na Upangaji wa Matumizi ya Ardhi;
c. Programu 5: Usimamizi wa Huduma za Maji na Nishati;
d. Programu 6: Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi.

Mhe. Naibu Spika, jumla ya Tsh Bilioni 57,456,186,000 zinatarajiwa kutumika katika utekelezaji wa Programu hizi nne.

Mhe. Naibu Spika, Naomba sasa uniruhusu kutoa maelezo kwa ufupi kuhusu Programu na Programu ndogo zinazohusiana na Wizara yangu kama ifuatavyo.

PROGRAMU YA MIPANGO, SERA NA UTAWALA WA ARDHI, MAJI, NISHATI NA MAZINGIRA

Mhe. Naibu Spika, programu hii ina jukumu la kuimarisha uratibu katika utekelezaji wa Kazi za Wizara ambapo matokeo ya muda mrefu yanayotarajiwa ni Kukuza ufanisi katika utawala wa rasilimali ardhi pamoja na utoaji huduma za kijamii. Programu itasimamiwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na Afisi Kuu Pemba ambapo jumla ya Tsh. 2,342,446,000/= zinatarajiwa kutumika kwa utekelezaji wake. Programu hii imegawanyika katika Programu ndogo.

Mipango na Sera za Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/Mabadiliko ya Tabianchi

Mhe. Naibu Spika, dhumuni la Programu ndogo hii ni Uratibu wa Shughuli na Kazi za Wizara kwa Ufanisi, ambapo matokeo ya muda mfupi *output* yanayotarajiwa katika utekelezaji wa Programu hii ni Kuratibu/Kuandaa Mipango na Miongozo ya Kisera ya Utekelezaji wa Kazi za Wizara, Kuratibu, Kufuatilia na Kutathmini Utekelezaji wa Programu, Miradi na shughuli za Wizara na Kuandaa Tafiti kwa ajili ya Kuendeleza ufanisi katika utoaji wa huduma katika sekta za Wizara. Jumla ya Tsh 173,067,000/= zinatarajiwa kutumika.

Utawala na Maendeleo ya Rasilimali watu

Mhe. Naibu Spika, dhumuni la programu ndogo hii ni kuhakikisha usimamizi thabiti na utawala wa rasilimali za Wizara, ambapo matokeo ya muda mfupi *output* yanayotarajiwa katika utekelezaji wa programu hii imepanga kukuza Viwango vya Wafanyakazi kwa kuwapatia fursa mbali mbali za kielimu, kusimamia shughuli za uendeshaji wa ofisi na kuhifadhi kumbukumbu na Taarifa za Wafanyakazi. Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekelezeka jamuku wake kwa mwaka 2016/17 naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tsh 808,112,000.

Uratibu wa Shughuli za Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, Pemba

Mhe. Naibu Spika, dhumuni la programu ndogo hii ni Uratibu na Usimamizi Thabiti wa Kazi za Wizara kwa pemba, ambapo matokeo ya muda mfupi *output* yanayotarajiwa katika utekelezaji wa programu hii ni Kuratibu Shughuli za Mipango na Utawala pamoja na Kuratibu na Kusimamia masuala ya Ardhi, Makaazi maji na Nishati Pemba. Jumla ya Tsh 1,361,267,000/= zinatarajiwa kutumika.

PROGRAMU YA USIMAMIZI NA UPANGAJI WA MATUMIZI YA ARDHI

Mhe. Naibu Spika, programu hii inajukumu la kuhakikisha kunakuwepo na usalama wa matumizi ya ardhi kwa maendeleo ya nchi *security of land tenure*. Matokeo ya muda mrefu yanayotarijiwa ni kuwa na matumizi ya ardhi yaliyobora na fanisi. Programu hii inasimamiwa na Kamisheni ya Ardhi na Mahakama ya Ardhi ambapo jumla ya Tsh. 2,275,072,000/= zinatarajiwa kutumika.

Mhe. Naibu Spika, programu hii imegawanyika katika Programu ndogo ndogo kama ifuatavyo:

Utawala wa Ardhi

Mhe. Naibu Spika, Dhumuni la Programu ndogo hii ni kuhakikisha Usalama wa Umiliki wa Ardhi kwa Wananchi ambapo matokeo ya muda mfupi *output* yanayotarajiwa katika utekelezaji wa Programu hii ni ugawaji na usimamiaji wa ardhi kwa matumizi mbali mbali, Uthamini wa ardhi na Usimamiaji wa shughuli za Upimaji na Ramani, Usajili wa ardhi. Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/17 Kamisheni ya Ardhi kupitia programu ndogo wa utawala wa ardhi imepanga kutekeleza kazi ifuatazo:-

Kutayarisha Hati Miliki 1350 na vitambulisho vya umiliki wa ardhi za eka tatu 90;
Kutayarisha Mikataba ya ukodishaji ardhi 130;
Kuingiza taarifa za ardhi katika mfumo wa Kompyuta sawa na hati na mikataba itakayotaarishwa;
Kukagua maeneo yote yatakayohitajika kutayarishiwa mikataba ya uwekezaji wa maeneo ya kilimo ya eka tatu;
Kufanya kazi za uthamini 300 zikiwemo kazi 200 za uthamini wa miradhi 50 za fidia na 50 za kutambua soko la sasa;
Kuimarisha na kusimamia shughuli za upimaji ardhi na utayarishaji ramani kwa matumizi mbali mbali nchini;
Kuendeleza na kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa taarifa zinazohusiana na ardhi ambao utawanufaisha wadau mbali mbali ndani na nje ya sekta za ardhi;

Upangaji wa Miji na Matumizi ya Ardhi

Mhe. Naibu Spika, dhumuni la programu ndogo hii ni Kuhakiksha Kunakuwepo Uwiano wa matumizi ya Ardhi kati ya Matumizi ya Uchumi na Kijamii, ambapo matokeo ya muda mfupi *output* yanayotarajiwa katika

utekelezaji wa programu hii ni kuwepo kwa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi kwa Miji yote ya Zanzibar, Kusimamia Maendeleo ya Ardhi Mijini, Mikoani na maeneo ya Fukwe, Kuimarika kwa Miji ili Kukuza Uchumi na Kuleta Maisha Bora. Jumla ya Tsh 1,021,398,000/= zinatarajiwa kutumika.

Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi

Mhe. Naibu Spika, Dhumuni la Programu ndogo hii ni kuhakikisha kwamba kunakuwepo na utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa haraka zaidi kadri ya inavyojitokeza, ambapo matokeo ya muda mfupi *output* yanayotarajiwa katika utekelezaji programu hii ndogo ni pamoja na kupungua kwa migogoro ya Ardhi. Jumla ya Tsh 188,214,000/= zinatarajiwa kutumika.

PROGRAMU YA USIMAMIZI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI

Mhe. Naibu Spika, jukumu la programu hii ni kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2016/17 naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla Tsh. Jumla ya Tsh 1,065,460,000.

Mhe. Naibu Spika, Programu hii itasimamiwa na Idara ya Nishati na Madini, Mamlaka ya Kudhibiti Huduma za Maji na Nishati, Shirika la Umeme na Mamlaka ya Maji ambapo jumla ya Tsh. 48,978,195,000/= zinatarajiwa kutumika katika utekelezaji wake.

Mhe. Naibu Spika, matokeo ya muda mfupi *output* yanayotarajiwa katika utekelezaji wa programu hii ni usimamizi wa usambazaji wa mafuta nchini, usambazaji wa huduma za Umeme, uhifadhi wa maeneo ya vianzio vya maji, upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa watumiaji mijini na vijijini.

Mhe. Naibu Spika, kupitia Baraza lako hili tukufu ninaomba Waheshimiwa Wawakilishi kuwa karibu na wananchi katika kulinda, kuhifadhi, kuenzi na kutunza miundo mbinu na vianzio vya maji pamoja na kuitikia wito wa uchangiaji wa huduma ili kuiwezesha mamlaka kutoa huduma endelevu.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii ya usimamizi wa huduma za Maji na Nishati, kutelekeza majukumu yake kwa mwaka 2016/2017 naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya milioni arubaini na nane, milioni mia tisa sabini na nane laki moja sitini na tano elfu.

PROGRAMU YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA NA MABADILIKO YA TABIA NCHI

Mhe. Naibu Spika, programu hii itatekelezwa kupitia programu ndogo ya Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi na utekelezaji wake utaimarisha usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabia nchi. Programu hii inasimamiwa na Idara ya Mazingira na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira.

Mhe. Naibu Spika, dhumuni la programu hii ni kuhakikisha usimamizi endelevu wa masuala ya kimazingira, ambapo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 programu hii imepanga kutayarisha kanuni za mazingira, kuandaa ziara za ufuatiliaji na ukaguzi wa kimazingira, kufanya tathmini za kimazingira, kufanya operesheni za mifuko ya plastiki pamoja na maliasili zisizorejesheka na kuendeleza maeneo yaliyoathirika na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wa programu hii ndogo ya usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabia ya nchi utahitaji mashirikiano makubwa kutoka kwa wadau mbali mbali kwa upande wa mabadiliko ya tabia ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii ya usimamizi wa huduma za maji na nishati kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2016/2017, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla T.Shs.3,860,473,000/-.

HITIMISHO

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa sana naomba kuchukua nafasi hii kwa mara nyingine tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa ya kuwatumikia Wananchi wenzangu kupitia Wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Wizara na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, naomba kuchukua nafasi hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa Nchi marafiki, Mashirika ya Kimataifa na yasiyo ya Kimataifa, Sekta binafsi, *NGOs*, *CBOs* na wananchi kwa jumla kwa mashirikiano makubwa waliyoyaonesha kwa Wizara yangu kwa misaada yao ya hali na mali waliyoitoa na wanayoendelea kutoa kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara hii. Washirika hao ni JAPAN, NORWAY, SWEDEN, CHINA, OMAN, FINLAND, HOLLAND, UNITED KINGDOM, INDIA, *UNICEF*, *UNESCO*, *UNDP*, *JICA*, *Sida*, *UN HABITAT*, *AfDB*, *TASAF*, *NORAD*, BENKI YA DUNIA, *RAK GAS TANZANIA*, *EU*, pamoja na wale wote ambao kwa bahati mbaya hatukuweza kuwataja. Tumepata faraja kubwa sana kwa michango yao kwa maendeleo ya

nchi yetu, tunaahidi kuienzi na kuiendeleza na kuithamini michango hiyo.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein; kwa kuniamini na kunipa dhamana ya kuiongoza Wizara hii pamoja na miongozo yake mbali mbali anayoendelea kutupatia ambayo ina lengo la utendaji wetu katika kuimarisha sekta zetu muhimu zenye kugusa maisha ya kila siku kwa wananchi wetu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, naomba nitoe shukurani za pekee kwako Mhe. Spika, Mhe. Mwenyekiti wa Baraza, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako kwa kunisikiliza kwa utulivu na umakini wa hali ya juu.

Mhe. Naibu Spika, shukurani maalumu nazitoa kwa ndugu yangu Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira Mhe. Juma Makungu Juma kwa mashirikiano yake makubwa anayoendelea kunipa katika kuongoza Wizara hii. Vile Vile shukurani kwa Katibu Mkuu Ndugu Ali Khalil Mirza, Katibu Mtendaji Kamisheni ya Ardhi, Wakurugenzi, Mameneja, Afisa Mdhamini, Wenyeviti wa Bodi, Mahakimu na Maafisa wa ngazi zote ambao walinipa mashirikiano yao ya hali juu kwa wakati wote na kutuwezesha kutekeleza malengo na majukumu yetu kwa ufanisi katika kipindi cha mwaka 2015/2016.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, napenda kuishukuru sana familia yangu, mama, baba na mwanangu kwa msaada wao mkubwa ulioniwezesha kufanya kazi zangu vizuri katika kipindi hiki kigumu kwangu kilichonikabili katika maisha yangu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, naomba waheshimiwa wajumbe wa Baraza lako Tukufu wayapokee, wayajadili kwa kina, watushauri na kutuelekeza na hatimae wayapitishe makadirio haya. Tunaimani kubwa kuwa michango ya waheshimiwa wajumbe wa Baraza lako hili itatusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu ya kazi vizuri zaidi katika kipindi kijacho cha mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza programu kuu na programu ndogo nilizozieleza, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe matumizi ya jumla ya Tsh Bilioni 57,456,186,000/= na pia naomba idhini ya kukusanya mapato ya Tsh Bilioni 6,100,000,000/= kutokana na vianzio mbali

mbali vilivyomo ndani ya Wizara yangu kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. *(Kwa ufafanuzi zaidi ninaomba muangalie kiambatanisho "H1, H2 na H3")*

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.(*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri nikushukuru sana, hongera sana.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya hotuba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, sasa tutamsikiliza Mhe. Mwenyekiti. Lakini mimi kwa sasa nitaondoka hapa na nitampisha Mhe. Mwenyekiti wa Baraza atakuja kuendelea na sisi kwa siku leo. Kwa hivyo tukijaaliwa tutaanza kuchangia ninafikiria kuanzia kesho au kama leo watachangia si zaidi ya watu wawili ninafikiri hivyo. Kwa hivyo baada ya hapo niwashukuru sana kwa utulivu wenu. Ninamkaribisha sasa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alikatia kiti

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe sasa ninamwita Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. (*Makofi*)

Mhe. Hamza Hassan Juma: (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi: Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa upande wangu ninataka tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa wingi wa rehma na mwenye kurehemu ambaye aliyeumba Mbingu na Ardhi, ametujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo tukiwa ndani ya Baraza lako tukufu, tukitekeleza majukumu yetu mbali mbali ya kuwatumikia wananchi wetu ambapo leo tunajadili Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2016/2017.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, Kwa dhati kabisa, napenda pia kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, Nichukue nafasi hii pia kumpongeza Waziri na Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira Mhe. Salama Aboud Talib, Mhe. Juma Makungu Juma pamoja na Katibu Mkuu wa wizara hii alhaj Alkhalil Mirza pamoja na watendaji wengine wote wa Wizara hii kwa

mashirikiano yao ya dhati kwa Kamati wakati wote tulipokuwa tukipitia na kujadili Bajeti ya Wizara hii. Tunawashukuru sana.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, Aidha, napenda kuipongeza tena Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa kuweza kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa umahiri na ufanisi mkubwa katika mfumo wa bajeti unaozingatia programu *"Program Based Budget"*(*PBB*).

Mhe. Mwenyekiti, **s**itakuwa nimetenda haki iwapo nitaendelea na hotuba hii bila ya kutoa shukurani za pekee kwa Waheshimiwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati yangu, ambao tumeshirikiana kwa umoja wetu kuyapitia na kuyachambua makadirio haya ya Bajeti ya Wizara hii na hatimae kuyakubali bila ya marekebisho yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa kuheshimu, kuthamini na kutambua mchango wao mkubwa kwenye Kamati hii hadi kufanikisha kazi hii iliyokusudiwa, naomba niwataje kwa majina Waheshimiwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati hii ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma	Mwenyekiti
2. Mhe. Suleiman Sarhan Said	M/Mwenyekiti
3. Mhe. Abdalla Ali Kombo	Mjumbe
4. Mhe. Nassor Salim Ali	Mjumbe
5. Mhe. Said Omar Said	Mjumbe
6.Mhe.MohammedrazaHassanaliMohammedali	Mjumbe
7. Mhe. Bahati Khamis Kombo	Mjumbe
8. Mhe. Kadija Omar Kibano	Mjumbe
9. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Mjumbe

Na ninawaomba Wajumbe wa Baraza hili tumuombee dua mwenzetu huyu aweze kupata afueni ili aje kushiriki katika shughuli zetu, kwa sababu kipindi chote cha kamati mwenzetu huyu bado ameeendelea kuugua na tumuombee basi Mwenyezi Mungu ampe afua.

1. Ndg. Fatma Omar Ali	Katibu; na
2 Ndg. Himid Haji Choko	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Baraza la Wawakilishi iliiidhinishia Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira Matumizi yenye

jumla ya Tshs. 7.198, 900,000 bilioni kwa ajili ya Fungu N01 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Aidha, Baraza pia liliidhinishia Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kutumia jumla ya Tshs. 28.750,560,000 bilioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo. Vile vile, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara iliidhinishiwa kukusanya jumla ya Tshs. 4,799,625,000 bilioni kama ni mapato yatokanayo na vianzio mbali mbali katika Taasisi zake, ambapo hadi kufikia Machi, 2016 Wizara ilikuwa imeshakusanya jumla ya Tshs. 3,596,948,678 ambazo sawa na asilimia 75% ya makadirio kwa mwaka

Mhe. Mwenyekiti, imeelezwa katika hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa mwaka huu wa fedha 2016/2017 Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwamba imepangiwa jumla ya Tshs.9,555,400,000 bilioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Tshs. 47,900,786 bilioni kwa ajili ya kazi za maendeleo. Aidha, Wizara inakadiriwa kukusanya jumla ya Tshs. 6,100,000,000 bilioni kutoka katika vianzio mbali mbali vilivyomo katika Taasisi zake.

Aidha, katika utaratibu mpya wa Bajeti inayozingatia Programu (*PBB*), Wizara hii imepangiwa kutekeleza Programu Kuu Nne (4) na Programu Ndogo Nane (8). Kama zilivyofafanuliwa wakati hotuba ya Mhe. Waziri alipokuwa anawasilisha hapa Barazani.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu kama Kamati nyingine imefanyakazi ya kuipitia na kuichambua bajeti hii katika mazingira magumu kwani imekubali kupitisha mipango na bajeti zake bila ya hata kwenda kukagua na kuona hizo shughuli zilizopangwa kutekelezwa hasa kutokana na kuchelewa kuanza shughuli zetu Barazani katika kipindi hiki lakini nnaamini kua kwa Bajeti ijayo tutaweza kumsaidia sana Mhe.Waziri kwa kumpa ushauri mzuri katika kufanikisha majukumu yake. Kwani wakati huo tutakuwa tumepata nafasi ya kutosha kuweza kuipitia wizara na taasisi zake kuweza kujua changamoto zake na kuweza kuwashauri ili kuweza kuendeleza wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu pia inasisitiza Wizara kuwa makini sana na matumizi ya fedha zitakazoingizwa katika Programu hizo kwani licha ya uhaba wa fedha, matokeo ya fedha zitakazoingizwa yatahitaji kuonekana na kupimwa kwa umakini na ufanisi mkubwa hususan katika utekelezaji wa Programu hizo Muhimu.

PROGRAMU YA USIMAMIZI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI

Mhe. Mwenyekiti, kama ilivyoelezwa Programu hii kuwa ina jukumu kubwa la kuhakikisha kunakuwepo upatikanaji wa Huduma bora za Nishati, Umeme na Maji katika Visiwa vyetu hivi viwili kwa upande wa Unguja na Pemba pamoja na visiwa vidogo vidogo vinavyoishi watu hapa Zanzibar, kuzingatia na mahitaji ya wananchi wetu. Aidha, kupitia Programu hii ya utekelezaji wake ni Usimamizi wa usambazaji wa mafuta nchini, Usambazaji wa huduma za umeme, Uhifadhi wa maeneo ya vianzio vya maji, Upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa watumiaji wa mijini na vijijini.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu kupitia Programu hii inapenda kuchua fursa hii tena kuwapongeza Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kupitia Mamlaka ya Maji (ZAWA), kwa jitihada zao kubwa za kuhakikisha kuwa hadi wananchi wanaoishi vijijini kuwa wanapata huduma ya maji safi na salama. Kama tunavyojua kwa upande wa usambazaji maji vijijini kwa hivi sasa Zanzibar inaongoza kwa Nchi za Afrika Mashiriki na katika Kusini mwa Bara la Afrika kwa kuwafikishia huduma ya maji huko vijini, pamoja kwamba bado kuna baadhi ya vijiji bado havijafanikiwa kupata huduma hii lakini kupitia mradi wa uchimbaji visima wa Raas-El-Khaima tunategemea kwa kipindi kifupi tu cha hapo baadae basi wananchi wengi zaidi wataweza kupata huduma ya maji safi na salama katika vijiji vyao.

Aidha,changamoto kubwa tunayoiona kwa kuvikamilisha visima hivyo kwasababu mkataba wake na Ras El Khaima ni kuchimba visima tu lakini huduma nyingine za ununuzi wa *Pump* na usambazaji wa mabomba ni jukumu la SMZ, jambo ambalo bado kutokana na gharama kubwa linaweza kuchukua muda mkubwa kuweza kukamilisha visima hivyo ili kuweza kufanikiwa kutoa huduma hiyo kwa wananchi, kwa kua hivi sasa visima vingi tayari vimeshachimbwa kupitia mradi huo na uwezo wa Serikali kupitia Mamlaka ya Maji kwa hivi sasa ni mdogo kuweza kukamilisha visima hivyo, basi tunamuomba Mhe. Waziri kufanya safari maalum kwenda Raas-El-Khaima ili kufanya mazungumzo zaidi ili Serikali ya Raas-El-Khaima ili waongeze mkataba mpya wa kusaidia kusambaza maji kupitia visima hivyo, kwani lengo la mradi huo ni kuwaondolea wananchi tatizo la upatikanaji wa maji kwani maji yameshapatikana lakini hayajawafikia wananchi kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizo za Serikali kuwasogezea huduma ya maji safi na salama wananchi wake, lakini bado kuna wananchi ambao wanajenga karibu na vianzio vya maji na kupelekea uhaba wa upatikanaji wa maji lakini pia kuchafua maji kutokana na uchafu wa majumbani mwao.

Mhe. Mwenyekiti, kama tulivyoeleza upatikanaji wa maji safi mijini na vijijini umepiga hatua kubwa lakini bado kwa Mkoa wa Mjini/Magharibi hususani Wilaya ya Mjini Unguja bado tatizo la upatikanaji wa maji limekua ni tatizo kubwa kwani kuna baadhi ya maeneo upatikanaji wake ni mdogo sana jambo ambalo linawafanya wananchi wengi kununua maji na wengi wao ambao hawana uwezo lakini vile vile pia kutokuwa na uhakika wa ubora wa hayo maji ambayo wanayonunua kwa sababu hawawezi kujua yametekwa wapi. Kamati yangu inataka kujua vipi ule mradi wa Japan kupitia Mkoa Mjini/Magharibiambao ulitegemewa kuliondoa tatizo hilo sijui umefikia hatua gani kwa hivi sasa. Pamoja na changamoto mbali mbali zinazoikabili Mamlaka ya Maji kwa kua kamati yangu haikupata muda wa kuweza kukagua na kujua matatizo ya Mamlaka hii naomba kamati yangu ipewe muda tunaamini kwa mwaka ujao baada ya ukaguzi tutaweza kuishauri vizuri serikali kupitia Mamlaka ya Maji, ili kuhakikisha wananchi wote ambao mtandao wa maji, basi wanaweza kupata huduma hii ya maji safi na salama kama ilivyokusudiwa.

Mhe Mwenyekiti, kamati yangu inaitaka Mamlaka ya Maji kwa kushirikiana na masheha, kuandaa utaratibu wa mawasiliano ya karibu, ili kutoa taarifa ya mabomba yanayovuja maji, kwani kuna maeneo mengi hapa mjini mabomba ya maji huwa yanavuja maji kwa muda mrefu bila kufanyiwa ukarabati kwa wakati, na hii pia hupelekea maji mengi kupotea na kuwakosesha wengine kupata huduma hii muhimu kwa binaadamu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kamati yangu inaitaka Mamlaka kuweza kuwaajiri vijana ambao wapo Wizarani kwa muda mrefu, na wengine wana dhamana muhimu lakini bado wapo kama wafanyakazi wa muda bila ya kuajiriwa. Hii inaweza kupelekea kutokua waaminifu na kuweza kufanya udokozi kwani hawana uhakika wa ajira yao. Hivyo, kamati yangu inaitaka tena Mamlaka kuweza kuwapatia posho la usafiri linalostahiki, kwa watumishi wao ambao hupangiwa kufanya kazi mashamba na vijijini, kwani mshara wao sehemu kubwa huutumia kwa usafiri wa kwenda kutoa huduma kwa wananchi mbali mbali, jambo ambalo huwarudisha nyuma katika mipango yao ya kimaisha.

Mhe. Mwenyekiti, pia kamati yangu kupitia Programu hii, inaiomba wizara husika kuwaongezea uwezo na ujuzi watendaji wa Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) katika utendaji wao wa kazi za kila siku. Ili kuweza kuondokana na kadhia ya utendaji wa kazi kimazoea, hali ambayo hupelekea kuikosesha serikali au shirika mapato na ufanisi katika kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na mafanikio makubwa yaliopatikana katika maeneo yetu ya mjini na vijijini kwa Unguja na Pemba. Kamati inaishauri

Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) kuanzisha utaratibu maalum wa ulipaji wa ada ya maji, kwa kutumia njia ya simu za mkononi, ili kuweza kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato ya huduma ya maji, kwani wakati mwingine mtu huwa anaona taabu ya kufuata maeneo ya kulipia maji, lakini kupitia huduma ya simu ya mkononi ni wakati wowote anaweza kulipa bila ya usumbufu wa aina yetote, na hii pia itaweza kuliongezea shirika ukusanyaji wa mapato. Pia kamati yangu inaitaka mamlaka kuboresha huduma zao za ulipaji bili za maji, kwani inaonekana hauko salama sana na unashawishi mkusanyaji kuweza kuchota fedha, kwani pesa ina bilisi mbaya.

Pia tunaishauri Mamlaka ya Maji kutengeneza *Database* ya wateja wake wote ambao wanaopata huduma ya maji, ili kuweza kuwa na uhakika wa makusanyo yao wanayoyarajia kuyapata kwa kila mwezi. Katika utaratibu huo, wanaweza kuweka utaratibu wa kulipa kwa mwaka au kila miezi mitatu na shirika linaweza kuokoa fedha nyingi kwa kupitia utaratibu huu. Pia katika kuboresha mapato na kudhibiti matumizi ovyo ya maji, basi kamati yangu inashauri Mamlaka iendeleze ule mpango wake wa kununua mita za kusomea maji, ili kuweza kuhakikisha kwamba maji yanayotumiwa yanapata malipo yanayostahiki.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inaishauri Mamlaka ya Maji kwa kuweka mabomba yalioimara, ili kuweza kuwarahisishia wananchi kupata huduma hizo kwa urahisi. Pia kubadilisha yale mabomba ya zamani yaliyochakaa, na baadhi yao yamekua yakivujisha maji, na mengine hata spea zake zimekua taabu kupatikana kwenye soko kwa hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu haijaridhika hata kidogo kutokana na kiwango kidogo cha makusanyo ya ada ya maji ambapo kama alivyoelezea Mhe. Waziri kuwa kati ya malengo waliyojiwekea kukusanya Tshs. 5.1 bilioni, hadi kufikia mwezi Machi wameweza kukusanya 1,9 bilioni kiasi cha asilimia 37% tu. Kiasi hiki ni kidogo sana kwa hiyo tunaitaka Mamlaka kuhakikisha kwa mwaka ujao wanaweza kukusanya pesa zote walizokadiria na kama nilivyoelezea hapo mwanzo, kamati yangu inaahidi kutoa msaada wa mawazo na fikra mpya ili kuhakikisha kwa mwaka ujao lengo hili linafanikiiwa kwa 100%.

SHIRIKA LA UMEME

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inalipongeza sana Shirika la Umeme Zanzibar kwa kuweza kuwapatia huduma ya umeme wananchi wote wa Zanzibar mijini na vijini, kama ilivyo huduma ya maji, serikali yetu kupitia Shirika la Umeme

imeweza kuwasambazia huduma hii Wazanzibari karibu, asilimia 80 ni mfano wa kuigwa katika nchi za Afrika ya Mashariki, Kusini pamoja na Kati.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na huduma hii hasa vijijini wananchi wengi wamekua wakijiongezea mapato kupitia biashara mbali mbali, ikiwemo sekta ya uvuvi. Pia kamati yangu inalipongeza Shirika la Umeme kwa kuweza kuwapatia wananchi huduma wa uungaji wa umeme kwa njia ya mkopo, kwani hali za wananchi wetu hasa vijijini za kiuchumi ni duni, na kupitia huduma hii wameweza kuwaungia na kuwakata katika bili zao za kila mwezi.

Vile vile kamati inaishauri wizara kukaa pamoja na Shirika la Umeme, ili kuweza kutafuta mbinu mbadala ya kulitatua tatizo la foleni katika vituo vinavyotoa huduma za uuzaji umeme, hususan kwa Wilaya ya Mjini (Unguja). Aidha, kamati inaishauri wizara kupitia Shirika la Umeme, Zanzibar kuongeza vituo vya uuzaji umeme katika maeneo mbali mbali ya mjini na vijijini, ili wananchi waweze kuondokana na usumbufu huu wa huduma ya umeme.

Mhe. Mwenyekiti, pia kamati yangu inaliomba Shirika la Umeme kurejesha tena ile huduma ya ulipaji wa umeme kwa njia ya siku ya mkononi, huduma ambayo ilikua inapunguza foleni na usumbufu kwa wananchi wengi, lakini sasa wananchi wamerudi tena katika foleni. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri kwa kupitia Shirika la Umeme kurejesha kwa haraka sana huduma ile ili kuweza kuwaondolea wananchi usumbufu.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo, kamati yangu haikusita kuishauri Shirika la Umeme, Zanzibar kuanzisha kituo kimoja cha kuuzia umeme kisiwani Pemba katika mji wa Chake Chake, Ili kuweza kuwasaidia wananchi kupata huduma hii ya malipo ya umeme kwa wepesi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kamati pia inasikitishwa na taarifa za ucheleweshwaji wa mapato, kutoka katika taasisi za serikali ya Zanzibar na baadhi ya taasisi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo yangeliweza kulisaidia Shirika la Umeme katika kutimiza majukumu yake ya msingi, ambalo linachangia kwa kiasi kikubwa kudhoofisha kazi za Shirika la Umeme hapa Zanzibar, ikiwemo kutoa huduma kwa wateja wapya na kulipia madeni makubwa yanayoikabili Shirika la Umeme kutoka Tanesco. Kwa kuwa kamati yangu inaamini taasisi zote zinaingiziwa fedha katika vifungu vyao, ambazo wanatakiwa kulipa bili ya umeme, kamati yangu kwa bajeti inayokuja haitokubali kuipitisha bajeti ya wizara yoyote, ambayo inadaiwa na Shirika la Umeme, kwani wanalipa mzigo mkubwa wa madeni shirika ambalo linatoa huduma ya umeme kwa hasara kutokana na bei wanayouziwa na Tanesco.

Kwa hivyo, kamati inatoa angalizo hili kwa Mawaziri wote, kwani shughuli zao bila ya umeme, basi hawawezi kutoa huduma katika taasisi zao. Ili kuweza kuondoa kadhia hiyo bado kamati yangu inaitaka Shirika la Umeme kuwawekea mita za Tukuza wizara zote, ili kuliwezesha Shirika la Umeme kufanya kazi zake kwa ufanisi na kuondokana na mzigo wa madeni wa kila siku kutoka Tanesco. Kwa kuwa katika Bajeti ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Mhe. Waziri wa Fedha wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, alieleza kuwa madeni na bili zote za umeme kwa taasisi za Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, hivi serikali kupitia Wizara ya Fedha zitalipwa moja kwa moja kutoka kwenye vifungu vya wizara.

Kamati yangu imefarijika na mpango huo, kwa hivyo namuomba Meneja Mkuu wa Shirika la Umeme, kumuandikia Katibu Mkuu Wizara ya Fedha wa Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kuhusu deni inalodai Jeshi la Wananchi wa Tanzania, na kuwajulisha kuwa malipo mengine yalipwe moja kwa moja kwa Shirika la Umeme Zanzibar, na sio kupitia kwa JWTZ, kwa sababu wao wanapata huduma kutoka Shirika la Umeme Zanzibar. Kwa hivyo, hili namuomba waziri alifanyie kazi kwa kupitia *ZECO*. Kamati yangu hadi tunaandika ripoti hii Shirika la Umeme inazidai taasisi hizo za serikali karibu shilingi bilioni 30, taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na za Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kweli hili ni deni kubwa sana, nawaomba waheshimiwa tulisaidie shirika letu, ili kuweza kulipwa pesa zao, ili liweze kutuhudumia ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Pemba kamati yangu inaishauri serikali kuwavutia wawekezaji katika kisiwa cha Pemba, ili kuweza kusaidia kununua huduma ya umeme, kwani shirika linapata hasara kubwa kila mwezi kwa kulipa gharama kubwa kwa Tanesco kwa umeme katika kisiwa cha Pemba kulingana na mapato yanayokusanywa katika kisiwa cha Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo kamati yangu inalitaka shirika kujiandaa na upatikanaji wa gesi asilia hapa Zanzibar, ili kuweza kuzalisha umeme kwa bei ndogo kupitia umeme wa gesi, kama ilivyo kwa upande wa wenzetu kule Tanzania Bara, kwani bado wananchi wetu wanapata huduma ya umeme kwa gharama kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na yote, kamati yangu inalipongeza shirika, kwa utoaji wao wa huduma kwa haraka hasa pale inapotokea hitlafu kwenye maeneo tofauti bila ya kujali wakati ikiwa usiku au mchana. Kamati yangu pia inalipongeza shirika kwa kuhakikisha wateja wote hivi sasa wanapatiwa

huduma ya umeme wa Tukuza, jambo ambalo litasaidia kuongeza mapato kwa serikali.

IDARA YA NISHATI NA MADINI

Mhe. Mwenyekiti, nipongeza idara hii kwa kutoa huduma za nishati, kwa kazi nzuri na tafiti nyingi wanazozifanya, hasa kwa upatikanaji wa umeme mbadala ikiwemo umeme wa upepo na wa *solar,* kwa kushirikiana na mashirika mbali mbali ya Kimataifa, pamoja na pongezi hizo, lakini tunaitaka Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati ya Maji na Mafuta (*ZURA*) katika kudhibiti mwenendo wa biashara ya uagizaji na uingizaji wa mafuta wawe makini sana, kwani hivi sasa kuna malalamiko mengi kwa baadhi ya watumiaji wa vyombo vya moto, hasa kwenye vipando ikiwemo magari pamoja na pikipiki, wakati mwingine huuziwa mafuta machafu na hayana kiwango, ambapo hupelekea kuwatia hasara kubwa kwa uharibifu katika mashine au injini za magari yao kutokana na mfuta machafu yasiyokuwa na viwango. Kutokana na hali hiyo, kamati yangu inaitaka wizara kuhakikisha inatafuta Kampuni ambayo itaweza kuyapima mafuta hayo na kuyakagua kujua viwango vyao vya mafuta, kama wanavyofanya wenzetu Tanzania Bara kwa upande wa Mamlaka ya Kudhibiti Mafuta (*EWURA*).

Kwa hivyo, ni vyema na hapa Zanzibar tukawa na taasisi kama hiyo ambayo itaweza kutuhakikishia ubora wa mafuta ambayo tunatumia hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala hili tunamtaka Mhe.Waziri akija kufanya majumuisho, atuelezee wananpango gani wa kuwa na taasisi kama hiyo hapa Zanzibar, ili kupunguza hasara kwa wenye vyombo vya moto, kwani hata wakipata matatizo hakuna fidia yoyote wanayolipwa aidha na Mamlaka au katika vituo vya mafuta walikopatiwa huduma hiyo.

PROGRAMU YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA NA MABADILIKO YA TABIANCHI

Mhe. Mwenyekiti, lengo kuu la Programu hii ni kuhakikisha usimamizi thabiti wa masuala yote yanayohusiana na mazingira na kudhibiti athari za kimazingira na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, hapo awali utekelezaji wa Programu hii ulikuwa ukitekelezwa na Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais na baada ya mabadiliko ya wizara, utekelezaji wa Programu hii utasimamiwa na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Programu hii iliombewa kuidhinishiwa kutumia jumla Tshs. 624,076,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Programu hii ya Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi. Aidha, kati ya fedha hizo zilizoidhinishwa ilikuwa Tshs. 174,076,000 kutoka serikalini na Tshs. 450,000,000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa kudhibiti matumizi mabaya ya kimazingira yanayoendelea katika baadhi ya sehemu kwa upande wa Unguja na Pemba. Kamati inaiomba wizara kupitia Mradi wa Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi utakaosimamiwa na wafadhili wa *UNDP, DFID* na *AFDB* pamoja na serikali yetu, kuweza kutoa elimu kwa wananchi kupitia vyombo vya habari mbali mbali juu ya umuhimu wa uhifadhi wa mazingira, na kuzisaidia jamii katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Aidha, kamati pia inaishauri kamati zote za masheha kuunda kamati za mazingira katika Shehia zao, ili kuweza kusaidia na kulinda maeneo yetu yasiharibiwe na yalindwe kwa mujibu wa Sheria za Mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu imegundua hivi sasa kuna maeneo mengi hapa Zanzibar hasa yaliyoko kwenye fukwe mbali mbali, hivi sasa yamekua yakivamiwa na maji ya Bahari na hata kwenye maeneo ambayo yalikua wanachi wakiyatumia kwa shughuli zao hasa za kilimo, na hivi sasa yamejaa maji chumvi ya Bahari hasa kwa upande wa kisiwa cha Pemba. Watu wengi wameingia kwenye umasikini baada ya maeneo yao ya kilimo kuingia maji ya chumvi yaani maji ya bahari. Kwa upande wa Ukanda wa Maisara kwa hapa Unguja hata yale maeneo ambayo tumekua tukiyatumia kwa ajili ya kufanya mazoezi kwenye fukwe, hivi yameanza kujaa maji na inakua shida kuyatumia maeneo hayo wakati maji yanapojaa.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inaomba ufafanuzi kuhusu suala la Zanzibar inavyofaidika na misaada ya kimataifa kupitia programu za Kimataifa za kusaidia hifadhi ya mazingira Duniani, kama ipo basi tungelipenda kuona ni miradi gani tunayosaidiwa, kwani tunasikia katika mikutano mbali mbali ya Kimataifa kuwa mataifa ya Dunia ya tatu, yamekua yakidai fidia ya uharibifu wa Mazingira unaofanywa na Mataifa makubwa Duniani, kupitia moshi wa viwanda vyao ambao unaharibu sana anga, hasa katika ile "*ozone layer*"ambayo inasababisha joto kali, pia husababisha mvua kubwa sana za" *el nino*" na mfano mzuri mvua za hivi karibuni zilizonyesha hapa Zanzibar zimesababisha maafa makubwa sana, lakini hatukusikia mfuko wa mazingira huo wa Dunia kuweza kuwasaidia wananchi walioathirika, kwani kuna maeneo tangu tuzaliwe hatukuyasikia kujaa maji, lakini katika mvua za hivi karibuni maeneo hayo yamekua yakijaa mvua. Hivi sasa katika maeneo mengi wananchi

wengi wanasubiri kuzama zinaponyesha mvua na kwa sababu Wazanzibari sasa hivi wameanza kuingi hofu, kwa sababu eneo lolote sasa hivi mvua kubwa zinaponyesha basi kuna hatari ya nyumba zao kuzama.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapo mwanzo kuwa kamati yangu haikuwahi kufanya ziara kwenye wizara na kuona utendaji wao, nitamuomba Mhe. Waziri akija hapa, aje atueleze kuhusu baadhi ya miradi mikubwa inayojitokeza hapa Zanzibar, hususan mradi wa ujenzi mkubwa unaoendelea hapo Mtoni Unguja, mradi ambao unafukia eneo la Bahari kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja cha michezo ya baharini na michezo mingine ya watoto. Kamati yangu inataka kujua je, ni athari gani ya mazingira inaweza kupatikana kupitia ufukiaji wa bahari katika mradi ule? Vile vile aje atueleze Je, mradi ule wa ufukiaji wa bahari, hautoathiri ule mkondo wa meli kubwa zinazopita na kuingia katika Bandari ya Malindi ya Zanzibar, pamoja na hii bandari tunayoitegemea bandari kubwa ya Mpiga Duri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa mradi huu ni mpya kwa hapa kwetu basi ni vyema tukapata taarifa sahihi kutoka serikalini, kwani katika nchi ya Dubai walipoanza kufukia Bahari na kujenga kisiwa na baadae kujenga hoteli, zilijitokeza athari nyingi za mazingira ikiwemo maji ya bahari kupanda kwenye maeneo mengine, lakini kwa kuwa wenzetu wanauwezo mkubwa kiuchumi waliweza kuidhibiti hali hiyo kwa haraka sana. Lakini hapa kwetu kutokana na hali yetu lazima tuweze kujua athari za baadae na serikali itachukua hatua gani aidha athari hizo zinapojitokeza.

PROGRAMU YA USIMAMIZI NA UPANGAJI WA MATUMIZI YA ARDHI

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa majukumu makuu ya Programu hii ni kuhakikisha kunakuwepo na usalama katika matumizi ya ardhi kwa maendeleo ya nchi yetu kiujumla. Aidha, kamati yangu inaiomba wizara husika kuwa makini katika utekelezaji wa Programu ndogo zilizomo ndani ya Programu hii kuu.

Mhe. Mwenyekiti, kama inavyofahamika kuwa moja kati ya changamoto inayowakumba wananchi wetu ni usalama wa umiliki wa ardhi zao kwa ajili ya matumizi ya ardhi kiholela, pamoja na utatuzi wa migogoro ya ardhi inayoendelea kila muda ukisonga mbele katika Mahakama zetu za Ardhi. Kamati yangu inaamini kadhia hii itamalizika pale tu mpango wa wizara kusajili ardhi yote na kuwamilikisha wahusika, basi kadhia hii itaisha kwani kuna maeneo mengi hasa kwetu vijini, kuna mashamba ambayo tumerithishwa

na wazee wetu kutokana na uzoefu tu, lakini hata wao baadhi yao hawana hata hizo hati miliki, lakini wameshajenga, wanalima na vijukuu vyao pia wanaendeleza shughuli zao kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo mpango huo utasaidia kuondoa tatizo hilo la kunyang'anywa au kuporwa wananchi ardhi zao.

Mhe. Naibu Spika. Kamati yangu imegundua kutokana na matatizo mengi yaliyojitokeza hasa kunyanganywa baadhi ya wawekezaji maeneo yao na mengine kufutwa kinyume na taratibu na mengine pia kuundiwa Kamati Teule na Baraza hili, lakini hadi leo hutukuletewa taarifa ya utekelezaji wa maamuzi ya Baraza hadi leo hatujui kilichoendelea, kwa hiyo ni vyema basi Wizara ikaandaa taarifa maalum ya utekelezaji wa maagizo yale ili kujiridhisha kua ile kazi kubwa iliyofanywa na Baraza na kutumia pesa nyingi imeleta matunda gani kwa jamii, lakini pamoja na hayo tunamuomba Waziri kuweza kuwarejeshea maeneo yao wale wawekezaji ambao tayari wanataka kuekeza kwenye Miradi Mikubwa ambayo itaongeza ajira kwa watu wetu lakini pia kuongeza wigo wa mapato yetu hasa ukizingatia kua Bajeti hii inalenga kutegemea mapato ya ndani zaidi kwa mapato ya ndani kuliko kutegemea misaada kutoka nje ambapo kwa miaka ya hivi karibu imekua na masharti magumu kuweza kuyatekeleza.

Mhe. Mwenyekiti kamati pia inaomba Kamisheni ya Ardhi kuandaa utaratibu maalum wa kutoa elimu kwa wananchi juu ya matumizi mabaya ya Ardhi na athari kwa pamoja, ili kuweza kuondokana na kadhia hii ya migogoro ya ardhi zinazouzwa na kusajiliwa kinyume na taratibu zilizowekwa kisheria. Kutokufanya hivyo, ni kuiongezea mzigo Serikali na kuikosesha mapato yatokanayo na wawekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili tunakuomba Mhe. Waziri uwe mkali hasa kwa baadhi ya waekezaji ambao wameyachukua maeneo yao kwa ajili ya uwekezaji pamoja ya kuwa Ardhi ni mali ya Serikali lakini mwananchi anapokubali kupisha muekezaji basi alipwe fidia kwa mujibu wa makubaliano na sio kutumia nguvu na ubabe katika kuwadhulumu wanyonge haki zao.

Aidha, katika jambo hili Kamati yangu haitokuwa tayari kuwaona wananchi wetu wakipokonywa haki zao za matumizi ya Ardhi zao na matajiri kwa kutumia uwezo wa kifedha waliokuwa nao, kwani na wao ni raia wa Nchi hii na ni wajibu wao kufaidi matunda ya Mapinduzi Matukufu ikiwemo kumiliki Ardhi zao. Na katika suala hili Kamati yangu inaahidi kuwasaidia wananchi wake katika kuweza kupata haki zao katika umiliki wa ardhi lakini vile vile

katika kupatiwa haki zao hasa kwa wawekezaji ambao wamechukua maeneo yao.

MAHKAMA YA ARDHI

Mhe. Mwenyekiti kamati yangu inaipongeza Wizara kupitia Mahkama ya Ardhi kwa kazi nzuri ambayo hivi sasa wanaifanya kwani kwa mwaka uliopita kati ya kesi 168 zilizoripotiwa karibu kesi 138 zimeshatolewa maamuzi ambapo kwa Unguja kati ya kesi 118 zilizoripotiwa tayari 98 zimeshapatiwa hukumu na kwa Pemba kati ya kesi 50 tayari kesi 40 zimeshapatiwa hukumu ,hapa kwa heshima kubwa Kamati yangu inaipongeza Mahkama ya Ardhi kwa kufanya kazi zao vizuri na kile kilio chetu Waheshimiwa Wajumbe wako wa Baraza hili tukufu cha muda mrefu kwa kesi za Ardhi zinachukua muda mrefu tayari zimeweza kupatiwa ufumbuzi.

Lakini tunawaomba sana Mahakimu wa Mahkama ya Ardhi waendelee kufanya vizuri na kuwa waadilifu kama walivyoanza kuonyesha hivi sasa isijekua ile kesi ya Mgema ukimsifu “TEMBO “ akaja kulitia maji. Aidha, pamoja na pongezi hizo tunawaomba Mahakimu wa Mahkama za Ardhi kujitahidi kuwa waadilifu katika kuendesha na kutoa hukumu hizo kwani mara nyingi kesi hizo hutawaliwa sana sana na vishawishi vya matajiri kutaka kuwadhulumu haki zao wanyonge kupitia Mahkama hizo kwani wanyonge hawatokuwa na uwezo wa kuhonga ili kujiokoa na kunyang’anywa ardhi zao na mapapa ambayo yako vinywa wazi kwa gharama zozote ilimradi waweze kuwanyang’anya haki za wananchi wanyonge kwa kuwatumia Mahkama hizo. Kwa hiyo, Mahakimu wajue kuwa wamebeba dhima kubwa kwa Mwenyeenzi Mungu kwani ardhi sio jambo la mchezo hata kidogo, kwani ukisikia Mataifa makubwa Duniani wanapigana vita basi sababu kubwa ni kutaka kunyang’anya Ardhi za Nchi na nchi.

PROGRAMU NDOGO YA UPANGAJI WA MIJI NA MATUMIZI YA ARDHI

Mhe. Mwenyekiti Kamati yangu pia inaipongeza Idara hii ya Mipango Miji na Vijiji kwa kuandaa upangaji upya wa Miji na Viji pamoja na matumizi bora ya Ardhi, ili kuwawezesha wananchi wetu kuweza kufaidika na matumizi bora ya ardhi kiuchumi na kijamii kwa maeneo yote ya Zanzibar. Pamoja na pongezi hizo Mhe. Waziri ameeleza kwenye kitabu chake kuwa Idara ya mipango miji tayari imeshapanga maeneo matatu ya wazi katika Eneo la Kibandamaiti, Eneo la Daraja Bovu na Eneo la Kiembe Samaki kupitia mfuko wa *(Urbarn Development Fund)* tunamuomba Mhe. Waziri akija kufanya majumuisho

atuelezee kuwa ni uboreshaji gani ambao unaokusudiwa kufanywa katika maeneo hayo aliyoyataja kwani wananchi wengi hawaijui mipango hiyo ili na wao kujitayarisha kukabiliana na changamoto zozote zitakazojitokeza wakati wa utekelezaji wa mipango hiyo ambayo maeneo hayo sasa hivi wananchi wanayatumia katika shughuli mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, Pia, Mhe. Waziri katika kitabu chake ametuelezea kwamba katika mradi mpya wa mpango mkuu wa matumizi ya Ardhi, *(Zanzibar Town Master Plan)*kuwa kwa hivi sasa kitovu kikuu cha Mji Mkuu wa Zanzibar kinahama kutoka Mji Mkongwe na kuhamia maeneo ya ng'ambo bila shaka shughuli nyingi za za kijamii, maofisi kiuchumi na kibiashara na sehemu za mapumziko zitaongezwa na kuimarishwa katika maeneo ya ng'ambo ambapo kaulimbiu yake ni *"Ng'ambo Tuitakayo"*mpango huu kwa kweli ukifanikiwa utaiongezea haiba mji wetu wa Zanzibar kwani hivi sasa mji upo kienyeji sana na hata majengo yake hayailetei haiba nzuri mji wetu. Hivyo, tunaiomba Idara kuendelea kutoa elimu kwa wananchi ili waweze kujua mipango yenu ili na wao waweze kutoa maoni yao na pia kutoa ushirikiano wakati wa utekalezaji wa mpango huo. Pia, Kamati yangu inaishauri Idara kuweza kuchora ramani ya mji wetu utakavyokuwa na kuweka mabango *(Bill Board)* makubwa sehemu zenye mikusanyiko mikubwa kwenye maeneo hayo ili wananchi kuona nikitu gani kilicholengwa kufanywa hapo baadae kama wanavyofanya nchi za wenzetu.

PROGRAMU NDOGO NA USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA UJENZI NA NYUMBA

Mhe, Mwenyekiti kama alivyoelezea Mhe. Waziri program hii inatekelezwa na Idara ya Ujenzi na Shirika la Nyumba, Kamati yangu inaipongeza Idara kwa kazi walizozifanya katika kipindi hiki ikiwemo usafishaji wa makaro na uzibuaji wa mabomba ya maji machafu katika nyumba zetu za maendeleo, pamoja na uandaaji wa michoro mbali mbali ya ujenzi usajiliwa wakandarazi mbali mbali na hizi zote zinahitaji utaalamu mkubwa kwa hiyo iko haja ya kuwalinda na kuwapa maslahi bora watumishi wa Idara hii ili waweze kufanya kazi zao vizuri zaidi kutokana na utaalam wao.

PROGRAMU NDOGO YA UHIFADHI NA UENDELEZAJI WA MAMLAKA YA MJI MKONGWE

Mhe. Mwenyekiti Kamati yangu pia inaipongeza Mamlaka ya Uhifadhi Mji Mkongwe kwa kuendelea kuulea na kuuweka Mji Mkongwe kuendelea kuwa na hadhi yake kuwa ni mji kati ya Miji Mikongwe Duniani ambayo ni urithi wa

kimataifa, sisi Wazanzibari tunapaswa tuulinde na tuuhifadhi kwa pamoja mji huu kwani ni sehemu ya kivutio kikubwa Duniani ambapo unaitangaza Zanzibar na kuweza kuwavutia watalii wengi pamoja na wanafunzi wakiwemo watafiti mbali mbali ambao hufika Zanzibar ili kuja kufanya shughuli zao za kitalii na kimasomo. Kwa maana hiyo, tunawaomba sana wale wote wanaoishi na kufanya shughuli zao za kimaisha za kila siku kuhakikisha kuwa wanatunza mazingira lakini pia kuhakikisha urithi huu haupotezi hadhi yake, kwa hiyo tunamuomba sana Mkurugenzi aendelee kusimamia na kuulinda mji wetu ili usije kupoteza hadhi yake kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaipongeza tena Idara kwa kutafuta mradi wa ujenzi wa ukuta wa uzio wa Bahari hapo Mizingani ambapo Kamati yangu inatarajia kuwa baada ya kumaliza ujenzi huo basi utaweza kubadilisha haiba ya Mji wetu ili kuongeza kuvutia Mji wetu na pia kuongeza shughuli za kibiashara na kiuchumi ambapo tunategemea pia kutaongeza shughuli za ajira katika eneo hilo.

Mhe. Mwenyekiti Kamati yangu inapongeza pia jitihada za Mamlaka ya Uhifadhi Mji Mkongwe, kwa kufanikisha upatikanaji wa ufadhili wa ukarabati mkubwa wa jengo la Beit-el-Ajaib kupitia Serikali ya Oman. Aidha, Kamati yangu inamuomba Mkurugenzi asichoke kufuatilia mradi huu kufuatilia uharakishwaji wa ujenzi kwa muda uliopangwa, kwani tangu nyumba hiyo ilipoporomoka jengo hilo limeikosesha Serikali mapato mengi ambayo yalikua hupatikana kupitia ada ya jengo hilo. Pamoja na hayo, Kamati yangu inaitaka Serikali baada ya kukamilika ukarabati huo basi kuwe na mfuko maalum ambao utakusanya mapato ya jengo hilo ili ziweze kusaidia kurekebisha pale patakapo leta khitlaf yoyote kwani makosa tuliyoyafanya kwa mapato yanayokusanywa huingia katika mfuko mwengine ambapo zikihitajika inachukua muda mwingi kupatikana.

UKARABATI WA JENGO LA CHAWA DARAJANI

Mhe. Mwenyekiti kamati yangu inaitaka Mamlaka ya Mji Mkongwe kusimamia karibu karibu waukarabati wa ujenzi ule kupitia mfuko wa Hifadhi ya jamii *ZSSF* kutokana na umuhimuwa shughuli za uchumi kwa wananchi wetu katika jumba hilo. Aidha, tunaziomba taasisi zinazohusika na ujenzi huo kuhakikisha ukarabati huo unaenda kwa haraka ili wale wananchi waliokuwa wakifanya shughuli zao katika jengo hili waweze kurejea tena ili waweze kuendelea na shughuli zao za biashara kila siku, kwani katika kipindi cha ukarabati huo kutaleta usumbufu mkubwa kwa wao na familia zao lakini kama tunavyojua shughuli maendeleo pia huleta changamoto ndani yake.

Kwa hivyo tunawaomba wananchi kuwa wastahamilivu katika kipindi hichi kigumu, pamoja na hayo tunaiomba tene Idara husika kuhakikisha wale wadau ambao walikuwepo mwanzo wenye maduka na wapangaji waliokuwepo mwanzo waliokuwa wamepanga katika zile nyumba na biashara na shughuli zao mbali mbali basiu baada ya kukamilika ujenzi ule waweze kurejeshwa wale wale na kama yatakuwepo maeneo ya ziada basi waweze kutafutwa wengine, isijekuwa mtu anaondolewa halafu ujenzi unakamilika wanatolewa wanawekwa watu wengine

Vile vile, Kamati yangu inapongeza Mamlaka kwa kuanzisha utaratibu wa kuratibu na kuyasimamia maeneo ya wazi na kuyasajili Katika Mji Mkongwe kwani katika miaka ya hivi karibuni kumekua na utaratibu wa uvamizi wa maeneo ya wazi aidha kwa kujengwa au kufanya shughuli neingine za kijamii na kibiashara na inapofika mtu kuondolewa basi anakua mkali hataki kuondoka na jambo hili mwisho hupelekea kuharibu ile haiba ya Mji mkongwe. Kamati yangu inaendelea kuiomba Mamlaka kuhakikisha hizo sehemu za wazi zilizobakia zinaendelea kuhifadhiwa ili kuwapa wananchi wengi fursa kuweza kuzitumia na sio kuwamilikisha watu na kuweza kuzitumia kwa shughuli zao binafsi. Pamoja na yote Mamlaka hii inafanya kazi zake vizuri na tunampongeza sana Mkurugeni kwa Usimamizi wake imara.

Mhe. Mwenyekiti, Mwisho kabisa kama nilivyosema nawapongeza tena Wajumbe wa kamati hii kwa kuweza kunisaidia sana na kunipa mashirikiano katika kipindi chote ambacho tumepitia bajeti ya Wizara hii.

Lakini kama nilivyoeleza mwanzo Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu haikupata nafasi hata ndogo ya kuenda kukagua idara yoyote katika Wizara hii, kwa hiyo kuna changamoto nyingi ambazo zinaikabili Wizara Mhe. Mwenyekiti, nitaomba waheshimiwa wachangie wakosoe, walekeze na baadae tuipitishe bajeti hii. Kamati yangu ina ahadi kwa kila kwenye changamoto basi kamati yangu itazichukua na itakapokuwa tunapangiwa kazi na kiti chako Mhe. Spika, tutakwenda kuzifanyia kazi.

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, nikiwa muwakilishi wa jimbo la Shaurimoyo nitaomba kidogo nipate japo dakika chache niweze kutoa maoni au vilio vya wananchi wangu katika Wizara hii. Kwanza tunaipongeza sana Wizara hii kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya na nashukuru katika baadhi ya maeneo katika jimbo langu la Shaurimoyo yale yaliiyokuwa hayapati maji kuna baadhi yao wameanza kupata maji, lakini bado kuna changamoto kubwa hasa katika eneo la Shaurimoyo yenyewe na changamoto hii Mhe. Mwenyekiti inaninyima sana usingizi wananchi wangu wanapokuja nyumbani kwa

kunilalamikia kwamba maji hawapati ya kutosha. Na kwa kuwa mimi ndio mwenyekiti wa kamati hii kwa kiasi fulani siwezi hata kupiga buti na kuzuia fungu la Wizara hii, lakini namuomba sana Mhe. Waziri basi tukishamaliza shughuli zetu hizi basi aniruhusu kwa muda mwingi sana katika shughuli zangu za jimboni nimtumie sana Mkurugenzi wa Mamlaka ya maji kumpitisha katika maeneo mbali mbali kwa kushirikiana na Masheha wangu ili kuangalia zile changamoto hasa katika mwezi huu mtukufu wa ramadhani.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wangu wanaendelea kupata tabu kwa kweli nataka suala hili tuweze kuhakikisha linakuwa historia na kwa bahati mbaya sana jimbo langu Mhe. Mwenyekiti, hayo maji yote yanayokwenda Mji Mkongwe hawawezi kuyapata bila ya kupita ndani ya Jimbo langu, lakini mwenyewe tunahangaika na ndoo za maji usiku na mchana. Sasa Waswahili wanasema "Mchawi au mwanga mpe mtoto alee" Mamlaka ya maji nimepewa mimi niilee basi ninaamini wataweza kunipa mashirikiano ili kuhakikisha kwamba kadhia hiyo basi inaweza kuondoka.

Lakini la mwisho kabisa la jumla Mhe. Mwenyekiti, baada ya kueleza changamoto ya wananchi wangu naomba Mhe. Waziri aniikilize vizuri sana kuna kadhia kubwa ambayo wananchi wa jimbo la Matemwe na kwa bahati mbaya wananchi wale miongoni mwao mpaka Naibu Waziri na yeye wanamgusa, kuna kadhia kubwa ya muwekezaji ni muwekezaji mkubwa ambaye sitopenda kumtaja hapa hadharani, lakini katika maeneo ambayo ameyachukua mpaka sasa hivi bado kuna kadhia kubwa ya wananchi hawajaweza kuwalipa fidia zao, na sheria zetu Mhe. Mwenyekiti kwamba eneo lolote ambalo litachukuliwa kwa maslahi ya taifa basi mwananchi atazingatiwa kwanza kabla ya ule mradi kuanza. Sasa tatizo linalojitokeza mradi umeshaanza muwekezaji huyu anawanyanyasa wananchi kitu ambacho ninachokiomba Mhe. Waziri Wizara uliyopewa ni ngumu, wizara uliyopewa ina changamoto nyingi, Wizara yako Mhe. Waziri inahudumia wananchi moja kwa moja.

Sasa naomba uwe mkali, uwe msimamizi mzuri, na usimuonee haya mtu yoyote hata mtu akiwa tajiri kiasi gani, anaponyang'anya mali za watu na yeye mnyang'anye eneo. Mhe. Mwenyekiti, kadhia hii naamini Mhe. Waziri naamini wananchi wameshamfuata kwa sababu na mimi kama mwenyekiti wamenifuata lakini waliponifuata tayari nimeshaandika hotuba kwa hivyo nikashindwa kuweza kulishughulikia suala hili. Lakini kama nilivyosema kwa kuwa kamati yangu haikupata muda wa kupita katika Wizara kuweza kujua changamoto hili Mhe. Mwenyekiti nitaomba sana Mhe. Waziri tushirikiane kwa pamoja ili wale

wananchi wa Matemwe waweze kupata haki zao na yule muwekezaji aweze kufanya shughuli zake bila ya usumbufu wa aina yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache nashukuru kwa kuweza kunivumilia nakushukuru sana asante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Hamza Hassan Juma Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa hotuba yako nzuri na uwasilishaji mzuri.

Waheshimiwa Wajumbe tuendelee, wachangiaji ni wengi wa hotub hii, lakini kutokana na muda naona tutawapata wachangiaji watatu, na kama hali itaruhusu na muda utaruhusu tunaweza tukaingiza na wanne. Lakini kwanza ninamuomba Mhe. Shadya achangie, ameniomba dakika tano lakini afuatie na Mhe. Jaku na Mhe. Nadir ajitayarishe na Mhe. Abdalla Diwani kama muda utaruhusu.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuweza na mimi kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa pumzi zake mchana huu nikaweza kusimama katika Baraza lako Tukufu nikiwa katika hali ya uzima na afya njema.

Mhe. Mwenyekiti, Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu naomba tena niendelee kuchukua nafasi hii kuwapa pole wananchi wa Mkoa Kusini Pemba kwa mitihani inayowakuta hususan wananchi wa Jimbo la Kiwani, naomba wazidi kuwa na subira wakiamini kwamba Mwenyezi Mungu yuko pamoja nao.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nianze kuchangia hotuba yangu hii kwa kuanza kusema kwamba sitounga mkono hotuba hii lakini naona kwamba sitomtendea haki Mhe. Waziri kwa vile yeye ni mpya kwa wizara hii. Kwa hivyo nimuombe tu Mhe. Waziri baada ya kuchangia tukutane tuzungumze ili tumpe mambo ya hapa na pale katika wizara yake na vile vile nianze kwanza kwa kumpa pole kwa kupewa wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu nitaanza kwenye ukurasa wa 19 wa hotuba hii ya Mhe.Waziri, na kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu ninukuu.

"Programu ndogo ya uratibu wa usimamizi wa shughuli za ujenzi wa nyumba za Serikali. Mhe. Mwenyekiti, programu hii ndogo imetekelezwa na Idara ya Ujenzi na Shirika la Nyumba ambapo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 shughuli zifuatazo zimetekelezwa; kuzifanyia matengenezo nyumba za maendeleo Unguja na Pemba.".

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kwa dhati kumpongeza Rais wetu wa mwanzo Mhe. marehemu Mzee Karume Mwenyezi Mungu amlaze pema peponi na amjaalie kila la kheri huko aliko.

Mhe. Mwenyekiti nimesema haya kwa sababu natambua kwamba mzee wetu huyu alijenga majumba haya ya maendeleo kwa ajili ya wananchi wake ambao hali zao ni duni kimaisha, akaona iko haja ya kuwajengea majumba haya wananchi hawa na kuweza kuishi. Lakini jambo la kusikitisha Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa wananchi hawa ambao wanaishi katika majumba yale, wameweza kupandishiwa kodi kubwa mno, na tukiangalia kwamba wananchi wetu hali zao za maisha ni ngumu, mwananchi huyu anatakiwa alipie maji, alipie umeme na bado hajatafuta kijio.

Kama nilivyosema wananchi wetu hali zao ni duni na uchumi wetu tunaufahamu. Kwa hivyo tu nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja hapa anieleze, walipokaa katika kutafakari suala hili la kupandisha hizi kodi, walizingatia viwango vya wananchi wetu wanaokaa katika majumba hayo. Kwa sababu kama nilivyosema kuna wananchi wetu bado maisha yao yako chini na wao hali zao ni duni. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri atakapokuja katika majumuisho anipe ufafanuzi kidogo wa suala hili.

Halafu vile vile Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri katika huu ujenzi wa nyumba za serikali. Katika mji wa Chake Chake kuna kijiji kinaitwa Kilimatinde, pale pana jumba la serikali ambalo linahatarisha maisha ya watu, jumba lile ni bovu sana, limeshaanguka si mara mbili, tatu na wakati limo katika mikono ya serikali, namuomba Mhe. Waziri akija anieleze wana utaratibu gani hususan kwa jumba lile ili lisije likaleta maafa zaidi kwa wananchi wetu.

Nikitoka katika ukurasa wa 19 Mhe. Mwenyekiti, naomba niende ukurasa wa 24 Mamlaka ya Maji. Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba uniruhusu kidogo ninukuu.

"Mhe. Spika, sekta ya maji inaendelea kutoa mchango mkubwa katika ustawi wa jamii zetu mijini na vijijini katika kuimarisha afya za wananchi kwa matumizi ya majumbani".

Kama hivyo ni sawa Mhe. Mwenyekiti, nataka nimueleze Mhe. Waziri, naamini amefanya ziara nyingi na tumemuona kwenye vyombo vya habari, na tunapata taarifa zake lakini tu nataka nimwambie, kuna visima vyetu Pemba bado ni vichafu Mhe. Waziri, visima hivyo vinasafishwa *pump* tu, lakini vile visima hasa havisafishwi, na tunasema maji safi na salama na tukiangalia maji ni uhai wa mwananchi. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri jambo hili alichukulie hatua ipasavyo.

Niingie katika ukurasa wa 34, Shirika la Umeme. Mhe. Mwenyekiti, vile vile kwa ruhusa yako naomba uniruhusu ninukuu kidogo.

"Mhe. Spika, Shirika la Umeme ni taasisi inayohusika na usimamizi na usambazaji wa huduma ya nishati ya umeme hapa nchini, kwa lengo la kuimarisha upatikanaji na usambazaji wa nishati hiyo kwa ufanisi".

Mhe. Mwenyekiti, kama hivi ni kweli Mhe. Waziri alivyosema kuhusu Shirika la umeme, kwa hivyo nataka nimwambie Mhe. Waziri kama Shirika la Umeme, katika Shirika lililooza ni Shirika la Umeme, nasema hususan katika kisiwa cha Pemba kuna matatizo mengi Mhe. Waziri mengine tutakuja huku tuzungumze, lakini nasema hivi kuna kijiji kimoja cha Chambani, katika wiki mbili za nyuma zilizopita kulikuwa na utaratibu wa kuzimiwa umeme asubuhi mpaka jioni, hatujui kuna tatizo gani au pana nini pale, na wananchi wanakosa kuangalia kupata habari, ambalo ni jambo muhimu la kikatiba mwananchi kuweza kuona na kupata taarifa za nchi yake.

Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri na hili vile vile akija atujuze kulikoni katika kijiji kile cha Chambani, muda wa asubuhi kikakosa umeme mpaka jioni kuna tatizo gani.

Mhe. Mwenyekiti, halafu niendelee na mchango wangu. Tunafahamu kwamba likizo ni kitu cha lazima kwa wafanyakazi wote inapofika muda anatakiwa mfanyakazi yule achukue likizo na mfanyakazi yule anachukua likizo. Lakini mfanyakazi yule amekwenda likizo mpaka amemaliza hajapewa pesa zake za likizo, namuomba Mhe. Waziri nalo atueleze, kulikoni wafanyakazi hawa wa Mamlaka wameshakwenda likizo wamesharudi wameshaanza kazi pesa za likizo hamna.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, mfanyakazi anafanya kazi, na anapokea mshahara na katika mshahara wake ule ule kuna kiwango wanachokatwa kinachopelekwa *ZSSF*, ambao ni manufaa yake mwenyewe baadae, baada ya kwishakustaafu ziweze kumsaidia. Lakini kuna malalamiko kwamba huu mwezi wa tano wafanyakazi wa Mamlaka wanakatwa pesa hizo na pesa hizo hazijafika *ZSSF*. Naomba Mhe. Waziri atakapokuja anieleze kulikoni, ni taratibu zipi zilizosababisha pesa zile zisiingie au pana nini?

Mhe. Mwenyekiti, halafu suala jengine naomba nimueleze Mhe. Waziri kama analitambua au halijui basi mimi nataka nimueleze kuhusu magari.

Tunafahamu kwamba wafanyakazi wa mamlaka lazima wawe na usafiri kwa ajili ya shughuli zao za kazi, kwa sababu shughuli zao ziko vijijini na sehemu mbali mbali. Kwa maana hiyo lazima wafanyakazi wale wanahitajika wawe na usafiri, lakini sasa hivi magari ya mamlaka yamelala, ukiuliza unaambiwa hakuna mafuta, pesa hamna wanakochukua mafuta sheli ya Tibirinzi wamefungiwa hawalipi, sasa hivi wameelekea sheli ya Michakaini, tunaomba Mhe. Waziri na hapa tujue kulikoni pesa hii ya mafuta haifiki Mamlaka pana kitu gani?

Halafu mwisho Mhe. Mwenyekiti, unanitizama unaangalia dakika zako, namalizia kutaka kumwambia Mhe. Waziri katika kisiwa cha kijiji cha Wambaa pana kisima ambapo pana barabara, kipindi cha nyuma alikubali kwamba barabara ile itatengenezwa kwa ajili ya kurahisisha kazi za kwenda pale kwenye kisima kile cha Wambaa ili wananchi wasipate tabu. Lakini mpaka hii leo kibarabara kile bado hakijatendewa kazi wala hakijaulizwa.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia 95 mpaka hapo Mhe. Waziri atakapokuja kunijibu nitammalizia tano yake. Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru wewe kwa kuniruhusu na nitakuwa sijafanya haki kama sijamshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kusimama hapa nikaweza kupumua kwa pumzi zake, ameniazima na sijui saa ngapi atazihitaji. Huu si ujanja wangu wala uwezo wangu, ni neema yake kubwa Mwenyezi Mungu, *alhamdulillah*.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Waziri mpya, na Wizara nyeti aliyoipata, na Naibu Waziri wake lakini sifa pekee za aina yake

zimuendee Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndugu Ali Khalil Mizra. Katibu Mkuu ambaye katulia ni miongoni mwa Makatibu bora.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na Kamisheni ya Ardhi Mazingira. Nashukuru Mhe. Mwanasheria yupo, leo nimefurahi kweli kweli, kitengo kile tulipitisha sheria humu ndani lakini kwa masikitiko sijui tuseme Waziri aliyekuwepo au wanasheria waliokuwepo kule tena kama kunishukuru wanishukuru sana mimi watu wa Kamisheni, kwa kuwazindua katika usingizi mzito waliokuwa wamelala, wamekaa pale bila sheria na wakawa wanachukua mishahara bila ya sheria, ama kuna msemo *shari imo ndani ya tumbo la kheri*.

Mimi ndiye niliyekuja kuwaokoa pale na Mwanasheria kwa ufundi wake aliokuwa nao wa wanasheria akastiri hali ile, wala halina mjadala wala halina *objection* kwa hilo. Kamisheni imekaa pale kinyume na utaratibu wa nchi hii na ikasokota watu. Sasa sijui kama waziri aliyekuwepo pale kasahau majukumu yake, wanasheria walioko pale wamesahau majukumu yao.

Naomba unisikilize sana kwa makini Mhe. Waziri na nikupe pole sana kwa wizara hii, wizara ambayo mawaziri wengi wamefeli sio mchezo, wizara nyeti Mhe. Mwenyekiti, kazungumza. Nikuombe pale tutakapokupigia simu Mhe. Waziri usifikiri kama tunahitaji kiwanja au ardhi, tunakupigia tuna majukumu hasa suala la maji. Ukishatoka BLM au ukatoka pahali iangalie simu kakupigia nani uturudishie.

Kulikuwa kuna kilema kwa waziri aliyepita. Kwa hivyo Mhe. Waziri nikuombe sana utakapopigiwa simu utapotoka baadae angalia kapiga nani, usifikiri mtu anataka kibali, mtu anataka ardhi, ni suala la maji, na sisi majukumu yetu kukusaidia wewe Mhe. Waziri, tuwe makini tupo kwa niaba ya wananchi.

Kamisheni ile imekaa pale sijui kwa kitengo gani, lakini baadae imefika hatua tena ikasawazishwa, wamesokota watu na pengine watu walikula hasara kitengo kile. Tumepitisha sheria humu ikawa haikwenda.

Vile vile Mheshimiwa nilikuuliza swali, hapa kumekuwa na usumbufu wa kitengo kile mimi shahidi, wananchi huchoka kupanda ngazi wakifanya mazoezi bila ya kutaka, narudia tena msemo huo ile si hisani wala ni fadhila, ni wajibu wao kuwatumikia wananchi wa nchi hii. Kuna *lease* ishaandikwa, mimi nishajua kila kitu kishatakiwa mpaka leo mwenyewe hataki kupewa.

Sizungumzi kwa kubahatisha Mhe. Naibu Waziri ni jamaa yangu wewe, nafikiri nikianguka ndio wa mwanzo kuweza kuniokota mimi ukanipeleka

Muyuni. Kwa hapa Maalim Haroun hayupo, lakini unaweza ukanichukua ukaenda ukanipeleka Muyuni.

Mhe. Waziri kwetu ni kumoja, nakuheshimu na nitaendelea kukuheshimu, lakini hebu tufike tunawafanyia nini wananchi. Ulijibu swali hapa juzi na nitahitaji maelezo yako naomba ninukuu Mheshimiwa.

Mhe. Waziri ni wazi kwamba hapo nyuma kweli kulikuwa na madudu mengi ambayo yalikuwa hayapendezi, na wawekezaji walisumbuliwa sana, na mtu tayari hati anayo hata bila ya kupewa *notice*. Sasa uje unambie Mhe. Waziri haya madudu kayafanya nani na hatua gani ndio tutatumbua yale majipu haya? Haya uwe makini sana na Kitengo cha Kamisheni.

Chengine pale pale Kamisheni pana Kitengo ya Uhaulishaji sijui nini kazi yake, nilikuwa nina msemo mimi binadamu humalizi maneno yote mengine uweke hakiba. Kitengo cha Uhaulishaji nini kazi yake, Mhe. Waziri uje utueleze nini kazi yake, na nani ana haki ya kuhaulishiwa ardhi yake, ana sifa gani, pamekuwa pana mateso na usumbufu kitengo kile.

Cha kusikitisha mtu mmoja pale ana kofia nne, akikukosa huko anakuja kukukamata huku, akitoka huku anakuja kukukamata huku, tunakwenda kweli? Mtu mmoja pale ana kofia nne katika kitengo kile, anakutafutia sababu ukatoka huku anakuja kukamata huku, ukatoka anakuja kukukamata huku ndio, utawala bora huo, mtu mmoja kushika nafasi nne, tano pale?

Mengine sitaki kuyasema itapofika wakati nitayazungumza, lakini nini maana yake kitengo kile kuhaulisha nani anaghushiwa, mtu anakuwa ana haki zote za kuhaulisha sababu unaweza kupewa utacheka mpaka utaanguka, sijui tunakwenda wapi.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala la maji, Mheshimiwa hapa hapana msalie mtume, hasa suala la maji, na wananchi wa Michamvi hapana msalie mtume Mheshimiwa kwa hili.

Historia naomba isije ikanihukumu huenda ikarudia tena humu ndani wiki iliyopita ikanikuta, historia huenda ikanikuta tena, na niko tayari. Nazungumza wazi mchana historia itajiandika tena. Wananchi wa Michamvi tokea uhuru miaka 52 wamekosa nini kwenye serikali hii kukosa maji? Cha kushangaza hata huu mwezi wa Ramadhani hamjapeleka gari hata moja, huja mkatangaza kwenye *radio* usanii mtupu.

Hapa Mhe.Waziri ninakuheshimu sana, sana, lakini hapa hapatoshi, wananchi wale wa Michamvi wamekosa nini, tokea dunia kuanza mpaka leo hawajanywa maji kutoka kwenye mfereji au bomba, napeleka mimi, wala sitaki kujisifu, kaulize kule shilingi ngapi natumia kwa mwezi, sitaki kukwambia, kaulize, tokea muda niliokaa mwezi wa Oktoba mpaka leo tena napeleka gari tatu kwa siku hazikidhi, kesho ninapumzika siku nyengine napeleka, nawakisia. Sizungumzi kwa kutaka kujisifu, si wajibu wangu, wajibu wa serikali, mimi kazi yangu kuja kuwatetea hapa ndio wajibu wangu, ni wajibu wa serikali, si wajibu wangu kupeleka kule maji.

Leo kisima kimechimbwa kule shilingi milioni mia mbili, mia tatu serikali inashindwa hapa, Mhe. Waziri pana shughuli pevu sana. Lakini nitakuwa sijafanya haki kama sijamshukuru Mkurugenzi Mkuu wa Maji, Sheikh Mustafa, nimshukuru kwa dhati jitihada anazozifanya ni kubwa mno, na nimshukuru msaidizi wake Mkurugenzi Maulid wamenipa mashirikiano makubwa sana, sana, na wenyewe wanajua. Lakini kama sikuwashukuru mafundi wawili; fundi anayeitwa Njuma na fundi Haji Said nitakuwa sijafanya haki.

Hivi sasa Jambiani maji hayatoki, na Mungu asijejaalia kipindupindu hiki maji ya Jambiani ni chukwa, ni machungu tunaita kule, pampu imeharibika nimeshawaambia wanambie pampu shilingi ngapi ili wananchi wasije wakapata matatizo kipindi hiki cha Ramadhani na kipindupindu na maji ya Jambiani hayafai.

Nilisema humu ndani kuna milango mitatu ya kuingilia; na nitaendelea kusema, Jimbo la Wananchi, Jimbo la Uteuzi wa Ikulu au Viti Maalum. Michamvi mimi nime-*spend* karibu milioni ishirini naa, kuna mradi wa maji ya chumvi kufanya maji matamu tayari nimeshachimba msingi mimi hakuna kitu mpaka leo. Cha kusikitisha nilifanya biashara nikupeni hadithi ndogo, nilifanya biashara moja tumekwenda Arusha mimi na yeye, ninamdai miaka 10 hataki kunipa hivi, basi likavamiwa na majambazi akanambia zile pesa hizo hapo chukua leo, majambazi si wakataka kuninyang'anya zile pesa, ndio nilichofanyiwa jana, mazingaombwe Michamvi.

Nimefanyiwa mazingaombwe jana Michamvi, pana ule mradi unaenda kufunguliwa maji leo kwa kuwa leo ni bajeti. Nitakubali wapi mimi? Siwezi kukubali kwa kuwa leo bajeti eti jana wananchi pale wamekwenda kudanganywa maji dakika mbili tatu, siwezi kukubali. Hili historia huenda ikajirudia tena ya kipindi kifupi kilichotokea juzi.

Miaka 52 ya uhuru mpaka leo hatuyapati maji, tena kuna mahoteli chungu nzima; kuna vitega uchumi tunawafanyia nini. Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi kwenda namna hii, wananchi wanateseka suala la maji miaka 52 karibu mpaka leo maji yale hayajatoka.

Nije kwenye Shirika la Umeme. Shirika la Umeme lina mtihani hasa katika uuzaji wa umeme imekuwa inawasumbua wananchi vibaya sana, mara kadhaa mimi humpigia simu Mkurugenzi wakati mwengine hapokei, wakati mwengine yupo vikaoni inawezekana. Lakini ile si sadaka wanayotoa pale wala msaada. Mtu anakunyima pesa zake inafika mtu anapanga foleni, vituo vitatu kweli mjini vitatosha kuuza umeme? Hatuwezi kwenda namna hii. Mtu anapanga foleni Michenzani mpaka barabarani kule anakosewa kupondwa na gari.

Juzi ilikujakufanywa miundombinu tu iko wapi baada ya miundombinu mmoja ule hakuna mwengine. *Simultaneous equation* hesabu ina *method* mbili ya ku-*solve,* inabidi tukafeli ile hakuna njia nyengine wananchi wateseke.

Shirika la Umeme bado hamjajipanga, na sijui ule mradi wenu wa Zantel umekwenda wapi, kama mnadaiwa au umekufia njiani ulikuwa ukasaidia watu ule. Hatuwezi kufika kwa namna hii, bado hamjajipanga, hata mtu akija kuungiwa umeme anachukua muda, utafanyiwa hesabu ya nguzo hizo, maana yake sijui hizo nguzo gharama zake humu humu kwenye majibu ya serikali utaambiwa serikali inawajali wananchi wake haiogopi hasara. Tunafanya nini humu humu ndani, *hansard* tunazo, serikali haiogopi hasara kutumikia wananchi wake, kumbe tunakuwa tunazungumza mdomoni tu vitendo ni tofauti. Tunataka kufa kuzimia tunaogopa, uzimie ndipo ufe, hivyo hatuwezi kwenda.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Mahakama ya Ardhi. Nimepigia kelele sana hili jengo halifai na usalama wake ni mdogo, hauridhishi, hiyo ngazi yenyewe ukiipanda unaomba dua mpaka ukafika, na ukiteremka unaomba dua, mbao zinalia vile ukipanda, jengo lile ni bora lifungwe.

Jengine la kusikitisha jumba lililokuwepo Marikiti. Mimi naishukuru serikali kwa nia yake nzuri inayofanya, lakini serikali ilikuwa haijawa tayari kujenga lile jengo mpaka hivi sasa. Nilikuja kuuliza mimi *permit* yake iko wapi, kumbe hamna. Tumeenda kuwaondosha wafanyabiashara mwezi wa Ramadhani sasa hivi tumewekeza mabati tu pale *construction* hamna, na tuko hapa hapa, nije nioneshwe *permit* iko wapi, *permit* ya ujenzi haijatoka pale.

Mhe. Mwenyekiti, Ramadhani hii watu wana wake zao, wana watoto wanategemea maisha muda huu kwa nini tusiwaachie, imekuwa ni hadithi ya nyoka mdimu. Nyoka mdimu kukaa kwenye mdimu yeye huwa hana kazi nazo lakini ukienda kuzichuma anakurukia, hadithi yenyewe ndio hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku malizia una dakika kama mbili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naheshimu muda wako.

Mhe. Mwenyekiti, hii ndio hali ilivyo, Kamisheni jipangeni msiwasumbue wananchi, ule si msaada hamtaki kumpa mtu kitu basi msimpe, tukaja kuzungumza mengine hayatoshi.

Suala la umeme narudia tena bado wananchi msiwanyanyase, wana haki kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar. Kuna suala la msikiti sasa hilo ndio ninahitaji maelezo kule Mombasa umezuiwa kujengwa kwa sababu gani? Mhe. Waziri naomba usikilize kwa makini, ile ni nyumba ya ibada, kiwanja mtu mwenyewe amejitolea, nilihoji Wizara ya Katiba na Sheria jawabu halikuja, na sikuhoji kwa kuwa ndio wahusika maana yake wajue kama pana sheria nchi hii zinafuatwa au vipi.

Msikiti wa pale Mombasa mwezi huu mtukufu wa Ramadhani unataka kujengwa jamaa ameshalipa, halmashauri ina kibali, ilimradi mnatusokota na kutuzonga. Wizara ya Ujenzi iko kwengine sasa pale ndani pana vibali na kuna vitengo vitatu, kwa nini hamumpelekei Mhe. Ali Karume, yeye ndiye mwenye dhamana ya ujenzi ilimradi ametoka mwananchi huku anakuja anasokotwa huku. Ah! Nini tunafanya?

Mhe. Mwenyekiti, dhamana ya ujenzi ni Mhe. Ali Karume hivi sasa, leo kitengo kipo pale, vibali utapanda ngazi na kama utakuwa mzee basi unaweza ukaanguka mule ndani. Ni kwamba tunawasumbua wananchi, sio utawala bora huu, mimi sizungumzi kwa kubahatisha Mhe. Mwenyekiti, haya tunayaona na yanatukuta.

Watendaji wako juu hao hapo na waje wanisute mimi kama nazungumza uongo, unajua ukiisimamia hoja wala hupati shida, lakini kitengo kile sasa Kamisheni, kibali sijui halmashauri, iwekeni pahali pamoja tu, kama mnataka mapato kachukueni kule kwa Mhe. Ali Karume ndiye mwenye dhamana ya ujenzi sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, naheshimu muda wako lakini suala la maji la Michamvi naiomba tena serikali kwa hili, mimi nimechukua dhamana na nitaenda kuulizwa kwa Mwenyezi Mungu nimewatumikia vipi wananchi, wamenichagua ili nije kuwasemea, si wajibu wangu mimi kupeleka maji. Mimi nimepewa dhamana na nitaenda kuulizwa kwa Mwenyezi Mungu nimewatumikia vipi wananchi wangu, hiki cheo ni dhamana. Nakushuku sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Alwardy: *Bismillahi Rahman Rahiim*. Namshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia uzima kwa kuhudhuria hapa pamoja na wajumbe wote kwa ujumla.

Vile vile nimpongeze Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kufanya uteuzi wa Waziri wa wizara hii pamoja na Naibu Waziri, naamini hawatomuangusha na ninavyoamini mimi kwa kuwaona na kuwajua ni watendaji wazuri na waaminifu.

Vile vile Katibu Mkuu wake wa wizara hii ni muaminifu kama wao pamoja na Wakurugenzi wa Mji Mkongwe wako vizuri sana kwenye kutenda kazi zao. Mimi hata siwajui lakini nawasifu kwa sababu ya kazi zao, na nawasifu Mawaziri na Manaibu Mawaziri walioteuliwa kwa sababu ni watu wazuri na watu waaminifu.

Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda kwenye kuchangia hoja na nitazungumzia mambo manne, nitaingia kwenye ardhi, itafata maji na nishati halafu kama nitawahi na mazingira. Lakini naomba nimueleze Mhe. Waziri wa Ardhi kwamba hii wizara yake hapo nyuma kuna baadhi ya mawaziri walikuwa majambazi, sio mawaziri. Nasema dhahiri kwa sababu nina ushahidi, mawaziri baadhi yao waliopita ni majambazi, wameitumia wizara ile kuibia watu na kufutia watu *lease* bila ya hata yeye mwenyewe kujua kama amefutiwa *lease*.

Nampongeza sana wakati ule Katibu Mkuu aliyekuwepo na nafikiri ndiye huyu huyu pengine ni mtendaji mzuri lakini kuna mambo anashindwa kwa sababu wale mabaka wakubwa wana nguvu zaidi. Lakini kwa kushirikiana na waziri huyu aliyeteuliwa na Mhe. Rais na Naibu Waziri wake kwa utendaji wao, naamini sana watamsaidia Mhe. Rais na hatopata jina baya nje, kwa sababu mawaziri waliopita baadhi yao wanamtia mpaka Mhe. Rais jina baya kwa ule wizi wao.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye suala la ardhi kuna ma-*investors* wamefutiwa *lease* bila ya wao wenyewe kujua wakati wanalipia, wanafanyiwa mambo ya

kienyejienyeji tu, kwa kuwa mtu tu ana nafasi au labda ana shemeji yake anatumia nguvu kwenye masuala haya.

Vile vile kuna maeneo ya ardhi za watu wengine wananyanyaswa, wazee hasa wa vijijini, watu wazima kwa kuwa tu labda waziri yule au mkubwa yule ana mtu wake anawaondosha watu kiholela tu katika maeneo yale, wapo wengi wanalalamika hawakulipwa inavyotakiwa, hivyo wamedhulumiwa.

Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri aliyekuwepo na Mhe. Naibu Waziri wake, kwa uaminifu kabisa wale walionyang'anywa ardhi zao wajitahidi kadri ya uwezo wao waje wawarejeshee, naomba sana suala hili, na wale waliofutiwa *lease* wengine tayari yale maeneo yameshajengwa na ma-*investors* wengine waliopewa na wale wizi waliopita. Sasa wawatafutie maeneo wawape mengine, ili waje wapate kujenga wale wasihisi hii serikali ni serikali ya watu ambao inadhulumu, wakati hii serikali haimdhulumu mtu. Mhe. Mwenyekiti, ni mtu mmoja tu ndiye aliyesababisha yote.

Mhe. Mwenyekiti, nina ushahidi wa watu watatu wamefutiwa *lease,* wanalipa na wenyewe hawajui, wanakuja kuambiwa baadae tu kama ilitoka barua wakati yeye mwenyewe hajaipata.

Vile vile nina eneo moja nilikwenda Pemba ambalo amepewa huyu *investor* wa Mauritius alilifuta Mhe. Mansour namtaja kwa jina. Kwa hiyo, alilifuta na huu wote ametumia madaraka yake vibaya, akalifuta hili akampa jamaa wa Mauritius ameshajenga hoteli kubwa, na hili suala mpaka lishakuja kwenye Kamati ya Baraza la Wawakilishi, lakini cha kushangaza wale watoto yatima mpaka leo waliodhulumiwa eneo lao hawajarejeshewa wakati waliambiwa wachague Kiwani Pemba ama Michamvi.

Mimi nilikwenda nikashuhudia suala lile, na nikalifuatilia mpaka Michamvi ameshaangalia yule kijana ambaye yatima aliyedhulumiwa hajapewa eneo mpaka leo, na kauli haijatoka mpaka leo ya kukabidhiwa eneo lake.

Namuomba sana Mhe. Waziri hapa hakitopita kitu kama hatujafahamiana kuhusiana na hili suala ambalo limefanyika, na nataka aje anipe maelezo mazuri sana, na Mhe. Mwenyekiti namshukuru sana kasema hajapita huko na angepita nafikiri hata hiyo hotuba yake asingeileta leo angeona haya mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile ningemuomba Mhe. Waziri aangalie sana ardhi zile ambazo ziko tupu, akashirikiana na *ZIPA* ili wakaziweka tayari kwa wale ma-

investors, wanapata shida wanapokuja kutaka ku-*invest* hawajui hata waanzie wapi na waende wapi. Washirikiane na *ZIPA* ili muweke maeneo na mutenge kabisa mtu anapokuja mnampa, haina haja mtu akija unataka kujenga hoteli gani *five star*, eneo lako linaweza likakufaa hili, chagua unataka lipi dili inakwenda. Lakini tukienda tu hivi kiholela holela, na mimi nakuaminini mliochaguliwa ni viongozi wazuri sana pamoja na Katibu wenu Mkuu na Wakurugenzi wenu ni wazuri sana. Mimi naamini wizara hii itaenda vizuri lakini hiyo wizara ya nyuma ilikuwa haifai hata kutajwa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile namuomba Mhe. Waziri azungumze na viongozi wake wanaopitisha au kuhalalisha zile *documents* ambazo mtu amenunua kiwanja mpaka kupata *documents*. Kwa kweli usumbufu ni mkubwa, mambo ni marefu, mpaka mtu anafika kusamehe zile *documents* au kwenda kuulizia kutokana na kupanda na kushuka kama alivyozungumzia Mhe. Jaku.

Mhe. Mwenyekiti, ninachoomba kuja kujua mpaka hivi sasa kuna *documents* ngapi, au kuna watu wangapi ambao wameshapewa hati wanazomiliki ndani ya Unguja na Pemba kama ardhi zao. Ni wangapi mpaka hivi sasa wanaoishi kwenye nyumba zao na viwanja vyao bila ya hati yoyote. Naomba sana uje unijibu utapokuja kufanya majumuisho yako.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba uje unijuulishe katika hawa mawaziri niliozungumza, mamba walioiba, ni ardhi ngapi ambazo zimedhulumiwa kupewa watu na ngapi zimefutwa *lease* kiholela, uje unieleza bila ya kumuonea mtu haya, kwa sababu sasa hivi ni wakati wa kufanya kazi, hapa ni kazi tu.
Pia Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein yuko safi kabisa kwa kila kitu, najua binadamu hakukamilika lakini nitamtolea asilimia 5 lakini 95 yuko vizuri. Kwa hiyo, nakuomba sana Mhe. Waziri uje unijibu, ni viwanja vingapi waliodhulumiwa watu kufutiwa *lease* na mumechukua hatua gani na hawa mawaziri waliodhulumu mali za watu mtawachukulia hatua gani.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi nitaenda kwenye mada yangu ya pili mambo ya maji. Hili suala la maji kwa ufupi ni nyimbo. Kweli kuna sehemu yanapatikana lakini naweza kusema zile sehemu zinazopatikana maji, sehemu nyingi za matajiri matajiri na viongozi. Ukiangalia Mbweni hatuna shida ya maji kwa kuwa tunakaa Mawaziri, Manaibu Waziri, Mwakilishi, Makamu, lakini ukienda kwengine mpaka maji yana uchafu hili ni jambo la kusikitisha.

Mhe. Mwenyekiti, tunapofanya maendeleo siwalaumu wizara hii mpya na Katibu wake, nalaumu wizara zilizopita, tunapofanya maendeleo basi tuwatizame kwanza hao wanyonge kuliko wenye pesa. Sisi viongozi kama

tunajiweza tutanunua wenyewe, tutachimba visima, tutatia ma-*pipe*, lakini kwa wale wanyonge tunawaumiza halafu tunawaambia walipe, walipe nini wakati *service* hakuna?

Mimi Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri nawapendekeza sana kwamba wale wanyonge waendewe mbio hasa wale wanaoishi shamba pamoja na Jimbo langu la Chaani, wapite kote wakahakikishe wananchi kwanza wale wanyonge wanapata maji vizuri na wanapitishiwa *service* vizuri halafu ndio tutizame mengine. Lakini leo pengine watu wanakunywa maji yenye mavi ndio wanapata kipindupindu, huo ni mtihani. Haya mambo tunacheka lakini si ya kucheka, wakati mwengine yanasikitisha, kwa sababu wale wanyonge hawafikiriwi.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile ningemuomba sana Mheshimiwa, mimi sitaki kuzungumza sana kwa sababu muda haupo, lakini nitachangia kwenye nishati sasa.

Mhe. Mwenyekiti, hii nishati naomba sana viongozi wenzangu kwa ujumla, Wawakilishi wote tuje tuipitishe sheria hii ya gesi na petroli ili nchi hii basi angalau tuje tufanane na hiyo Dubai na Singapore na Oman, Kuwait na Qatar ambazo ni nchi ndogo kama hii lakini ndani ya miaka 25 au 30 nyuma sisi nchi yetu ni nzuri mara mia kuliko wao, tumeanza kutangulia mwanzo kuliko wao. Lakini angalia leo kama Dubai ina mafuta asilimia 4 tu lakini vipi ile nchi imejijenga, na sisi *in sha Allah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tutapochimba haya mafuta, tunao uwezo wa kuja kujenga kuliko wao, kwa sababu sisi tutakuwa na mafuta mengi, lakini na sisi wenyewe tuwe safi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaomba sana tuje tuipitishe hii sheria ili tufanye kazi kwenye kuchimba mafuta na gesi, wananchi waliokuwa wanyonge watapata mishahara mikubwa, viongozi na nyinyi mkitaka kuongezewa mishahara itaongezeka kwa sababu mafuta yapo, na tuna uwezo na tutakuwa sisi hatukopi tena na hatudai, kwa kisiwa kama hiki tukitoa mafuta tutakuwa tunajiendesha wenyewe bila ya matatizo, bajeti zitapita bila ya matatizo. Lakini ikiwa kila siku tu tunazungumza hatufanyi vitendo, tunasema tu wenzetu wameshatoa gesi sisi hatutotoa gesi mpaka tutakufa sote hapa.

Mhe. Mwenyekiti, masuala ya *diesel* sasa hivi cha kushangaza *petrol* duniani *50 dollars per barrels*, ajabu kwamba hapa japokuwa ni serikali inajitahidi sana na naipongeza sana kupunguza mafuta kujitahidi kuwatia *pressure* wale wakashusha mafuta bei. Lakini sasa hivi kwa mujibu wa bei ya mafuta duniani yalikuwa angalau haya mafuta yawe 1,200, lakini cha kushangaza zaidi mpaka

leo 1,800 au 1,900. Je, hii *barrel* ya oil ikija ikafika dola 115 tutakuja kuuziwa 5000 lita moja hapa. Kwani hapa tunaonekana dhahiri kwamba hawatiwi *pressure* na wala hawachunguzwi, tunajua dhahiri *barrel* moja ni dola 45 au dola 50 lakini tuachilie bado bei zile zile tu za maajabuajabu. Wazishushe ikija ku-*peak* hii *barrel* kufika dola 115 basi lita moja watakuja kusema wanataka kuuza 5000 na serikali itakuwa haina maneno kama ilivyokuwa sasa hivi, wanatiwa *pressure* lakini hawajawa-*pressurized* zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile hawa wafanyabiashara kuna kampuni tatu zinatuuzia mafuta, ya Bakhressa naipongeza sana ina mafuta mazuri, ina wafanyakazi wazuri na waaminifu. Lakini hii Kampuni ya *GAPCO* na *ZP* wanachakachua kweli kweli kwenye mafuta, na wale wenye gari zao nzuri wanapotia pale mafuta yana maji na wafanyakazi wao ni wezi kweli kweli, ukizubaa kama mafuta ya shilingi 20,000 usipoangalia unapokwenda pale kutia mafuta 20,000, basi wakitia mafuta 15,000 hawaiondoshi kwenye ile *system* yao, ukienda wewe ukisema unataka kutia 20,000 wanakujazia ile 5000 ya juu unatoa shilingi 20,000. Tena huwa wanashirikiana, wana mtandao mkubwa kampuni hizi mbili, mimi nishazikamata mara tano nimeshagombana nao, mimi binafsi wameshaniibia mara tano.

Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi wa kampuni zile natuma salamu kwa mabosi wao wanaomiliki waweke wafanyakazi waliokuwa waaminifu wasiibie watu, sio wote wanaojua suala lile la kuangalia, wengine hawajui, mtu anajiona ameshatia lita 20 kumbe ametiliwa lita mbili. Na mtindo wa kuchakachuliwa mafuta hizi kampuni iundwe tume maalum Mhe. Waziri nakuomba, ili kwenda kuchunguza mafuta yale na kuyapima, watu binafsi, leo Zanzibar wana magari mpaka shilingi milioni 250,000,000, waheshimiwa viongozi wanatumia gari nzuri nzuri, na sisi wenyewe tukiwemo.

Leo gari mtu unakwenda kuharibiwa *injector* kwa mafuta ya lita mbili yametiwa maji wanachakachua kwa kufanya biashara haramu. Kwa hiyo, naomba sana Mhe. Waziri aunde tume akafanye uchunguzi, na vile vituo vyote vitakavyokamatwa vinafanya masuala hayo vifungiwe na wapewe watu wengine, wako watu tele wanataka kufanya biashara hiyo, lakini nashangaa kwamba wanaachiliwa achiliwa tu hawachunguzwi.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu wa Dar es Salaam miaka iliyopita Mhe. Kikwete gari zake saba zilizima njiani kwa sababu ya mafuta hayo mabovu…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir umebakiwa na dakika mbili.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Alwardy: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana mimi dakika mbili zinanitosha kwa leo mazingira wala siyaingii sana.

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba Mhe. Waziri na Naibu wake wahakikishe sana kwenye biashara ya mafuta inashuka kwa sababu mafuta duniani yameshuka. Na vile vile waweke tume maalum ya kuchunguza mafuta haya kwenye watu wanaouza mafuta, mafuta ni machafu, yanaharibu gari zetu kwa ujumla na hasa wanaharibia wanyonge zaidi, mtu mwenye uwezo ataweza kutia *injector*, mtu aliyekuwa hana uwezo ataenda kuweka nini. Gari imekufa matokeo yake pengine anafanya daladala anafanya mambo mengine yamekwama.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile ningempongeza sana Mkurugenzi wa Mji Mkongwe kwa kazi yake nzuri ya kusimamia mji wake, na najua kwamba ana vipingamizi vingi vinambana huko nje, lakini utendaji wake wa kazi ni mzuri.

Kwa hiyo, ningemuomba sana akahimiza lile suala la Forodhani kulikotiwa mabati kumalize ili shughuli ziende vizuri na kuzidi kupendeza, kwa sababu hali ile ya kuziba mabati hata ile hadhi ya ile *museum palace* imeondoka na baadhi ya mahoteli na vitu vyengine. Na wale wanaopita na gari vile vile wanakuwa wanahisi bado hali haiko nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la mazingira kwa ufupi tu Mhe. Waziri nakuomba sana tufanye usafi wa hali ya juu, tuoteshe miti, tufuatilie kwa ujumla na tuweke sheria ya wale wanaotupa taka au kuharibu mazingira wapigwe faini kama nchi nyengine.

Nakuomba sana weka polisi jamii bila ya malipo, wao malipo yao watakapomkamata mtu ndio alipwe na *camera* wape za dola mia mia. Mtu anapigwa picha na anachukuliwa *video* bwana huyu nimemkamata amerusha mfuko faini yake ni shilingi 50,000 shilingi 25,000 mtu aliyemkamata na 25,000 inaingia kwenye mfuko wa wizara yenu. Nalipendekeza hili ili hili suala likome, la sivyo hamjaweka sheria kama hii ya kukamatisha watu tutafanya mradi wa mazingira tutasema kila siku hatufiki kokote.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono asilimia 90, asilimia 10 yangu atapokuja kunijibu kwenye hotuba ndio nitapoimalizia. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuahirisha kikao tuna matangazo mawili.

Tangazo la kwanza Waheshimiwa wote wa Chama cha Mapinduzi mnatakiwa ukumbi wa juu kuna kikao, na la pili Mheshimiwa yeyote ambaye ameacha mzigo wake ofisi ya Mshika Fedha baadae aufate.

Kingine kesho tukijaaliwa tutakuwa na wachangiaji wa kwanza kabisa atakuwa Mhe. Abdalla Maulid Diwani akifuatiwa na Mhe. Simai Mohamed Said. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe, nawapongeza wachangiaji wote waliochangia mwanzo, na sasa hivi kikao nimekiahirisha mpaka kesho saa 3:00 asubuhi.

(Saa 9:00 jioni Baraza liliahirishwa hadi tarehe 16/06/2016 saa 3:00 asubuhi)